# Jarida la BUNGE

ISSN-085-6046 TOLEO LA TISA FEB, 2025



# "Miaka Minne ya Rais Samia"

## Bunge Lang'ara Kimataifa

## Yaliyomo




Spika Akabidhi Uenyekiti Jukwaa La Maspika EAC UK 02



Misingi ya Uratibu na Uendeshaji wa Bunge UK 10



Bunge Kinara Tuzo Za Uandaaji Bora Wa Hesabu UK 33



Azania Bunge Bonanza Lafana UK 56


*Scan hii Code kusoma na kupakua jarida hili*

# Dibaji



Ndugu Msomaji,

**Nakukaribisha kwenye Jarida la Bunge Toleo la Tisa, Jarida hili pamoja na mambo mengine limeangazia kuhusu shughuli za Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, mafanikio ya Bunge Kimataifa katika utawala wa miaka minne ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Makala nyingine elimishi kuhusu Bunge.**

Kuhusu Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, Jarida hili lina habari na makala kuhusu taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge zinasosimamia matumizi ya fedha za umma kufuatia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Jarida hili pia lina habari na makala kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026 na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26.

Aidha, Jarida hili pia lina habari kuhusu makabidhiano ya nafasi ya Mwenyekiti wa Jukwaa la Maspika wa Bunge wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na habari kuhusu tuzo ya Uandaaji Bora wa Hesabu za Mwaka 2023 katika Kundi la Wizara na Taasisi za Serikali ambayo Ofisi ya Bunge iliipata.

Pia Jarida hili lina makala ambazo zinaendelea kuchambua kwa kina Misingi ya Uratibu na Uendeshaji wa Bunge, Usimamizi wa Kibunge wa matumizi ya fedha za umma pamoja na umuhimu wa Kamati za Bunge.

Pamoja na hayo masuala mengine ambayo yameandikwa katika Jarida hili ni pamoja na Makala kuhusu Spika Mstaafu wa Bunge, Mheshimiwa Pius Msekwa, habari kuhusu Azania Bunge Bonanza, habari kuhusu ushiriki wa Bunge la Tanzania katika michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika Jijini Mombasa, Kenya na habari kuhusu mafunzo ya Wabunge Vijana.

Nawatakia usomaji mwema wa Jarida la Bunge.

Ndugu Baraka Leonard
Katibu wa Bunge.

**BODI YA UHARIRI**

**MLEZI WA JARIDA**
Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb)
Spika wa Bunge

**BODI YA UHARIRI**

**Mwenyekiti**
Ndg. Baraka Leonard

**Makamu Mwenyekiti**
Ndg. Zuhura Mtatifikolo

**WAJUMBE**
Ndg. Athuman Hussein, *ndc*
Ndg. Hanifa Masaninga
Ndg. Abdallah Hancha
Ndg. Chacha Nyakega

**WAHARIRI**

**Mhariri**
Ndg. Lawrence Raphaely

**Mhariri Msaidizi**
Ndg. Debora Sanja

**Limeandaliwa na:**
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA.
**Nukushi:** +255 26234218
**Simu:** +255 26 232276-5
**Barua Pepe:** cna@bunge.go.tz

*Scan hii Code kusoma na kupakua jarida hili*

# Yaliyomo






Miaka Minne ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan – Bunge Lang'ara Kimataifaa UK 02
Bunge laitaka TRA kukabiliana na upotevu wa mapato UK 06
LAAC: Halmashauri zashindwa kukusanya mabilioni UK 08
Misingi ya Uratibu na Uendeshaji wa Bunge UK 10






Serikali: Sehemu kubwa ya Bajeti ya 2025/26 itabebwa na mapato ya ndani UK 14
PIC yataka Usimamizi thabiti Mashirika ya Umma UK 18
Umuhimu wa Kamati za Bunge katika Utekelezaji wa Madaraka ya Bunge UK 21
Kamati: Mifumo ya ukusanyaji Kodi iimarishwe UK 25






Wabunge Vijana wapewa Mafunzo ya Uongozi na Maadili UK 27
Spika Akabidhi Uenyekiti Jukwaa la Maspika EAC UK 29
Bunge Kinara Tuzo Za Uandaaji Bora Wa Hesabu UK 33
Andaeni taarifa za utekezaji Maazimio ya Bunge - Waziri Mkuu UK 35






Bunge Lampongeza Rais Samia Kuandaa Mkutano Wa Nishati Afrika UK 37
Usimamizi wa Kibunge wa Fedha za Umma UK 40
Baraza la Wafanyakazi lakutana Zanzibar UK 44
Bunge lawaaga Watumishi Tisa Waliostaafu UK 46






Hayati Dkt. Ndugulile alivyohudumu Bungeni UK 47
Pius Msekwa: Hazina ya Bunge, Hazina ya Taifa! UK 50
Ushiriki wa Bunge la Tanzania Michezo ya EAC UK 54
Mashabiki wa Simba Waibuka Kidedea Bunge Bonanza UK 56
KONA YA MALENGA UK 53

# Miaka Minne ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan - Bunge Lang'ara Kimataifa



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan** katika picha na Spika wa Bunge, Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson**

**Na. Debora Sanja**

**Machi 19, 2025, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anatimiza miaka minne ya uongozi tangu alipoingia madarakani.**

Katika kipindi hiki, nchi yetu imepata mafanikio makubwa kwenye nyanja nyingi zikiwemo utendaji na uchumi, usimamizi na utoaji haki, na uwakilishi na utungaji wa sheria. Hayo yote yanadhihirisha umahiri wa uongozi ulioonеshwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mbali na kutimiza majukumu yake ya kikatiba, kwa mara ya kwanza limevuka mipaka na kuiwakilisha nchi kwenye ngazi za juu katika medani za kimataifa kutokana na ushawishi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Rais aliridhia nchi yetu kutoa mgombea na kumuunga mkono kwa hali na mali katika kinyang'anyiro cha urais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) ambapo Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb) alishinda nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika Oktoba 27, 2023 Luanda nchini Angola.

Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb) ambaye ameweka historia kwa kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika kushinda nafasi hiyo tangu umoja huo ulipoanzishwa mwaka 1889, alikiri kutambua na kuthamini mchango wa Mheshimiwa Rais katika safari yake ya kuusaka urais wa IPU.

Katika hotuba yake aliyoitoa wakati wa mapokezi Bungeni Dodoma, Mheshimiwa Dkt. Tulia alimuelezea Mheshimiwa Rais kuwa ndiye shujaa wa safari ya ushindi wake kwa kuridhia agombee nafasi hiyo na kumuunga mkono wakati wote wa kampeni.

Alimshukuru Dkt. Samia kwa kutengeneza rekodi ya kipekee ya uongozi wake, kwa kuwa bila yeye asingeweza kugombea na kuipata nafasi hiyo.

Kwa kutambua kuwa ushindi uliopatikana ni heshima kwa taifa letu, Mheshimiwa Rais alimpongeza Dkt. Tulia kwa nafasi hiyo na kueleza kwamba ni matokeo ya kujituma kwake katika utumishi wa umma, jambo ambalo ni mfano bora kwa watoto wa kike nchini, Bara la Afrika na nje ya Afrika.

Nafasi aliyoipata Dkt. Tulia inampa jukumu la kuwa mkuu wa kisiasa wa IPU, akiongoza mikutano ya kisheria na kuwakilisha chombo hicho katika matukio ya kimataifa. Aidha, utekelezaji wa majukumu hayo unampa Dkt. Tulia fursa ya kuitangaza Tanzania katika diplomasia na siasa za dunia, sambamba na kuimarisha uhusiano baina ya Bunge la Tanzania na Mabunge mengine duniani na hivyo kuchochea ustawi wa taifa letu.

Ndani ya kipindi cha uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nchi yetu ilifanikiwa pia kutoa mgombea wa nafasi ya Ukurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Kanda ya Afrika, hii ikiwa ni mara ya kwanza. Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Marehemu Dkt. Faustine Ndugulile, baada ya kuteuliwa na kuungwa mkono na Serikali alishinda nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika Agosti 27, 2024 Brazaville, Kongo na kushirikisha wagombea watano.

Akizungumza katika uzinduzi wa kampeni za kuwania nafasi hiyo Mei 8, 2024, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile alimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumpendekeza, na kuridhia agombee nafasi hiyo huku akiahidi kuwa Serikali itamuunga mkono katika kampeni zake.

Ushindi wa Dkt. Ndugulile ulikuwa ni sifa kwa taifa letu na Bara la Afrika, na Mheshimiwa Rais alionesha furaha yake kwa kutuma salamu za pongezi kwa Dkt. Ndugulile kwa kuchaguliwa katika nafasi hiyo akieleza kwamba, ameipa fahari nchi yetu na Bara la Afrika litafaidika na kazi yake.




> **Mheshimiwa Rais umeweka bidii kubwa sana kuhakikisha mimi, na Dkt. Ndugulile ambao tumetoka upande wa Bunge tunashindana nafasi tulizogombea na kuleta heshima kwa nchi yetu na umesikia matarajiayo ya wenzetu waliyokuwa nayo kuhusu utumishi ambao ungeenda kufanywa na ndugu yetu Dkt. Ndugulile ni kama tumekatizwa hivi.**
>
> Tunakushukuru sana na sina shaka utaendelea kuwaunga mkono watanzania wengine wanaojitokeza - *Dk. Tulia Ackson.*

Aidha, kwa upande wake Mheshimiwa Spika kwa nyakati tofauti amekuwa akielezea shukrani zake kwa Mheshimiwa Rais kwa kuwaruhusu na kuwaunga mkono watanzania wanapojitokeza kuonesha uwezo wao katika medani za kimataifa, akitoa mfano wa namna yeye na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile walivyonufaika.

Akizungumza katika msiba wa Marehemu Dkt. Ndugulile, Spika alimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuweka bidii na kuhakikisha Dkt. Ndugulile anashinda nafasi ya Ukurugenzi wa WHO, Kanda ya Afrika, jambo ambalo limeongeza heshima ya Bunge na nchi kwa ujumla.

"Nakushukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna unavyoitumikia nchi yetu na kutusaidia wananchi wa Tanzania kuonyesha uwezo wetu katika fursa mbalimbali zinazojitokeza duniani"

"Mheshimiwa Rais umeweka bidii kubwa sana kuhakikisha mimi, na Dkt. Ndugulile ambao tumetoka upande wa Bunge tunashinda nafasi tulizogombea na kuleta heshima kwa nchi yetu na umesikia matarajiayo ya wenzetu waliyokuwa nayo kuhusu utumishi ambao ungeenda kufanywa na ndugu yetu Dkt. Ndugulile ni kama tumekatizwa hivi. Tunakushukuru sana na sina shaka utaendelea kuwaunga mkono watanzania wengine wanaojitokeza" alisema Dk. Tulia.

Kwa kushinda nafasi hiyo, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile angesimamia nchi 47 za Bara la Afrika katika sekta ya afya ambapo aliahidi kuendelea kuboresha huduma za afya ili kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa nchi zenye changamoto hiyo pamoja na kuimarisha mifumo itakayowezesha kuhimili athari za magonjwa ya mlipuko na majanga mengine.

Mipango na ndoto nzuri alizokuwa anajiandaa kuzitekeleza hazikuweza kutimia kwani Novemba 27, 2024, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile aliaga dunia nchini India alipokuwa akipatiwa matibabu, ikiwa ni takribani miezi miwili kabla ya kuanza kuitumikia nafasi hiyo Februari, 2025.

Mafanikio ya Bunge katika uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan hayakuishia katika kushika nafasi za juu kwenye medani za kimataifa tu, bali hata ndani. Ni katika kipindi

hicho, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchini yetu, Bunge lilipata Katibu wa Bunge mwanamke kufuatia uteuzi wa Bi. Nenelwa Mwihambi,ndc uliofanywa na Mheshimiwa Rais Mei 15, 2021.

Uteuzi wa Bi. Nenelwa Mwihambi,ndc katika nafasi hiyo iliyokuwa ikishikiliwa na wanaume tangu kuanzishwa kwa Bunge, umeibua chachu na hamasa kwa wanawake na mabinti wenye ndoto za kuwa viongozi wa nafasi za juu pamoja na kuhamasisha ushiriki katika masuala ya usawa wa kijinsia Bungeni na nje ya Bunge.

Hili limefanikiwa zaidi kutokana na Bunge kutoa fursa za uongozi kwa wanawake kwenye nafasi mbalimbali ikiwa ni pamoja na nafasi ya Mwenyekiti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati, Makamu Wenyeviti wa Kamati na nafasi nyingine katika Sekretarieti ya Bunge.

Mheshimiwa Rais pia akiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), alishiriki katika uteuzi wa mgombea wa nafasi ya Spika ambapo Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson aliteuliwa kugombea na kuwa Spika wa pili Mwanamke kushika nafasi hiyo katika historia ya Bunge la Tanzania.

Mbali na Bunge kung'ara katika anga za kimataifa kwa wagombea wake kushinda nafasi mbalimbali lakini pia katika miaka minne ya Mheshimiwa Rais Samia Mhimili wa Bunge unajivunia kuwa mwanachama wa vyama mbalimbali vya kibunge vya kikanda na kimataifa.

Ushiriki wa Bunge kikamilifu katika vyama hivyo umeongeza uzoefu wa Wabunge wa Tanzania katika uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, kujenga ushirikiano, kudumisha utawala bora na kukuza diplomasia ya kibunge na kimataifa.

Miongoni mwa vyama vya kibunge ambavyo Bunge la Tanzania ni mwanchama ni pamoja na Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC-PF), Bunge la Afrika (PAP), Chama Cha Mabunge ya Wanachama wa Jumuiya ya Madola, (CPA), Bunge la Pamoja la Nchi za Umoja wa Ulaya, Afrika, Caribbean na Pasifiki, (ACP/EU Joint Assembly), Umoja wa Mabunge ya Nchi za Maziwa Makuu (ICGLR) na Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

Mathalani, Julai 2023, Bunge la Tanzania kwa ridhaa ya Mheshimiwa Rais lilikuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 53 wa Mwaka wa SADC-PF uliofanyika Jijini Arusha. Katika mkutano huo ambao ulifunguliwa na Mheshimiwa Rais takribani wajumbe 200 kutoka nchi 15 wanachama wa Jukwaa la SADC walishiriki.

Aidha, Oktoba 2024, Bunge la Tanzania lilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa 53 wa Chama cha Mabunge ya Nchi za



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan** akihutubia Bunge, Aprili 2021. Kulia ni Spika wa Bunge wakati wa huo, **Mhe. Job Ndugai**

**"Bunge la Tanzania limekuwa likiridhia mikataba mbalimbali yenye tija kwa taifa kama vile Mkataba wa Uwekezaji na Uendelezaji wa Bandari ulioingiwa baina ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya DP World."**

Jumuiya ya Madola (CPA), Kanda ya Afrika uliofanyika Jijini Arusha. Mkutano huo uliokutanisha washiriki 280 kutoka Mabunge ya Nchi wanachama wa CPA na ulifunguliwa na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango.

Mikutano ya aina hii ni fursa nzuri kwani inaifungua nchi yetu na kuchechemua shughuli za kiuchumi katika maeneo inapofanyika. Mfano; mikutano iliyotajwa ilichangia kuchechemua uchumi wa Jiji la Arusha kwa kuongeza kipato na kuchangia katika uchumi wa taifa kwa ujumla.

Aidha, mikutano hiyo ni fursa nzuri za kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo katika Jiji la Arusha na maeneo ya jirani kwani wageni hao walipata fursa ya kutembelea vivutio hivyo ikiwa ni pamoja na Hifadhi za Taifa za Ngorongoro na Tarangire.

Mafanikio yote hayo hayakuliondoa Bunge katika kutimiza majukumu yake ya msingi ambayo kwa mujibu wa Ibara ya 63(2), na (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, Bunge limepewa mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake, pamoja na kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa maendeleo ya muda mfupi na muda mrefu unaokusudiwa kutekelezwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Bunge limekuwa jukwaa la kujadili na kupitisha sera na mipango ya maendeleo ya Taifa, na pia limechangia kuimarisha na kuwezesha utekelezaji wa sera na mipango inayolenga kuinua ustawi na maendeleo ya wananchi wa Tanzania.

Bunge la Tanzania limekuwa likiridhia mikataba mbalimbali yenye tija kwa taifa kama vile Mkataba wa Uwekezaji na Uendelezaji wa Bandari ulioingiwa baina ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya DP World.

Bunge pia limeendelea kuisimamia na kuishauri Serikali katika uanzishaji, utekelezaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo mradi wa kuzalisha umeme wa MW 2115 wa Bwawa la Julius Nyerere, mradi wa reli ya kisasa, mradi wa daraja la J.P Magufuli (Kigongo – Busisi) lenye urefu wa kilomita 3 na Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Dodoma.

Kwa ujumla katika kipindi cha miaka minne, Bunge limeendelea kuisimamia na kuishauri Serikali, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali, kupitisha maazimio mbalimbali na kutunga sheria.

Mathalani katika kipindi hicho Bunge limefanikiwa kutunga sheria mbalimbali kuhusu masuala ya fedha, ushuru wa forodha na bidhaa, posta na simu, takwimu, usajili wa vyama vya siasa, mambo ya ndani ya nchi na nyinginezo.

Kupitia kutimiza majukumu yake ya kisheria, Bunge limefanya kazi kwa karibu na serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia ili kuhakikisha uwajibikaji na utawala bora, uwazi na uwakilishi wa wananchi katika mchakato wa kufanya maamuzi.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan** akiwa katika picha na Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson** wakati akiwa Naibu Spika wa Bunge

# Bunge laitaka TRA kukabiliana na upotevu wa mapato



Spika wa Bunge, Mheshimiwa **Dkt.Tulia Ackson** akizungumza Bungeni

Na. Lawrence Raphaely

Katika Mkutano wake wa Kumi na Saba, Bunge lilipitisha Maazimio matatu yaliopendekezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa ajili ya kukabiliana na upotevu wa mapato kufuatia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuonesha upotevu wa mapato ya kiasi cha shilingi trilioni 1.069 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Maazimio hayo yalipitishwa na Bunge kufuatia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30Juni, 2023.

Taarifa hiyo iliwasilishwa na Mjumbe wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Joseph Kakunda kwa niaba ya Mweyekiti wa Kamati wakati wa Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge kilichofanyika tarehe 29 Oktoba, 2024, Bungeni Jijini Dodoma.

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ilibainisha kuwa kiasi cha shilingi trilioni 1.069 hakikusanywa kutokana na upungufu wa aina mbalimbali.

Upungufu huo ni pamoja na changamoto za mifumo ya kodi, mizigo inayotakiwa kusafirishwa kwenda nje ya nchi na badala yake inatumika hapa nchini bila kulipiwa kodi, kutowasilishwa kwa wakati ritani za kodi kwa wakati na dosari katika ushughulikiaji wa mashauri ya kikodi.

Mapendekezo ambayo yalitolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na hatimaye kupitishwa na kuwa maazimio ya Bunge ambayo yatasaidia katika kutatua dosari hizo ni pamoja na;

Katika Azimio la kwanza Bunge iliitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikamilishe maboresho ya ujenzi na usimikaji wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kuondokana na changamoto kwenye taarifa zinazopatikana kwenye mifumo iliyokuwa inatumika hapo awali.

Pamoja na hilo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilitakiwa iendelee na kukamilisha zoezi la kusafisha taarifa za kwenye mifumo ili kuondoa changamoto ya uwepo wa taarifa zisizo sahihi za walipa kodi.

Katika Azimio la pili Bunge liliazimia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikamilishe zoezi la kutambua na kusajili idadi halisi ya walipa kodi waliopo hapa nchini ili kuwezesha kutambua kila aina ya kodi na kiasi kinachotakiwa au kinachoweza kukusanywa kutoka kwa walipakodi husika.

**Katika Azimio la tatu Bunge iliitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ianze kuandaa hesabu zake za kila mwaka kwa kutumia mfumo (Revenue statements and financial statements) ili kuondoa uwezekano mkubwa wa kuwa na makosa ambayo huathiri taswira halisi *(Fair view)* ya vitabu vya hesabu.**

Sambamba na hilo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilitakiwa ihuishe kanzi data ya walipakodi ili kupata uhalisia wa mwenendo wa ukusanyaji wa kodi na kupanua wigo wa kodi.

Katika Azimio la tatu Bunge iliitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ianze kuandaa hesabu zake za kila mwaka kwa kutumia mfumo (Revenue statements and financial statements) ili kuondoa uwezekano mkubwa wa kuwa na makosa ambayo huathiri taswira halisi (Fair view) ya vitabu vya hesabu.

Kwa upande mwingine Bunge pia lilipitisha maazimio kufuatia ukaguzi Maalum wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ambao umebaanisha changamoto kadhaa katika mchakato mzima wa ugharimiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Akiwasilisha taarifa ya Kamati, Mheshimiwa Kakunda alisema taarifa ya CAG inaonesha kwamba matokeo ya Ukaguzi Maalum umeaanisha hoja mbalimbali ikiwemo Bodi kutokidhi mahitaji ya kifedha kwa wahitaji wa mikopo kwa kiasi cha shilingi bilioni 198.9 kwa kipindi chote ambacho mawanda ya ukaguzi yalizingatia.

Changamoto zingine zilizobaanishwa ni baadhi ya wanafunzi kupewa mikopo isivyostahili ambapo baadhi walipewa kiwango kikubwa au chini ya mahitaji waliyoomba na kutokusanywa kwa mikopo ya shilingi trilioni 2.2 ambayo imekwishatolewa hadi sasa.

Kufuatia changamoto hizo Bunge lilipitisha Maazimio yaliyopendekezwa na Kamati ambapo pamoja na mambo mengine iliishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuifanya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuwa Mfuko ili kuipa uwezo wa kupata vyanzo vya ziada vya fedha ikiwemo kuweza kuwekeza kwa faida na kujenga uwezo stahimilivu kukopesha.

Azimio lingine lililoridhiwa na Bunge kuhusiana na suala hilo ni la kuitaka Serikali iendelee kutilia mkazo kuunganishwa kwa mifumo ya kieletroniki kwa Taasisi zote za Umma ili kurahisisha zoezi la kuwabaini wanufaika wote wa Mikopo ya Elimu ya Juu na kuongeza ufanisi kwenye urejeshaji wa mikopo.

Mbali na hayo kupitia taarifa hiyo ya Kamati Bunge pia liliazimia kutatua za changamoto ya kukataliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa baadhi ya madai yanayopelekwa na hospitali.

Akisoma taarifa ya Kamati Mheshimiwa Kakunda alisema kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG walibaini kuwa madai hayo hukataliwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo upungufu wa nyaraka, kughushi nyaraka na makosa ya kiuandishi.

Aliongeza kuwa athari zitokanazo na kukataliwa kwa madai hayo ni pamoja na kupunguza uwezo wa hospitali kutoa huduma kwa kukosa fedha za kununua vifaa tiba na dawa, kulipa stahiki za watumishi na kulipia huduma za msingi kama umeme na maji.

Kufuatia changamoto hizo Bunge lilipitisha Maazimio yaliyopendekezwa na Kamati ambapo pamoja na mambo mengine Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa kushirikiana na hospitali walitakiwa waboreshe utaratibu uliopo wa uaandaaji wa nyaraka sahihi na utaratibu mzuri wa malipo ili kuhakikisha kwamba madai ni sahihi, ikijumuisha uhakiki wa nambari za malipo, kutoa maelezo ya wazi ya huduma zitolewazo na kutunza rekodi sahihi za wagonjwa.



Mwenyekiti wa kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Mheshimiwa **Nagenjwa Kaboyoka**

Aidha Bunge pia liliutaka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuanzisha mfumo utakaowezesha hospitali kupata mrejesho wa madai yaliyokataliwa kwa wakati ili kuweza kufanya marekebisho kwa wakati na kuyapeleka katika muda unaoruhusiwa kisheria.



# LAAC: Halmashauri zimeshindwa kukusanya bilioni 61.15/-

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Mheshimiwa **Halima Mdee**

**Na: Zuhura Mtatifikolo**

**KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imebaini upungufu mbalimbali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwamo halmashauri 130 kushindwa kukusanya shilingi Bilioni 61.15 kutoka kwenye vyanzo muhimu vya mapato kwa zaidi ya mwaka mmoja.**

Akisoma taarifa ya Kamati kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya hesabu zilizokaguliwa hadi Juni 30, 2023 Bungeni, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Halima Mdee alisema katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kiasi hicho hakijakusanywa.

Alisema kwa upande wa Halmashauri ya Kisarawe peke yake ilishindwa kukusanya shilingi Bilioni 6.02 kutoka kampuni ya Yapi Merkez iliyokuwa inajenga Reli ya Kisasa (SGR) tangu 2021.

Kamati imeiagiza TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa kufuatilia na kubainisha mashauri yote yaliyopo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) yanayohusishwa na fedha zilizokusanywa kwa kutumia mashine za kukusanya mapato (POS) ambazo hazikuwasilishwa benki na kuhakikisha zinawasilishwa kabla Juni 30, 2025.

Aidha, Kamati ya LAAC iliitaka Serikali kuhakikisha Halmashauri zote zinahuisha kanzi data ya walipa kodi ili kupata taarifa sahihi na idadi kamili ya wafanyabiashara wanaostahili kulipa ushuru wa huduma na kuwasilisha kwa CAG kabla ya Machi 30, 2025.

"Serikali ihakikishe Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inakuwa na takwimu sahihi za mauzo ghafi ili Halmashauri ziweze kukusanya kiwango sahihi cha ushuru wa huduma," alisema.

### Mawakala Kitanzini

Mheshimiwa Mdee alisema Kamati inaagiza Serikali kuhakikisha Halmashauri 12 zinakusanya kiasi cha shilingi bilioni 5.65 kutoka kwa mawakala wa ukusanyaji mapato na kuchukua hatua stahiki wa Mawakala wasiowasilisha mapato kwa mujibu wa mikataba yao.

Pamoja na hayo, alisema Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinafanya usuluhishi wa madai yote katika Mfumo wa Mapato (LGRCIS) yenye thamani shilingi bilioni 45.02

kwa lengo la kujua wadaiwa halali wa Halmashauri na wadaiwa wasio halali ili waondolewe katika mfumo kabla ya Machi 30, 2025.

### Stakabadhi Bandia

Katika taarifa yake, Kamati ya LAAC iliitaka Serikali kuhakikisha Halmashauri zote hazifanyi malipo yasiyo na stakabadhi za kielektroniki kama ilivyoelezwa katika

> **Serikali ihakikishe Halmashauri ambazo zilitumia shilingi bilioni 1.95 zaidi ya kiasi kilichowekwa katika akaunti za amana kurejesha kiasi hicho cha fedha kabla ya Juni 30, 2025, - Mdee**

Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Utozaji wa Kodi, Sura ya 438 iliyorekebishwa mwaka 2019.

"Imebainika Halmashauri 64 zilifanya malipo yasiyo na stakabadhi za kielektroniki za shilingi bilioni 7.42 ikiwamo Halmashauri ya Singida ilipokea stakabadhi bandia zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 147," alisema.

Pia alisema Serikali ihakikishe Halmashauri ambazo zilitumia shilingi bilioni 5.16 kwa shughuli ambazo hazikukusudiwa zirejeshe fedha hizo katika akaunti ya amana kabla Juni 30, 2025.

"Serikali ihakikishe Halmashauri ambazo zilitumia shilingi bilioni 1.95 zaidi ya kiasi kilichowekwa katika akaunti za amana kurejesha kiasi hicho cha fedha kabla ya Juni 30, 2025," alisema.

### Madeni ya Halmashauri

Mheshimiwa Mdee alisema kumekuwapo na madeni makubwa ambapo watumishi wanadai shilingi bilioni 17.13 na wazabuni shilingi bilioni 29.9 katika Halmashauri 55 na kutaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha ilipe madeni yote yaliyohojiwa na CAG kwa hesabu zinazoishia Juni 30, 2023.

Alisema Halmashauri 47 ambazo zinadaiwa shilingi bilioni 21.85 za mikopo ya Programu ya Kupanga, Kupima na Kurasimisha (KKK) zirejeshwe Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Vile vile, alisema kuna haja ya Serikali kuangalia upya utaratibu unaotumiwa na Mfuko wa Hifadhi wa Jamii wa Watumishi wa Umma (PSSSF) katika kutoza adhabu za ucheleweshaji.

Alisema tararibu za kisheria zinatakiwa kufuatwa ili kushughulikia hoja ya shilingi bilioni 32.07 inayotokana na faini au adhabu ya kutowasilisha michango kwa wakati.

### Miradi Kutokamilika

Mheshimiwa Mdee alisema kumekuwapo na tatizo la miradi kutokamilika kwa wakati na kusababisha kukosekana kwa tija ya uanzishwaji wa miradi hiyo pamoja na kuwakosesha wananchi manufaa ambayo yangepatikana iwapo miradi hiyo ingetumika kama ilivyokusudiwa.

"Bunge liazimie Serikali ihakikishe inatenga bajeti ya kutosha ili miradi ambayo haijakamilika yenye thamani ya shilingi bilioni 206.89 inakamilika ili thamani ya fedha ya miradi hiyo iweze kupatikana," alisema.

"Serikali iondoe dosari zote zilizobainishwa na CAG kwa miradi ambayo imekamilika lakini haijaanza kutumika ili miradi hiyo ianze kutumika kwa maslahi mapana ya wananchi," alisema.

### DCB irejeshwe Serikalini

Alisema tathmini ya uwekezaji wa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam katika Benki ya kibiashara ya utendaji wa Benki ya Jamii ya Dar es Salaam (DCB) umekuwa ukishuka kila mwaka hadi kusababisha thamani ya hisa moja kufikia shilingi 140 kutoka shilingi 1000 wakati wa uanzishaji wa benki.

"Kuporomoka kwa thamani ya hisa na utendaji usioridhisha wa DCB umesababisha wanahisa zikiwamo Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam ambazo zimewekeza shilingi bilioni 26.89 kupata hasara inayofikia shilingi Bilioni 16.7,"alisema

Aliomba Bunge liazimie kwamba Serikali ihakikishe mabadiliko ya Sheria yanafanyika ili DCB iondoke kutoka benki binafsi na iwe katika orodha ya Mashirika yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina.



# Misingi ya Uratibu na Uendeshaji wa Bunge

**Na. Athuman Hussein**, *ndc*
a.brambati@bunge.go.tz

**Mahatma Gandhi aliyewahi kuwa Kiongozi wa India na mtetezi wa haki za kiraia aliwahi kuwa na kauli: ''Hatua moja mbele ni mwanzo wa safari ndefu''. Kwa muktadha wa kauli hiyo, mwendelezo wa makala hii ni safari ya mawazo, uelewa na uzoefu kutoka matoleo yaliyopita. Katika toleo la Nane, maelezo yalitolewa kuhusu dhana ya hoja na aina za hoja. Ufafanuzi wa dhana ya hoja ulifanyika kwa kurejea Kamusi Kuu ya Kiswahili na kisha kuyaweka maelezo kwa muktadaha wa kibunge.**

Neno ''hoja'' katika uga wa kibunge liliainishwa kwa kutaja hoja kuu na hoja za pili. Mifano ya hoja kuu ilitolewa kwa kurejea Kanuni za Kudumu za Bunge. Rejea kuu ikawa ni kanuni ya 61. Hoja za pili zilielezwa kwa kuzipanga kwenye makundi matatu: Hoja ndogo, hoja zenye hadhi maalumu na hoja za kawaida. Ufafanuzi wa kina ulitolewa kwa hoja kuu lakini hoja za pili hazikufafanuliwa zaidi.

Toleo hili linafafanua hoja za pili kutoka kwenye maelezo yaliyotolewa na Toleo la Nane. "Hoja ndogo" ni mapendekezo yanayotolewa wakati wa kujadili hoja kuu. Mapendekezo hayo yanatumika kwa mambo matatu kuhusiana na hoja kuu. Jambo la kwanza ni kurekebisha maneno kwenye hoja kuu kabla ya kujadiliwa kwake au kupigiwa kura.

> **Kanuni ya 63 ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Tanzania inafafanua utaratibu wa kujadili hoja. Kwa mujibu wa kanuni ya 63 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge hoja ndogo inayohusu marekebisho au mabadiliko ya hoja kuu itahitaji kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua kumi.**
>
> Aidha, kanuni ya 64 (1) inafafanua zaidi hoja ya marekebisho au mabadiliko

Kwa mfano, Bunge linaweza kuwa linajadili mapendekezo ya kwamba, "**Serikali itenge shilingi Bilioni 20 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.**" Miongoni mwa Wabunge, anaweza kuwepo Mbunge anayeamini kuwa uboreshaji wa miundombinu hiyo unastahili kufanyika sambamba na kuboresha miundombinu ya barabara za mijini.

Kutokana na maoni yake, Mbunge huyo anaweza kutoa hoja ya kurekebisha hoja kuu kwa kuongeza maneno '**na Shilingi Bilioni 16 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara za mijini**'. Kwa marekebisho yanayopendekezwa Bunge litafanya uamuzi kwa hoja kuu ilivyo au hoja kuu iliyorekebishwa.

Kanuni ya 63 ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Tanzania inafafanua utaratibu wa kujadili hoja. Kwa mujibu wa kanuni ya 63 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge hoja ndogo inayohusu marekebisho au mabadiliko ya hoja kuu itahitaji kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua kumi. Aidha, kanuni ya 64 (1) inafafanua zaidi hoja ya marekebisho au mabadiliko. Kanuni hiyo inaarifu kwamba mabadiliko kwenye hoja kuu yanayopendekezwa kupitia hoja ndogo yanaweza kuwa mojawapo au zaidi ya mambo matatu.

**Kwanza,** ni kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine kwenye hoja kuu. Kwa mfano katika hoja kuu kuna pendekezo kwamba, '**Serikali itenge Shilingi bilioni 80 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya vijijini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**. Mbunge mwingine anaweza kuona kwamba badala ya Sekta ya Afya, mwelekeo uwe kuboresha Sekta ya Elimu.

Mbunge mwenye maoni hayo anaweza kuwasilisha pendekezo la kuondoa baadhi ya maeneo. Kwa hapa ni neno ''afya'' na kiasi cha fedha, "shilingi bilioni 80". Hoja ndogo kwa muktadha huo inaweza kuwa kwamba, neno ''Afya'' liondolewe na badala yake neno ''elimu'' liongezwe, na kiwango cha fedha kibadilishwe **kutoka shilingi bilioni 80 hadi shilingi bilioni 92''**. Ikiwa hoja ndogo hiyo itaafikiwa Azimio litakuwa ''Kwamba Serikali itenge Shilingi Bilioni 92 kwa ajili ya huduma za Elimu Vijijini katika Mwka wa Fedha 2025/2026''.

**Pili**, kuondoa maeno fulani bila kuongeza meneo mapya ni suala la marekebisho katika hoja kuu linaloweza kuwemo katika hoja ndogo. Kwa mfano, kwenye hoja kuu mbele ya Bunge kuna pendekezo kuwa, Serikali itenge shilingi bilioni 45 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya ya uzazi, watoto wachanga na vijana katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Mbunge mwingine anaweza kuona kuwa hoja inajumuisha vipengele ambavyo havipaswi kuzingatiwa kwa pamoja. Mambo ya kuondolewa kwa maoni ya Mbunge huyo yanaweza kuwa huduma za afya ya vijana zinapaswa kujadiliwa tofauti na ilivyo kwenye hoja kuu.

Mbunge huyo, anaweza kuwa na hoja ndogo: ''kwamba maneno na vijana' yaondolewe kwenye hoja kuu''. Kwa mapendekezo hayo azimio litakuwa, ''Kwamba, Serikali itenge shilingi bilioni 45 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya ya uzazi na watoto wachanga katika Mwaka wa Fedha 2025/2026''.

**Tatu**, ni kuingiza au kuongeza maneno mapya kama inavyofafanuliwa kwenye Kanuni ya 64 (1) © ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Mfano fafanuzi ni kw hoja kwamba ''Serikali ihakikishe upatikanaji wa huduma za afya bila malipo kwa wazee wenye umri wa miaka sitini na kuendelea''. Mbunge anaweza kusimama na kupendekeza marekebisho kwa kuongeza maneno mapya ambayo ni ''na makundi maalumu kama vile watu wenye ulemavu''.



Mambo yote matatu katika hoja ya mabadiliko au marekebisho yanafanyika kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge. Miongoni mwa masharti yanayohusu hoja ya mabadiliko au marekebisho yameelezwa kwenye Kanuni ya 64 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Mabadiliko hayo sharti yawiane na hoja inayokusudiwa kufanyiwa mabadiliko au marekebisho. Sharti la pili chini ya Kanuni hiyo linahusu hoja hiyo kutoingiza kwenye hoja kuu, jambo lolote ambalo kwa maoni ya Spika, linaweza kuwasilishwa kwa hoja maalumu.

Sharti la tatu linahusu hoja hiyo ya mabadiliko au marekebisho kutokuwa na jambo linalopingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa Kanuni ya 64 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inakataza badiliko la hoja linalopingana moja kwa moja na hoja ya msingi. Anayeamua iwapo badiliko hilo linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi ni Spika.

Hoja yoyote kuhusu mambo matatu yaliyoelezwa awali, imewekewa utaratibu kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni ya 63 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka sharti kwamba, Mbunge mwenye hoja ya marekebisho au mabadiliko atatakiwa kusimama mahali pake wakati anapoitwa na Spika ili kutoa hoja yake. Baada ya kufanya hivyo, hoja yake itahitajika kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua kumi, vinginevyo itatenguka.

Utaratibu wa kuunga mkono hoja ya marekebisho umebainishwa kwenye Kanuni ya 63 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Mbunge anayeunga mkono hoja anafanya hivyo kwa kusimama tu mahali pake bila kusema lolote kuhusu hoja hiyo, kisha kukaa. Sharti hilo haliondoi haki ya Mbunge huyo kuizungumzia hoja aliyoiunga mkono baadaye.

Katika utaratibu huo, swali linaweza kujitokeza pale ambapo Wabunge wawili au zaidi watasimama kwa ajili ya hoja ya mabadiliko au marekebisho kwa wakati mmoja na kwenye hoja moja ya msingi. Msomaji anaweza kuuliza ''inatolewaje hoja hiyo na uamuzi unakuwaje?''. Kanuni ya 65 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inafafanua kwamba, ikitokea hali hiyo, spika atawaita watoa hoja wote kwa kufuata mpangilio atakaoamua.

Baada ya hoja zote za mabadiliko ya hoja kuamuliwa, Spika ataitoa tena hoja ya awali ili ijadiliwe kama itakavyokuwa imebadilishwa. Maelezo hayo yametolewa katika Kanuni ya 65 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Aina nyingine ya hoja za pili ni hoja zitokanazo na hoja nyingine (*incidental motions*) kwa kawaida hoj ahizi hutokana na muktadha wa moja kwa moja hoja nyingine au mwenendo wa kikao. Madhumuni ya hoja hizi ni kushughulikia masuala ya kiutaratibu yanayotokea wakati wa kujadili hoja nyingine. Masuala hayo yanaweza kuw ani madai ya ukiukwaji wa Kanuni, kwa maneno mengine hoja zitokanazo na mjadala ulivyo ni hoja za kiutaratibu.

Hoja za kiutaratibu zinajitokeza kutokana na shughuli zinazojadiliwa na ni lazima ziamuliwe mara moja kabla ya kuendelea. Madhumuni yake ni kushughulikia masuala ya kiutaratibu, kufafanua kanuni au kutatua hali ya sintofahamu kuhusu mwenendo wa kikao au mjadala. Hoja hizi hazihusu moja kwa moja hoja kuu, bali zinahusiana na kanuni na taratibu zinazohusika na majadala wa hoja inayoendelea.

Sifa zinazopambanua hoja hizi ni pamoja na kuhitaji uamuzi wa haraka. Jambo linalohusu utaratibu linahitaji uamuzi wa haraka. Kwa asili yake, hoja za namna hii zinapaswa kuamuliwa bila kuahirishwa.

Sifa ya pili ya hoja hizi ni kutojadiliwa. Tofauti na hoja nyingine zinahitaji kujadiliwa, hoja hizi zinaamuliwa bila mjadala. Sifa ya tatu na muhimu ni kuwa hoja hizi hazihusu masuala ya kimaudhui katika hoja inayoendelea bali utaratibu. Mfano wa hoja za aina hiyo ni ''kuhusu utartaibu *(point of order)*'' kutoa taarifa *(point of information)* na kuomba mwongozo. Mambo hayo kwa pamoja yanahitaji uamuzi wa haraka. Kutoa maelezo zaidi, katika toleo hili ufafanuzi unatolewa kuhusu hoja za masuala hayo moja baada ya nyingine.

**Kwanza**, ni hoja ya jambo la kukumbushia utaratibu *(point of order)*. Hoja ya namna hii ni nyenzo muhimu katika mjadala na madhumuni yake yanajumuisha kuhakikisha kuwa mjadala unafuata kanuni na taratibu. Vilevile, hoja hii inakusudia kubainisha au kupinga vitendo au tabia zinazokiuka kanuni za vikao.

Hoja ya utaratibu inatolewa wakati wowote linapojitokeza suala la ukiukaji wa kanuni au taratibu. Masharti yake ni pamoja na kuruhusiwa kukatisha mchango wa mzungumzaji kwa sababu inahusiana moja kwa moja na usahihi wa shughuli zinazoendelea.

Kanuni ya 75 ya Kanuni za Bunge inafafanua hoja ya utaratibu. Katika ufafanuzi huo, ruhusa inatolewa kwa Mbunge kusimama ili kukatisha mazungumzo ya Mbunge anayejadili hoja na kutamka ''kuhusu utaratibu''. Wakati huo, Mbunge aliyekuwa akijadili atanyamaza na kukaa. Kwa mujibu wa kanuni hiyo ni wajibu wa Mbunge anayeibua hoja ya utaratibu kutaja kanuni au sehemu ya kanuni inayokiukwa.

Spika anatakiwa kuamua au kufafanua kadiri ya mahitaji. Uamuzi wa Spika unaweza kutolewa papo hapo au kuahirishwa kwa madhumuni ya kulifikiria zaidi jambo hilo. Aidha, Spika anaruhusiwa kuitaka Kamati ya Kanuni au Kamati nyingine yoyote ya Bunge impe ushauri kuhusu jambo linalohusika.

**Pili**, ni hoja ya kutoa taarifa (*point of information*) ambayo ni nyenzo ya ufafanuzi na masahihisho ya upotofu wa maelezo. Madhumuni ya hoja hii ni kutoa maelezo ya ziada ili kumsaidia mzungumzaji kuelewa au kufafanua jambo linalozungumziwa. Vilevile, hoja hii inalenga kusahihisha taarifa potofu pale ambapo mzungumzaji ametoa taarifa isiyo sahihi.

Kadhalika, hoja ya kutoa taarifa inafanya kazi ya kuujenga mjadala hususan wakati majadiliano yanagusa masuala magumu au yenye undani kitaalamu. Aidha, hoja hiyo inasaidia

**Kanuni ya 76 ya Kanuni za Bunge inamruhusu Mbunge kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika.**

Mwongozo huo unaombwa kwa jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi,

kuondoa mivutano au kutokuwa na uwazi katika mjadala kwa kutoa taarifa muhimu.

Kanuni ya 77 ya Kanuni za Bunge inafafanua ruhusa kwa Mbunge kutoa taarifa au ufafanuzi. Kanuni hiyo pia inabainisha utaratibu utakaotumika na hatima ya taarifa. Kwa mujibu wa kanuni hiyo, Mbunge anaruhusiwa kusimama mahali pake na kutamka ''Taarifa'' *(Point of Information)*. Kwa ruhusa ya Spika, Mbunge huyo atatoa taarifa au ufafanuzi kwa dakika zisizozidi mbili. Wakati huo, Mbunge aliyekuwa anazungumza atatakiwa kukaa nakusikiliza maelezo. Hatima ya ufafanuzi huo ni Mbunge aliyepewa taarifa hiyo kuikubali au kuikataa baada ya kuhojiwa na Spika.

**Tatu** ni hoja kuhusu mwongozo inayotolewa wakati Mbunge anapohitaji ufafanuzi wa Spika kuhusu kuruhusiwa kwa jambo lililotokea au utaratibu wa kufuata katika jambo litakalobainishwa. Madhumuni ya hoja hii ni kuwezesha upatikanaji wa ufafanuzi unaowezesha uzingatiaji wa taratibu. Hoja hii ni hoja ya kiutaratibu kwa sababu inahusiana na utekelezaji wa kanuni au utaratibu wa kibunge. Hoja hii haihusu moja kwa moja maudhui ya suala lililomezani.

Kanuni ya 76 ya Kanuni za Bunge inamruhusu Mbunge kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba 'mwongozo wa Spika'. Mwongozo huo unaombwa kwa jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi, iwapo jambo linalohusika linaruhusiwa au haliruhusiwi. Kinachozingatiwa hapo ni kanuni na taratibu za Bunge kuhusu jambo hilo.

Mbunge atakapoomba "Mwongozo wa Spika" anaweza kujibu papo hapo au badaye kadri atakavyoona inafaa. Kanuni hiyo imelenga kuwapa nafasi Wabunge ya kuhakikisha kwamba mjadala na matukio katika Ukumbi wa Bunge kwa ujumla vinafuata taratibu zilizopo, zinazingatia heshima na kwamba hakuna jambo linalotokea isivyopaswa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge.

**Nne** ni kutengua Kanuni au kuahirisha matumizi ya kanuni fulani. Hoja hii inahusu kuweka kando kanuni fulani kwa madhumuni maalumu. Madhumuni yake ni kuwezesha majadiliano kwa kuzingatia muktadha wa jambo au hali ya kipekee iliyopo. Msingi wa hoja ya aina hiyo ni nia ya kuwa na mjadala wenye tija katika muktadha wenye upekee. Kwa nia hiyo, Bunge linaweza kuwa na ufanisi zaidi kwa kutengua kanuni kuliko kutokufanya hivyo.

Katika Kanuni za Bunge la Tanzania hoja hii imezingatiwa. Kanuni ya 174 imeeleza namna ya kutengua kanuni yoyote ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa kanuni hiyo, anayeweza kutoa hoja ya kutengua kanuni ni Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mbunge mwingine yeyote. Kanuni ya 174 (3) ya Knauni za Bunge, inaweka sharti kwamba maelezo ya hoja ya kutengua kanuni yajumuishe madhumuni ya kutengua.

Masharti zaidi yamewekwa kwenye kanuni ya 174 (4) ya Kanuni za Bunge kwamba, hoja hiyo ikiamuliwa, kanuni inyohusika itatenguliwa kwa madhumuni hayo tu na si mengine yoyote. Masharti hayo yanazingatia azma ya hoja kugusa muktadha wa kipekee. Baada ya hapo, kanuni itaendelea kwa kuwa mambo yatarejea katika muktadha wa kawaida.

Kwa jumla, hoja ndogo (*subsidiary motions*) kama ilivyoelezwa katika toleo hili ni nyenzo ya Wabunge wote kushiriki kwenye mchakato wa kufanya uamuzi. Hoja hizi hutumika kuibua, kurekebisha au kuondoa suala linaloendelea. Wakati mwingine hoja ndogo (*subsiduary motion*) zinasaidia kuimarisha mjadala na kuulinda usitoke nje ya taratibu za Bunge wala kukiuka Kanuni za Bunge. Maelezo yote hayo ni mwendelezo wa Makala kuhusu Taratibu za Uendeshaji wa Bunge.

Kwa kuhitimisha, toleo lililopita lilieleza aina kuu za hoja ambazo ni hoja kuu, hoja ndogo na hoja zenye hadhi maalumu. Ufafanuzi wake ulikuwa wa jumla na uliendelea hadi kwenye taratibu za hoja kwa mujibu wa Kanuni za Bunge la Tanzania. Katika Toleo hili maelezo yametolewa kuhusu hoja ndogo hususani hoja za kiutaratibu. Aina nne za hoja za kiutaratibu zimeelezwa. Hoja hizo ni: hoja kuhusu utaratibu, hoja kuhusu kutoa taarifa inayosaidia kwenye mjadala, hoja ya kuomba mwongozo na hoja ya kuahirisha matumizi ya kanuni fulani.

Katika toleo lijalo, Toleo la Kumi, ufafanuzi utatolewa kuhusu hoja za zenye hadhi maalumu. Tukumbuke kauli ya kifalsafa iliyotolewa na Lao Tzu (Laozi) akiandika kwa kichina kwa tafsiri kuwa ''Safari ya maili elfu huanza kwa hatua moja''. Kauli hiyo ni msemo maarufu duniani unaosisitiza hatua ndogo kama ilivyoanza makala hii na uendelevu kama itakavyoendelea katika matoleo yajayo. SHIME MSOMAJI.

# Serikali: Sehemu kubwa ya Bajeti ya 2025/26 itabebwa na mapato ya ndani



Serikali itaendelea kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 ambavyo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza ujuzi.

*- Waziri Mwigulu*

Waziri wa Fedha, Mheshimiwa **Dkt. Mwigulu Nchemba**

**Na. Lawrence Raphaely**

**Serikali imepanga kuhakikisha kuwa mapato ya ndani yanaendelea kugharamia kiasi kikubwa zaidi cha bajeti ya Serikali kisichopungua 70% ya bajeti yote katika mwaka wa fedha 2025/2026.**

Akiwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26 wakati wa Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba alisema Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania na taasisi nyingine za Serikali itaendelea kutekeleza mkakati wa muda wa kati wa ukusanyaji wa mapato wenye lengo la kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa mikopo na misaada katika bajeti.

Alisema Serikali inakadiria kuwa na mapato na matumizi kutoka kwenye vyanzo vyote ya jumla ya shilingi trilioni 55.06 katika mwaka wa fedha wa 2025/26.

"Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani ni shilingi trilioni 38.96 ikilinganishwa na maoteo ya shilingi trilioni 34.6 mwaka 2024/25," alisema.

Aidha alisema ongezeko hilo limezingatia misingi ya uchumi jumla, mikakati na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA.

Aliongeza kwamba mikakati mingine itakayoendelea kuchukuliwa na serikali ni pamoja na kudhibiti utoaji wa



**"Dira ya Taifa ya Maendeleo itahakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa na athari chanya katika kuinuia kiwango cha miasha ya watu wetu na kupunguza umaskini"**

*- Waziri Prof. Kitila Mkumbo*

misamaha ya kodi, na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji zitakazowezesha uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato.

Kwa upande mwingine Mheshimiwa Mwigulu alisema Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 umeainisha maelekezo mbalimbali ambayo Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti.

Miongoni mwa maelekezo hayo ni pamoja na kuzingatia ukamilishaji wa miradi inayoendelea kabla ya kuibua miradi mipya sambamba na kulipa madeni ya miradi inayoendelea au iliyokamilika.

Maelezo mengine ni kuhakikisha matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato kwa kufanya uhakiki, usuluhishi na ukaguzi wa mifumo mara kwa mara kwenye vituo vyote vya makusanyo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.

Mkakati mwingine ni kuendelea kufuatilia kwa karibu utendaji wa mashirika ya umma hususani yale yanayojiendesha kibiashara na kuyaandalia mkakati wa kuyawezesha kujiorodhesha katika soko la hisa ili kupunguza wajibu wa Serikali kudhamini na kugharamia uendeshaji wa mashirika hayo.

Sambamba na hayo Mheshimiwa Mwigulu alisema mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambavyo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza ujuzi.



Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa **Hussein Bashe**



> **Serikali imeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi ambapo ujenzi umefikia asilimia 91 pamoja na ujenzi wa barabara zenye jumla ya km 4,202.36 za mijini na vijijini kupitia TARURA ambapo kati ya hizo, barabara za lami km 284.40 na barabara za changarawe kilometa 3,917.96,**

Alitaja maeneo mahsusi yatakayopewa kipaumbele cha bajeti kwa mwaka 2025/26 kuwa ni uendelezaji wa miundombinu, uimarishaji wa sekta za uzalishaji na huduma za jamii, usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Vipaumbele vingine ni kuboresha usimamizi na mifumo ya kitaasisi ili kuimarisha utawala bora, kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa makundi maalum na kugharamia maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwigulu alizungumzia pia mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 alisema ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa reli ya SGR kipande cha Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma (KM 722) na kuanza kutoa huduma pamoja na kuendelea na ujenzi katika vipande vingine.

Mafanikio mengine ni kuanza uzalishaji wa umeme wa maji katika Bwawa la Julius Nyerere ambapo megawati 705 za umeme zinazalishwa kupitia mitambo mitatu (3) kati ya tisa (9) na hivyo kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme nchini.

Kuhusu utekelezaji wa mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini alisema hadi sasa vimefikiwa vijiji 12,167 na vitongoji 32,827

Kwa upande wa utekelezaji wa programu ya elimu ya awali, Elimu msingi na Sekondari bila ada alisema Serikali imefanikiwa kujenga miundombinu ikiwemo shule za msingi mpya 302

Katika eneo la utoaji wa mikopo kwa wanafunzi Mheshimiwa Mwingulu alisema wanafunzi 229,652 wa elimu ya juu pamoja na wanafunzi 2,299 wa ngazi ya stashahada wanaosoma fani za kipaumbele ikiwemo afya, sayansi na ufundi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Kujenga na kukamilisha miundombinu pamoja na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya

Ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa, Hospitali za Rufaa za Kanda na mkoa pamoja na Hospitali Maalum ya magonjwa ambukizi ya Kibong'oto;

Ukamilishaji wa miradi 705 katika vijiji 1,733 na miradi 85 ya maji mijini ambapo imewezesha wastani wa wananchi wanaopata huduma za maji kufikia asilimia 79.6 vijijini na asilimia 90 kwa mijini.



Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa **Dkt. Godwin Mollel**



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa **Prof. Adolf Mkenda**

Mbali na hayo alisema kuwa Serikali pia imefanikiwa kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miradi mipya ya skimu za umwagiliaji yenye jumla ya hekta 143,482 na mabwawa yenye jumla ya mita za ujazo 936,535,700.

"Serikali pia imeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi ambapo ujenzi umefikia asilimia 91 pamoja na ujenzi wa barabara zenye jumla ya km 4,202.36 za mijini na vijijini kupitia TARURA ambapo kati ya hizo, barabara za lami km 284.40 na barabara za changarawe kilometa 3,917.96," alisema.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo akiwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026 alisema Dira ya Taifa ya Maendeleo inayoandaliwa na mipango itakayoambatana nayo, itajikita katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira nyingi, na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi.

"Dira ya Taifa ya Maendeleo itahakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa na athari chanya katika kuinuia kiwango cha miasha ya watu wetu na kupunguza umaskini," alisema.

Aliongeza kuwa ili kufikia adhima hiyo, mkazo mahususi utawekwa katika sekta za uzalishaji ambazo zinahusisha watu wengi.

"Mkazo wa kipekee utaendelea kuwekwa katika kuchochea maendeleo kijamii na kiuchumi vijijini," alisisitiza.

Aidha alisema kuwa vigezo vitakavyozingatiwa katika kuchagua vipaumbele vya ya Mpango kwa mwaka 2025/26 ni pamoja na ukuaji endelevu wa uchumi lengo likiwa kufikia ukuaji wa uchumi wa juu wenye ustahimilivu zaidi kwa kuongeza tija, mahitaji ya jumla na kulenga uwekezaji wa kimkakati katika sekta muhimu za kilimo, viwanda na huduma.

Alisema kigezo kingine ni kupunguza umaskini ambapo inalenga kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi jumuishi unaozingatia upatikanaji wa huduma za kijamii, programu zinazolenga kinga ya jamii na zenye kutengeneza fursa za kiuchumi.

Kigezo kingine ni kuzalisha Ajira kwa Wananchi ambapo inahusisha kuainisha afua zitakazoimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi zilizopo na zinazoanzishwa ili kutengeneza nafasi za ajira hususan vijana na wanawake.

Mbali na hayo alisema kigezo kingine ni kuimarishwa kwa ushindani katika Masoko ya Kikanda na Kimataifa ambapo inajumuisha kuboresha miundombinu, kuweka mazingira wezeshi ya biashara, kufuata taratibu za kimataaifa, kuimarisha rasilimali watu, kukuza uwekezaji wa ndani na nje.

Pia alianisha kigezo kingine kuwa ni maendeleo endelevu ambapo inalenga katika kuhakikisha matumizi endelevu ya maliasili na kupunguza uharibifu wa mazingira na upotevu wa viumbe hai.

Mwisho alisema kigezo kingine ni Utawala Bora na Utawala wa Sheria ambacho kinajumuisha hatua madhubuti za kupunguza rushwa, kuwezesha upatikanaji wa haki, kuimarisha uwajibikaji, na kulinda haki za binadamu.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 ni Mpango wa mwisho katika mfululizo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) uliobeba Dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu".



# PIC Yataka Usimamizi Thabiti Taasisi na Mashirika ya Umma

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), Mheshimiwa **Vuma Hoile**

**Na. Zuhura Mtatifikolo**

**KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imebaini mambo makuu nane yaliyosababisha kukosekana kwa ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma huku ikitaka kuwekwa kwa mikakati ya kuziwajibisha Bodi na Menejimenti za Taasisi na mashirika yanayoshindwa kutekeleza kigezo cha kisheria cha kuchangia katika mfuko Mkuu wa Serikali.**

Akisoma bungeni taarifa ya Kamati ya PIC kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka 2022/23, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mheshimiwa Vuma Hoile alisema baadhi ya taasisi na mashirika ambayo serikali imewekeza mtaji wa umma hayachangii kabisa na mengine kuchangia kidogo kuliko zinavyopaswa kuchangia katika mfuko huo.

Alipendekeza serikali kupitia Msajili wa Hazina iongeze usimamizi kwa Taasisi na Mashirika ya umma kuhakikisha yanaimarisha utendaji wake kwa lengo la kuongeza mapato yake na kuongeza mchango wake katika mfuko huo.

Alisema Msajili wa Hazina afanye marejeo ya vigezo vya utendaji na kuvipanga kwa Taasisi kwa kulingana na uhalisia wa majukumu ya Taasisi au Shirika husika na kuhakikisha zinajiendesha ndani ya vigezo vya utendaji ilivyopatiwa kwa lengo la kuleta ufanisi na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana.

"Kuweka utaratibu wa kuwachukulia hatua stahiki Bodi na Menejimenti za Taasisi zinazoshindwa kutekeleza vigezo vya utendaji walivyopatiwa,"alisema.

### Utegemezi Serikalini

Mwenyekiti huyo alisema ufanyike upembuzi wa Mashirika yanayotegemea ruzuku na kuyawekea mipango ya kupunguza utegemezi hususani katika kipengele cha mishahara na matumizi mengineyo (OC).

Alitaka pia serikali kusimamia Taasisi na Mashirika ya umma yanayotegemea ruzuku kuhakikisha yanatafuta njia mbadala za kupata rasilimali ikiwamo kutumia mikopo nafuu na kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji ya kibiashara ili kuipunguzia serikali mzigo wa kugharamia miradi hiyo.

Alibainisha kuwa kamati imebaini kusuasua kwa mashirika ni kutokana na upungufu wa mtaji wa uendeshaji, kupata hasara/nakisi kwa miaka mitatu mfululizo, kushindwa kutumia kikamilifu fursa za uwekezaji zilizopo, mchakato wa sheria ya manunuzi, kupata vibali vya ajira na kupata vibali vya mikopo.

"Serikali kupitia Msajili wa Hazina kufanya mapitio ya Taaasisi na Mashirika ya umma kwa lengo la kubainisha changamoto wanazokabiliana nazo na kuwa na mpango mahususi wa kutatua changamoto hizo ili kuongeza ufanisi wake na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana,"alisema.

### Mtaji TIB

Mheshimiwa Vuma alitaka pia Serikali iongeze mtaji kwa benki ya maendeleo (TIB) ili kukidhi matakwa ya sheria ya Benki Kuu (BoT) na kumudu ushindani kwenye soko kwani ni muhimu benki hiyo ikaendelea kuwapo ili itekeleze malengo ya uanzishwaji wake.

### Malipo ya Wakandarasi

Alisema ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi umewaathiri pia baadhi yao hasa wazawa ambao mitaji yao ni midogo hivyo kudumaa kiutendaji na kukosa sifa za kupata miradi mingine.

Aliomba Bunge liazimie serikali kupitia Msajili wa Hazina kusimamia kikamilifu taasisi na mashirika ya umma kuhakikisha wanakamilisha maandalizi yote ya awali kabla ya kuingia mikataba ya utekelezaji wa miradi husika kwa lengo la kuepusha kuiongezea serikali mzigo utokanao na ulipaji wa riba za ucheleweshaji.

### Mikataba Mikubwa

Alisema kamati imebainika kuna baadhi ya miradi ya uwekezaji imetolewa kwa wakandarasi ambao hawana sifa jambo linaloathiri uwekezaji wa utekelezaji wa mradi na kupelekea tija ya uwekezaji kuchelewa. Mfano mradi wa ujenzi wa kituo cha pamoja cha Manyoni na Nyakanazi.

Alipendekeza mikataba yote ya utekelezaji wa miradi hasa miradi mikubwa iwe inapitishwa na Msajili wa Hazina kabla ya kusainiwa kwa lengo la kujiridhisha juu ya kukamilika kwa maandalizi yote ya utekelezaji wa mradi lakini upekuzi wa wakandarasi umefanyika.

### Gharama za Umeme

Alisema gharama za uunganishaji umeme inayotozwa kwa maeneo ya vijiji – miji imesababisha kasi ya wananchi wa maeneo hayo kuunganisha umeme kuwa ndogo ukilinganisha na kasi ya usambazaji wa miundombinu ya umeme.

"Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Mamlaka zake zinazohusika ihakikishe inaharakisha kukamilisha tathmini za gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya namna hiyo na kubainisha majina ya maeneo na gharama ndani ya miezi sita ili kuongeza ufanisi wa mtaji uliowekezwa katika miradi hii,"alisema.

### NCAA na TANAPA

Alisema serikali irejeshe utaratibu wa zamani wa taasisi ya Ngorongoro na TANAPA kukusanya mapato yake kwa lengo la kuwawezesha kuwa na ukwasi muda wote ili kufanya maendeleo ya maeneo wanayosimamia kwa wakati.

### Stendi ya Msamvu

Mheshimiwa Vuma alieleza Bunge kuwa Mfuko wa PSSSF uliwekeza Sh.bilioni 14.76 katika mradi wa ujenzi wa Stendi ya Msamvu fedha ambazo ni sehemu ya michango ya wanachama wake na mwaka 2018 serikali ilifanya maamuzi ya kuhamishia uendeshaji wake Halmashauri ya Manisapaa ya Morogoro kwa ahadi kwamba serikali itairejeshea PSSSF fedha ilizowekeza katika mradi huu lakini ahadi haijatekelezwa kwa takribani miaka sita sasa.

"Bunge linaazimia kwamba, Serikali irudishe uendeshaji wa stendi ya Msamvu kwa Mfuko wa PSSSF ili mradi husika utumike kurejesha gharama za uwekezaji na baada ya Mfuko kurudisha gharama za uwekezaji stendi itarejea kuwa mali ya Manispaa ya Morogoro. Jambo hili pia litaipunguzia Serikali mzigo wa kulipa gharama za uwekezaji zilizotolewa na Mfuko wa PSSSF,"alisema.

> **"Bunge linaazimia kwamba, Serikali irudishe uendeshaji wa stendi ya Msamvu kwa Mfuko wa PSSSF ili mradi husika utumike kurejesha gharama za uwekezaji na baada ya Mfuko kurudisha gharama za uwekezaji stendi itarejea kuwa mali ya Manispaa ya Morogoro"**

### Michango ya Wabunge

Wakichangia taarifa hiyo ya kamati inayotokana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23, Waheshimiwa Wabunge waonyesha wamekerwa na baadhi ya mashirika na taasisi za umma kujiendesha kwa ufanisi duni, kuendelea kutegemea ruzuku hali inayoisababishia serikali hasara.

Katika Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2022/23, ilibainisha

kuwa utegemezi wa mashirika ya umma umeongezeka kutoka Sh. bilioni 13.2 hadi 17.4.

Kutokana na hilo, Waheshimiwa Wabunge wameishauri serikali kuangalia namna ya kuyafunga, kuyafilisi au kuzitafutia ubia na sekta binafsi(PPP) taasisi na mashirika hayo.

Akichangia hoja hiyo, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha alipendekeza mambo sita yanayolenga kuondokana na matumizi mabaya ya fedha za umma ikiwamo kutaja vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa kwenye teuzi za wajumbe na watendaji wakuu wa mashirika na taasisi za umma.

Alisema kuna matumizi yasiyo sahihi ya fedha za umma na kwamba matatizo wanayojadili yamekuwa yakijirudia kila mwaka na hayatokani na kukosekana kwa weledi wa masuala ya kihasibu bali ni udhaifu kwenye usimamizi na kutofuata maadili ya kazi.

"Namna ya kufanya teuzi za wajumbe wa bodi za wakurugenzi wa mashirika na taasisi za umma zizingatie taaluma, ujuzi, weledi, uzoefu na tabia, na watendaji wakuu wa mashirika ya umma wateuliwe kwa kuzingatia tabia zao, umahiri wao, uzoefu, elimu na mitizamo yao,"alisema.

Alitaka serikali ipeleke watendaji wakuu wa mashirika na taasisi kwenye mafunzo ya kikazi nje ya nchi hasa kwenye mashirika makubwa ya kihasibu ili wajifunze namna ya kuendesha mashirika hayo.

"Hivi sasa tuna Taasisi ya Uongozi serikalini ipo chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji lakini bahati mbaya haina majengo ya kudumu, wahadhiri wa kudumu napendekeza taasisi hii ihamishiwe Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili watoe mafunzo ya maendeleo ya uongozi,"alisema.

Aliomba serikali imarishe mifumo yake kwenye kutathmini utendaji wa mashirika na iongeze kasi ya kutekeleza agizo la kuimarisha matumizi ya mifumo ya serikali isomane ili kudhibiti udanganyifu.

Kwa upande wake Mbunge wa Njombe Mjini Mhe. Deodatus Mwanyika alisema katika mashirika 35 ya kibiashara bado mashirika 17 yanapokea ruzuku ya serikali.

"Haya ndiyo mambo yaliyosababisha mageuzi na kwanini baadhi ya mashirika kubinafsishwa, kufanya biashara kuna taratibu zake na moja kubwa ni kurudisha mtaji na kufanya kazi kwa tija...

Jambo hili tusilivumilie kwa muda mrefu, haiwezekani mpaka leo hii mashirika ya umma ya kibiashara mishahara yao bado inatoka Hazina hili halikubaliki, sio matumizi mazuri ya fedha za umma,"alisema

Alieleza kuwa serikali imeweka vigezo kwamba shirika au taasisi itoe kuanzia asilimia 15 ya mapato ghafi kama mchango, lakini bado kuna baadhi ya mashirika yanashindwa.

"Hata yale yaliyotoa mwenendo unaonesha kumekuwa na kuteremka kwa gawio kwa mapato mashirika ambayo yamekua yanatoa gawio,"alisema.

**Ukisoma ripoti hii mashirika kwa sasa yapo zaidi ya 248 lakini najiuliza ni lini tumeunda mashirika yote hayo mengi?, muelekeo kwasasa bado haujabadilika sana kwani bado kuna mashirika mengi yanaingiza hasara na hayajatambua uwekezaji wa serikali na inatakiwa ipate faida kwa ajili ya watanzania**

*Mheshimiwa Deodatus Mwanyika*

Aliongeza "Ukisoma ripoti hii mashirika kwa sasa yapo zaidi ya 248 lakini najiuliza ni lini tumeunda mashirika yote hayo mengi?, muelekeo kwasasa bado haujabadilika sana kwani bado kuna mashirika mengi yanaingiza hasara na hayajatambua uwekezaji wa serikali na inatakiwa ipate faida kwa ajili ya watanzania."

Alibainisha kuwa kuna mashirika ambayo yanatoa huduma yanavumiliwa lakini yapo yanayofanya biashara yanatakiwa yashindane, yarudishe mtaji na kutoa gawio.

"Jambo jingine ambalo limejitokeza, kuna kampuni za biashara zinaingiza hasara mpaka zaidi ya miaka mitatu mfululizo kwa utaratibu wa kibiashara kampuni ikiingiza hasara kwa miaka mitatu mfululizo hizo ni kampuni zinazofilisika zisiendelee kuharibu rasilimali za nchi,"alisema.

Alitolea mfano kuna mashirika yana majengo kama mali isiyohamishika lakini sio suluhisho la kufanya kampuni iwe na mtaji na kwamba basi serikali iangalie utaratibu mwingine wa kufunga, kufilisi au zitafutiwe wabia.

Naye Mbunge wa Mwanga Mhe. Joseph Tadayo alisema mashirika ya umma lazima yajiendeshe kama ya binafsi ili yafanye vizuri.

"Kwa bahati mbaya Bodi zetu nyingi ni zile ambazo hazina umahiri na sekta wanazozisimamia hawawezi kutupa matokeo tunayoyataka, kumekuwa na malalamiko ya hapa na pale kwamba Serikali inawaingilia lakini Bodi ambayo inauwezo haiwezi kukubali kuingiliwa na Serikali ni bora wajiuzulu" alisema

Alisema Bodi lazima zitambue kazi yake ni kuongoza ili kuleta faida na zisimamie mashirika yafanye miradi inayoleta faida.

# Umuhimu wa Kamati za Bunge katika Utekelezaji wa Madaraka ya Bunge



Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria katika kikao kazi na Watendaji wa Taasisi mbali mbali za Serikali

**Na. Athuman Hussein**, *ndc*

**"Kalamu ni ulimi wa akili" ni usemi wa Miguel de Cervantes ambaye ni mwandishi maarufu wa kihispania. Usemi wa mwandishi huyu aliyeishi mwaka 1547-1616, umechukuliwa kutokana na mchango wake katika fasihi. Ni usemi unaosisitiza maandishi yaliyoandikwa kuwa kielelezo cha mwanzo cha fikra na mawazo ya msingi kuhusu umuhimu wa Kamati za Bunge katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge.**

Msisitizo huo unaalika mwendelezo wa uandishi wa makala iitwayo "Umuhimu wa Kamati za Bunge katika Utekelezaji wa Madaraka ya Bunge". Ikumbukwe kuwa Toleo la Saba lilifafanua vipambanuzi vitano vya Kamati za Bunge vilivyoelezewa katika Toleo la Saba. Ufafanuzi uliofanywa katika Toleo la Nane ulihusu muktadha halisi wa Bunge la Tanzania kwa kupitia Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Masuala matano yaliyojadiliwa yalihusu Kamati kutofautiana na Bunge kimuundo, ambapo kanuni ya 135 ilirejewa na Kamati kuwa kitovu cha Bunge ambapo, kanuni ya 60 ilidadavuliwa kwa muono huo.

Vilevile, suala la Kamati kuhitimisha kazi kwenye kikao cha Bunge lilitolewa maelezo kwa kurejea kanuni ya 60 na kanuni ya 136 (15) za Kanuni za Bunge. Pamoja na masuala hayo, toleo lililopita lilieleza suala la Kamati kutokuwa na uamuzi kuhusu haoja inayoingia Bungeni na suala la uhuru wa Kamati katika utaratibu wake. Masuala hayo mawili yalifafanuliwa kwa kupitia kanuni ya 60(5) na kanuni ya 136(8) mtawalia.

Katika muendelezo wa maelezo yaliotolewa kwenye toleo lililopita, makala hii inaendelea kuleta mawazo na ufafanuzi kuhusu Kamati za Bunge. Ufafanuzi zaidi na wa kina unagusa uhusiano kati ya Bunge na Kamati. Eneo mahsusi katika uhusiano huo ni dhana ya uwakala na uwakilishi. Msukumo upo kwenye busara kwamba, "hakuna mwenye shida ya kuni atakayeangukiwa na jiti kavu asijitwalie." Hivyo, mwenye kiu kimawazo kuhusu uhusiano uliopo kati ya Bunge na Kamati zake, ulingo huu si wa kuacha.

Uhusiano wa kiuwakala kati ya Bunge na Kamati zake umejenga utaratibu wa Kamati kupata mamlaka yake kwa kukasimiwa na Bunge. Kwa mujibu wa Ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge ndiyo mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia shughuli za umma nchini.

Kwa mamlaka yake, Bunge limepewa madaraka ya kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi kama ilivyoelekezwa na Ibara ya 63(2) ya Katiba. Madaraka hayo yameruhusiwa yatekelezwe kwa namna Bunge litakavyoona inafaa. Ibara ya 96 ya Katiba imeliruhusu Bunge kuunda Kamati za namna mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake.

Kwa kuwa Bunge ndilo mamlaka yenye madaraka ya utungaji wa sharia na usimamizi wa shughuli za umma unaotekelezwa na Kamati za Bunge, linakuwa na ukuu. Kwa kuunda Kamati zake, Bunge linatengeneza wakala wa utekelezaji wa madaraka yake. Kamati hupewa jukumu na Bunge ili kufuatilia shughuli za umma. Kwa sababu hiyo, Kamati za Bunge zinawajibika kwa Bunge. Uhusiano huu unadhihirishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023.

Kanuni zinaonesha mambo makuu ya uhusiano wa ukuu na uwakala kati ya Bunge na Kamati za Bunge. Mambo hayo yanajumuisha mchakato wa Bunge kutunga sharia, utekelezaji wa jukumu la Bunge kusimamia shughuli za umma, namna Bunge linavyopitisha bajeti, Bunge linavyosukuma uwajibikaji wa Serikali na Bunge linavyosimamia utekelezaji wa madaraka yake yanayokasimiwa kwa mamlaka Serikalini.

Mchakato wa utungaji wa Sheria katika Bunge umefafanuliwa kwenye sehemu ya kumi na mbili ya Kanuni za Bunge. Kanuni ya 93 hadi kanuni ya 106 zimeeleza mchakato wa masharti na majukumu yanayoelekezwa kwa namna ya uhusiano wa ki-ukuu na uwakala (Principal-agent relation) kati ya Bunge na Kamati za Bunge.

Mchakato wa utungaji wa sharia Bungeni unaelezeka kuanzia muswada wa sheria Kusomwa Mara ya Kwanza. Hatua hiyo hufuatiwa na uamuzi wa Spika kuupeleka muswada wa sheria uliosomwa Mara ya Kwanza kwenye Kamati inayohusika. Ufafanuzi wa mchakato huu umebainishwa na kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Bunge. Kwa mfano, miswada ya sheria mitano iliyosomwa Mara ya Kwanza katika kikao cha tisa cha Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, tarehe 08 Novemba, 2024 ilipekekwa kwenye Kamati zinazohusika.

Kwa hatua hizo, kwa kila muswada kati ya miswada hiyo minne ilizingatia dhima ya uwakala wa Kamati za Bunge katika utungaji wa Sheria. Kwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024, wakala katika mchakato wa kutunga sheria ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria.

Mantiki ya muswada huu kupelekwa kwenye Kamati iliyotajwa inatokana na muswada huo kusainiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ofisi ambayo kisekta na kisera ni sehemu ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kifungu cha 6(2) cha Nyongeza na Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeipa Kamati hii jukumu la kuisimamia Wizara ya Katiba na Sheria. Vilevile, kifungu cha 7(1)(b) kinaitaka Kamati hiyo kushughulikia miswada ya sheria inayotoka Wizara ya Katiba na Sheria.

Dhanio (*assumption*) katika hilo ni kuwa Kamati hii itaufanyia kazi muswada unaohusika kama inavyostahili kuliko ambavyo ingeweza kufanya Kamati nyingine. Muhimu zaidi ni kuwa Kamati hiyo itabaki kuwa wakala katika mchakato. Mwenye mamlaka kuu ni Bunge lenyewe na ndiyo maana Kamati inaripoti kuhusu uchambuzi wake kwa Spika na Bungeni.

Ufafanuzi kwa miswada mingine mitatyu ni wa msingi huo. Miswada hiyo ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mazingira wa Mwaka 2024 ulifanyiwa kazi na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ikiwa ni wakala wa Bunge. Kadhalika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kazi wa Mwaka 2024 umechambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa dhima ya uwakala.

Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu Kamati za Bunge kuwa na dhima ya uwakala, kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Bunge inaeleza uwezo wa Kamati iliyopelekewa muswada kufanya marekebisho. Uwezo huo ni uwezo wa wakala sio wa mkuu. Kwa mujibu wa kanuni hiyo, uwezo wa Kamati kufanya marekebisho kwenye muswada ni wa kiushauri kwa mdhamini wa muswada.

Mwenye jukumu la msingi la kuupitisha au kutokuupitisha muswada wa sheria ni Bunge na si Kamati ya Bunge. Hivyo Kamati imepewa uwezo wa wakala ambao una nguvu tofauti na uwezo wa Mkuu (Bunge).

Pamoja na uwezo wa Kamati kuwa wa kiushauri, bado kanuni ya 97(4) ya Kanuni za Bunge imeweka sharti linalosisitiza nafasi ya wakala wa Bunge. Yaani Kamati ya Bunge iliyopelekewa muswada wa sharia kwa mujibu wa kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Bunge. Sharti hilo linahusu pia muswada uliorekebishwa kupelekwa kwenye Kamati kabla ya hatua ya kusomwa mara ya pili.

Swali muhimu hapa linaweza kuwa "**kwa nini tena muswada uliorekebishwa upelekwe kwenye Kamati iliyoufanyia kazi ilhali imekamilisha jukumu lake ni la kiushauri**?" Jibu lake linatosheleza kwa kuangalia mambo makubwa mawili: Kanuni yenyewe inavyoelekeza na dhana ya Kusomwa Mara ya Pili katika taratibu za utungaji wa sheria ya Bunge (Statute).

Jambo la kwanza, kanuni ya 97(4) ya Kanuni za Bunge imebainisha madhumuni. Kwa mujibu wa kanuni hiyo, madhumuni yake ni kuiwezesha Kamati izingatie marekebisho yaliyofanyika. Kusudio la sharti hilo ni kuiwezesha Kamati kuwa na maoni na ushauri wake unaotambua na kuzingatia marekebisho yaliyofanywa.

Jambo la pili ni dhana ya Kusomwa Mara ya Pili. Awali ieleweke kuwa kinachoelezwa hapo si "**kusomwa kwa mara ya pili**" bali "**Kusomwa Mara ya Pili**". Ufafanuzi unaotolewa ni kwamba, "**Kusomwa kwa mara ya pili**"ni lugha ya kawaida inayotumika kubainisha kipimo cha idadi ya ujirudiaji wa usomaji (Yaani, kujirudia kusomwa). "**Kusomwa Mara ya Pili**" ni lugha rasmi ya kibunge ya kueleza hatua rasmi katika mchakato wa Bunge kutunga sheria.

Sasa, dhana ya **Kusomwa Mara ya Pili** inajenga mantiki ya muswada uliofanyiwa marekebisho kupelekwa kwenye kamati kabla ya kusomwa mara ya pili. Wapo wanaoweza kuuliza swali. "Kwa vipi?" Kadhalika, swali hili ni muhimu hata kama ni **swali wakati wa kujibu swali**. Majibu yake ndiyo ufafanuzi wa dhana ya "**Kusomwa Mara ya Pili** lakini kwa kuzingatia dhana ya Kamati ya Bunge kuwa wakala wa Bunge ambayo ni kiini katika Makala hii.

Kusomwa Mara ya Pili ni hatua muhimu katika taratibu za Bunge kutunga Sheria. Kwenye hatua hii, misngi ya jumla

ya utungaji sheria na maudhui ya muswada ambao ni sheria inayopendekezwa vinajadiliwa na Bunge ili kufanya uamuzi wake. Wabunge wanaounga mkono au wanaopinga Muswada huo, wataonesha misimamo hiyo kwenye mjadala.

Mjadala wa Bunge huzingatia malengo makuu (broad objectives) na nia za kisera (policy intensions). Lengo ni kuona iwapo sheria inayopendekezwa (Muswada) ni ya lazima (necessary), inafaa (desirable) na inalingana na maslahi ya umma (aligned with public interest). Matokeo ya mjdadala yanaweza kuwa kukataliwa kwa muswada ama kupitishwa. Kwa ujumla hatua hii (Kusomwa Mara ya Pili) ni njia ya kufikia (gateway) uamuzi baada ya mjadala na kuhakikisha kuwa muswada usioungwa mkono hauendelei bila sababu.

Ufafanuzi huo mfupi wa dhana ya Muswada Kusomwa Mara ya Pili, unatetea muswada uliorekebishwa kupelekwa kwenye Kamati iliyoujadili kabla ya kusomwa Mara ya Pili. Utetezi huo unajengwa kwenye msingi kuwa, lengo la Bunge kuupeleka muswada kwenye Kamati kwa kanuni zake ni kutoa fursa kwa wadau, wataalamu na wahusika wengine kufafanua kwa kina maoni yao kwa Kamati inayoufanyia kazi Muswada huo.

Taratibu rasmi za kibunge kuzuia wasio Wabunge pamoja na changamoto ya muda wa kulitosha Bunge kuzama ndani ya madhumuni na maudhui, zinaweza kulinyima fursa ya kuingia ndani katika uchambuzi. Kukabiliana na hali hiyo, Bunge linaitumia Kamati ambayo ni wakala wake ili kupata undani kupitia tena muswada huo unaorejeshwa kwake.

Iwapo marekebisho yatafanyika na kupelekwa Bungeni, lengo la Bunge ambalo ni Mkuu kutumia Kamati ambayo ni wakala, litakwama kufikiwa. Hivyo, kwa kutambua umuhimu wa wakala, desturi za Bunge la Tanzania zimetambua nafasi ya Kamati. Utambuzi huo unaakisi dhana ya uwakala wa Kamati za Bunge kwa Bunge.

Kwa muendelezo wa Kanuni za Bunge katika muktadha wa uhusiano kati ya Bunge na Kamati zake, mapitio ya kanuni ya 98 na kanuni ya 99 ya Kanuni za Bunge yanaongezea ufafanuzi. Kanuni ya 98 inaonesha nafasi ya kazi za Kamati katka uamuzi wa muswada kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli. Kanuni ya 99 inaonesha mjadala wa Bunge kuhusu muswada wa Sheria uliofanyiwa kazi na Kamati unavyotegemea msaada wa wakala wa Bunge (Kamati).

Kwa ufafanuzi wa Kanuni ya 98 ya Kanuni za Bunge, kabla ya kuupanga Muswada kwenye ajenda ya kikao cha Bunge, Mwenyekiti anategemewa kutarifu juu ya kukamilika kwa kazi ya uchambuzi wa muswada. Baada ya kufanya hivyo, muswada unaohusika unaweza kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli za kikao cha Bunge (Order Paper). Sharti hilo linatambua nafasi ya Kamati ambayo ni wakala. Bunge ambalo ni mkuu linasubiri kupata matokeo ya kazi za wakala (Kamati) kabla ya kuanza kufanyia kazi muswada wa sheria.

Kwa upande wa ushughulikiaji wa bajeti ya Serikali, pia Kanuni za Bunge zinaonesha uhusiano wa kiuwakala kati ya Bunge na Serikali. Utaratibu wa Bunge kushughulikia bajeti unahusisha hatua mbalimbali zikiwemo tano. Hatua hizo ni Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango, Serikali kuwasilisha mapendekezo ya mpango na ukomo wa bajeti, ukaguzi wa utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka uliokwisha, uchambuzi wa Bajeti na mjadala wa bajeti Bungeni.

Katika kila hatua, uwakala wa Kamati ya Bunge kwa Bunge unajitokeza katika Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa kanuni ya 113 (2) ya Kanuni za Bunge, Mkutano wa Bunge wa Mwezi Oktoba-Novemba, kila mwaka isipokuwa Mkutano wa kwanza, Bunge linakaa kama Kamati ya Mipango. Wakati huo, Bunge linajadili mambo makuu matatu: mwongozo wa kuandaa mpango na bajeti, vyanzo vya mapato ya Seikali na vipaumbele vya mpango wa Serikali. Ili kutekeleza hayo kwa ufanisi, Bunge linaitumia Kamati ya Bajeti ambayo ni wakala wa Bunge katika uchambuzi. Kanuni ya 113(4) ya Kanuni za Bunge, imetambua uwakala huo na kuweka masharti yanayoshadidia uhusiano wa kiuwakala kati ya Bunge na Kamati ya Bajeti.

Kwa masharti hayo, kabla ya Bunge ambalo ni Mkuu kujadili, kazi ya uchambuzi wa kina inafanywa na Kamati ya Bajeti ambayo ni wakala wa Bunge. Kamati hii inatakiwa kuhitimisha uchambuzi kwa kutoa maoni kwa mkuu wake ambaye ni Bunge. Jambo hilo limeelezwa kwenye kanuni ya 113(5) (a) ya Kanuni za Bunge. Bunge linajadili mapendekezo ya Serikali kwa pamoja na maoni ya wakala wake ambaye ni Kamati ya Bajeti. Mjadala huo unapaswa kuendelea kwa siku zisizopungua tano.

Hatua ya pili inayoeleza uhusiano wa ki-uwakala katika mchakato wa bajeti ni Serikali kuwasilisha mapendekezo ya mpango wa Serikali na ukomo wa bajeti kwa Wabunge. Kwa mujibu wa kanuni ya 116, tarehe kumi na moja au tarehe ya siku nyingine ya kazi inayofuata, iwapo tarehe hiyo itakuwa si siku ya kazi, Serikali itawasilisha kwa Wabunge mambo mawili. Moja ni mapendekezo ya kiwango cha ukomo wa bajeti ya Serikali na mbili ni mapendekezo ya mpango wa Serikali kwa mwaka wa fedha uanofuata.

Katika hatua hiyo, mapendekezo hayo hupelekwa kwenye Kamati ya Bajeti kwa uchambuzi zaidi. Mchakato huu unaitambua Kamati ya Bajeti kuwa wakala wa Bunge. Uwakala huo ni kwa uchambuzi uliopaswa kufanywa na Bunge, badala yake unafanywa na Kamati hiyo. Bunge linatumia matokeo ya uchambuzi wa unaofanywa na wakala wake, Kamati ya Bajeti katika kushughulikia bajeti.

Hatua ya tatu, inayohusu uwakala wa Kamati ni ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Bunge huidhinisha bajeti ya kugharimia miradi ya maendeleo na baadaye kufuatilia utekelezaji wake. Kazi ya kufuatilia hufanywa na Kamati za Bunge za Kisekta ambazo ni wakala wa Bunge.

Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge inazitaka Kamati za Kisekta kutumia siku zisizozidi saba kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kazi hii ingelifanywa na Bunge lenyewe, lakini kwa ufanisi zaidi, kazi hiyo inafanywa na wakala wa Bunge. Yaani Kamati za Kisekta kila moja kwa sekta inazozisimamia.

Hatua ya nne ni uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka unaokwisha na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka unaofuata. Bunge ndilo lenye jukumu kuu la kufanya hivyo, lakini ili lipate undani kutokana na uchambuzi, Bunge linategemea wakala wake, Kamati za Kisekta.

Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge inaweka sharti kwamba Kamati za Kisekta zitatumia siku zisizozidi tisa kufanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi. Uchambuzi huo unaonesha uhusioano wa ki-uwakala ambapo, Bunge ambalo linapaswa kuchambua taarifa hizo na bajeti linamwachia wakala wake ambaye ni Kamati za Kisekta.

Matokeo ya uchambuzi unaofanywa na Kamati za Kisekta ni kubainishwa kwa masuala muhimu ya kibajeti ambayo hupelekwa kwenye Kamati ya Bajeti kupitia kwa Spika. Mchakato huo unazihusu Kamati za Kisekta, Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uongozi kwa mujibu wa kanuni ya 117(3) na (4). Masuala hayo hufanyiwa kazi katika ngazi ya wakala wa Bunge. Matokeo yake huripotiwa Bungeni kupitia taarifa za Kamati za Kisekta na Kamati za Bajeti. Bunge ambalo ndilo mkuu huamua baada ya kupokea taarifa za wakala, Kamati za kisekta na baadaye Kamati ya Bajeti.

Hatua ya tano ni mjadala wa Bunge kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka unaokwisha na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka unaofuata. Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Bunge inaonesha kuwa katika Mkutano wa Bunge utakaoanza mwezi Aprili kila mwaka, siku zisizozidi hamsini na nane zitatengwa kwa ajili ya kujadili bajeti. Kanuni ya 118(4) inaweka sharti kuwa Kamati za Bunge za Kisekta zitatangulia kuchambua. Kwa utaratibu huu Kamati zitafanya kazi ya uwakala wa Bunge wakati wa uchambuzi.

Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Bunge inataka taarifa ya Kamati kutokana na uchambuzi itangulie mjadala wa jumla. Msingi wake ni nafasi ya Kamati ambayo ni wakala katika uchambuzi wa bajeti. Mjadala wa jumla unafuatia taarifa ya Kamati ambayo kwa muktadha huu ni wakala wa Bunge.

Eneo lingine la uhusiano wa ki-uwakala kati ya Kamati za Bunge na Bunge, linahusu usimamizi wa kibunge. Katika eneo hili uwakala wa Kamati unaelezeka kwenye mambo matatu ya usimamzi wa Kibunge.

Jambo la kwanza ni usimamizi wa kisekta. Kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Bunge lina madaraka ya kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi. Kwa kawaida Serikali inaendesha shughuli za umma kupitia sekta mbalimbali.  Hakika hiyo imelisukuma Bunge kuwa na Kamati kulingana na sekta mbalimbali.

Kifungu cha 7(1) (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinazitaka Kamati za Kisekta kufuatilia utekelezaji unaofanywa na wizara mbalimbali. Kila Kamati ya Kisekta inasimamia sekta maalumu. Jukumu la Kamati kusimamia sekta linatekelezwa kwa namna ya wakala na mkuu. Katika utekelezaji, Kamati inafuatilia inachotakiwa na Bunge ambalo ni Mkuu, na kubaki kuwa wakala kwa kutegemea uamuzi wa mwisho kufanywa na Bunge lenyewe.

“Jambo la kwanza ni usimamizi wa kisekta. Kwa mujibu wa **Ibara ya 63(2)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Bunge lina madaraka ya kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi. Kwa kawaida Serikali inaendesha shughuli za umma kupitia sekta mbalimbali.  Hakika hiyo imelisukuma Bunge kuwa na Kamati kulingana na sekta mbalimbali.”

Jambo la pili ni usimamizi wa mitaji ya Umma. Bunge kwa nafasi yake ya kikatiba katika uendeshaji wa nchi, lina madaraka ya kusimamia tija na ufanisi wa mitaji ya umma. Kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, jukumu la kufuatilia hali ya uwekezaji wa mitaji ya umma linatekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Kwa namna ilivyo, Kamati hiyo, ni wakala wa Bunge katika kusimamia mitaji ya umma.

Jambo la tatu ni usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Bunge hupitisha bajeti na mipango ya Serikali. Kwa madaraka yake, Bunge ndilo lenye jukumu la kufuatilia matumizi ya fedha yaliyoidhinishwa na Bunge lenyewe. Kwa ajili ya kutekeleza vizuri madaraka yake, Bunge linaitumia Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikalo za Mitaa. Kila moja kati ya Kamati hizo ni wakala wa Bunge kwa nafasi zake.

Jambo la nne ni uchanguzi maalumu wa kibunge. Uchunguzi huo hufanyika linapotokea suala ambalo linahitaji upekuzi kwa namna inayoweza kulisaidia Bunge kutekeleza madaraka yake ya kuisimamia na kushauri Serikali. Zipo namna kuu mbili kwa jambo hilo. Namna ya kwanza ni uchunguzi wa Kamati Maalumu ya Bunge inayoweza kuundwa kwa mujibu wa kanuni ya 139(1) ya Kanuni za Bunge. Jambo la pili ni uchunguzi wa Kamati Teule inayoweza kuundwa kwa mujibu wa kanuni ya 139 ya Kanuni za Bunge.

Katika namna zote hizo, Bunge huwa na jukumu maalumu linaloendana na madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Madaraka hayo hutekelezwa kuanzia kwenye Kamati ambazo baadaye huripoti Bungeni kwa uamuzi. Katika mpangilio huo wa kiutekelezaji Kamati ni wakala na Bunge ni Mkuu kimadaraka.

Uwakala na Ukuu wa Kamati na Bunge mtawalia, unabainika katika taratibu za uchunguzi. Chimbuko na mantiki ya majukumu ya Kamati Maalumu au Kamati Teule ni madaraka ya Bunge. Isingelikuwa Bunge kuwa na madaraka, Kamati hizo zisingeliundwa. Aidha, utaratibu wa kazi za Kamati hizo

unakamilika kwa kuripoti Bungeni. Yaani Kamati ambazo ni wakala wa Bunge zina ripoti kwa mamlaka kamili ya asili ambayo ni Bunge.

Kwa ujuma uhusiano wa ki-uwakala kati ya Bunge na Kamati zake unaonesha madaraka na majukumu yanavyohusiana kati ya Bunge na Kamati zake. Bunge ndilo lenye mamlaka kwa mujibu wa Katiba. Ili litekeleze madaraka yake kwa namna bora, Bunge linakasimu sehemu ya majukumu yake kwa Kamati za Bunge. Uhusiano unaopatikana kati ya Bunge na Kamati unatokana na Bunge kukasimu majukumu kwa Kamati za Bunge.

Uhusiano huo unajengwa kwa sifa kuu tatu. Ya kwanza ni ugawanaji wa majukumu na ubainishaji wa mipaka. Bunge ambalo lina ukuu katika muktadha huu, linakabidhi majukumu kwa Kamati za Bunge. Kanuni za Bunge zinaruhusu mgawanyo huo wa majukummu na zinaweka masharti yanayotawala uhusiano wa ki-uwakala kati ya Bunge na Kamati za Bunge.

Ya pili ni tofauti ya kina cha taarifa kuhusu jambo linalofanyiwa kazi. Kwa kawaida wakala huwa na taarifa za undani zaidi ya mkuu kwa jambo linalofanyiwa kazi. Kamati katika muktadha huu ni wakala na ni kawaida kuwa na taarifa za kina kuliko ilivyo kwa Bunge lenyewe. Kwa mfano Kamati ya Nishati na Madini inapochambua Bajeti ya Wizara ya Nishati, inakuwa na undani wa taarifa kuliko Bunge.

Ya tatu ni utegemezi unaotofautiana. Kwa kawida mkuu anamtegemea wakala hususan kwa sababu ya changamoto ya ufinyu wa muda, undani wa jambo usiojitosheleza na uelewa kuhusu jambo linalofanyiwa kazi. Bunge katika muktadha huu linazitegemea Kamati zake kwa sababu ya ufinyu wa muda wa Bunge lenyewe na undani wa taarifa zinazopatikana kwenye Kamati ambao ni mkubwa kuliko kwenye Bunge.

Kwa upande mwingine wakala anamtegemea mkuu kupata majukumu. Kwa muktadha huo, Kamati ya Bunge inategemea Bunge kupata uhalali wa mamlaka yake. Hivyo, Bunge linategemea Kamati za Bunge katika mafanikio ya kazi na Kamati zinalitegemea Bunge kwa hadidu za rejea. Utegemezi huo unashadidia uhusiano wa ki-uwakala kati ya Bunge na Kmati. Kwa maneno mengine, Kamati za Bunge zinaonekana kuwa mikono ya Bunge lakini zinapaswa kuzingatia mipaka na tija kwa Bunge.

Zaidi ya uhusiano wa ki- uwakala, ulioelezwa hapo juu, yapo maelezo ya uhusiano wa kiuwakilishi kati ya Bunge na Kamati zake. Uhusiano huu unahusisha Kamati kuliwakilisha Bunge. Lengo lake ni usimamzi wa maslahi ya Bunge.

Mfano wake ni pale Kamati inapoalikwa kwenye shughuli za umma. Dhima ya Kamati ni kuona kuwa shughuli hiyo haivurugi maslahi ya Bunge. Kualikwa kwa Kamati ya Bunge kwenye shughuli za Bunge, kunalenga kuliwezesha Bunge kuwakilishwa kwenye shughuli ya umma kama vile uzinduzi au shughuli nyingine.

Kwa kuhitimisha, umuhimu wa Kamati za Bunge ikiwa ni mada iliyoanza matoleo yaliyopita unaelezeka kwa namna mbalimbali. Katika toleo hili ufafanuzi umetolewa kwa kuangazia uhusiano kati ya Bunge na Kamati zake. Uhusiano huu ni wa Ukuu- uwakala na Uhusiano wa uwakilishi ambao umedadavuliwa.

Muhimu ni wito kwa wasomaji kufuatilia safu hii katika Toleo lijalo. Nasaha muhimu kwa hilo ni methali yenye asili ya kanda ya ziwa kwamba "BAHARI HAIJAZWI KWA MAJI YA MVUA MOJA. Msomaji unasisitizwa kuwa toleo hili lisikutoshe katika maelezo yanayohusu umuhimu wa Kamati za Bunge. Inafaa kuendelea kufuatilia matoleo yanayokuja.

# Kamati: Mifumo ya ukusanyaji Kodi iimarishwe

**Na. Lawrence Raphaely**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeitaka Serikali kuhakikisha kwamba katika Mwaka wa Fedha 2025/26 suala la kukamilisha mifumo ya ukusanyaji mapato linapewa kipaumbele ili kuongeza mapato ya Serikali.**

Akiwasilisha taarifa ya Kamati kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26, wakati wa Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge,Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Oran Njeza alisema ili mfumo wa usimamizi wa kodi uwe na ufanisi unatakiwa kuepusha masuala makuu ambayo ni kuondoa ugumu wa kulipa kodi, kuepusha matumizi ya fedha tasilimu katika kulipa kodi na kuondoa muingiliano kati ya mlipa kodi na mkusanya kodi.

"Njia pekee na inayoweza kuleta matokeo ya haraka ni matumizi ya mifumo ya kisasa," alisema.

Aliongeza kuwa Kamati inatambua kwamba Mamlaka ya Mapato imekuwa ikiendeleza ujenzi na matumizi ya mifumo ya kisasa ya ukusanyaji kodi lakini hata hivyo wamebaini kwamba Serikali imekuwa haitengi fedha ya kutosha kwa ajili ya kukamilisha mifumo hiyo.




"Kamati imebaini mamlaka ilihitaji shilingi Bilioni 400 kwa ajili ya kukamilisha mifumo. Katika kipindi cha miaka mitatu (3) Serikali imekuwa haitengi Bajeti ya kutosha ili kukamilisha zoezi hilo," alisema.

Alisema midaki katika mipaka ya nchi hasa ya mizigo imekuwa ni changamoto kubwa ambapo pamoja na athari za kiusalama zinazoweza kujitokeza kutokana na kukosekana kwa midaki, kukosekana kwa vifaa hivyo kumesababisha Maafisa wa forodha kulazimika kukagua mizigo kwa kufungua na kuangalia hali ambayo inawakutanisha na walipa kodi na kufanya majadiliano na hivyo kufungua mwanya wa kuomba rushwa.

"Hivyo, Kamati inataka Serikali kuhakikisha kwamba katika mwaka wa fedha 2025/26 ni lazima itenge bajeti kwa ajili ya ununuzi wa midaki ya mizigo," alisisitiza

Kwa upande mwingine, Mheshimiwa Njeza alisema wanaishauri Serikali kuunda Timu chini ya Wizara ya Fedha itakayohusisha wataalamu kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Tume ya Mipango na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja Wizara, Idara au Mamlaka yeyote kadri itakavyoonekana inafaa ili kupitia matumizi ya Serikali na kutoa mapendekezo ni matumizi yapi yanaweza kupunguzwa bila kuathiri utendaji kazi wa Serikali.

Alisema ni muda sasa Serikali imekuwa ikitanabaisha dhamira yake ya kupunguza matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima lakini uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hakuna maelekezo yoyote mahususi kwa Maafisa Masuuli kuhusu kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

"Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kufanya mapitio ya Matumizi ya Serikali. Nchi ya Afrika Kusini inatekeleza sera ya kupunguza matumizi ya Serikali kwa muda wa miaka mitano (5) sasa," alisema.

Mbali na hayo Kamati imeishauri Serikali kufanya mapitio ya mgawanyo wa Watumishi wa Umma na kuleta ulinganifu katika kuwagawanya ikiwemo kuweka utaratibu wa mikataba pale ambapo mtumishi amepelekwa katika kituo kwa mara ya kwanza alazimike kukaa walau miaka mitatu hadi mitano kabla ya kuomba uhamisho

Alisema moja ya jambo ambalo Kamati imelibaini ni kuwepo kwa mgawanyo usio sawa kwa watumishi wa umma ambapo kuna baadhi ya maeneo watumishi ni wengi ukilinganisha na maeneo mengine.

"Mfano, maombi mengi ya watumishi kuhama ni kutoka maeneo ya vijijini kwenda maeneo ya mijini au kutoka Wilaya za pembezoni kwenda wilaya za mijini. Ni haki ya mtumishi kuhama lakini tujiulize ni kwanini uhamisho ni kutoka maeneo ya vijijini na Wilaya za pembezoni kuelekea mijini na si vinginevyo," alisema.

Akizungumzia maeneo ya kipaumbele ya Mpango kwa mwaka 2025/26, Mheshimiwa Njeza alisema kwa upande wa Sekta ya Viwanda, Kamati inaishauri Serikali kulinda viwanda vilivyopo katika maeneo huru ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje ya nchi ili kuongeza uwezo wa viwanda hivyo kuuza bidhaa nje ya nchi na kuongeza fedha za kigeni

Alisema pia Kamati inaishauri Serikali kuweka vivutio vya uwekezaji kwenye maeneo ambayo Tanzania ina nguvu ya ushindani katika jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC kama vile madini, utalii, kilimo na gesi asilia.

Kuhusu sekta ya Madini, Mheshimiwa Njeza alisema Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali zilizopo katika sekta ya madini pamoja na kutoa msamaha wa ada ya mwaka ya leseni kwa NDC ili kuhakikisha kwamba NDC inatekeleza majukumu yake kama ipasavyo.

Kuhusu sekta ya Maji alisema Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya upatikanaji wa maji nchini kuanzia ngazi ya Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, na Mkoa ili kupata hali halisi ya upatikanaji na uhitaji wa maji.

"Tathmini hiyo itatoa majibu sahihi yatakayowezesha kuandaa mpango wa utekelezaji wa miundombinu ya maji," alisema.

Aliongeza kuwa Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuendeleza miundombinu ya maji safi na salama sambamba na miundombinu ya maji taka.

"Kamati imebaini kuwa Serikali inawekeza zaidi katika miundombinu ya maji safi na salama, na kuweka mkazo mdogo katika miundombinu ya maji taka ili kulinda usafi wa mazingira," alisema.

Kuhusu sekta ya Afya Mheshimiwa Njeza alisema kwa kuwa Bima ya Afya kwa wote bado haijaanza kutekeelezwa na kwa kuwa bado kuna changamoto kubwa ya vifaa tiba, Kamati inaishauri Serikali kutumia fedha zinazopatikana kutokana na mapato ya ushuru wa bidhaa utakaokusanywa kutoka bidhaa za urembo, vinywaji laini na vileo ili kupunguza changamoto ya vifaa tiba katika Hospitali za Mikoa na Wilaya zilizojengwa nchini.

Kuhusu utekelezaji wa Bajeti, Mheshimiwa Njeza alisema imekuwa ikitekelezwa kwa wastani wa asilimia 95.14 katika kipindi cha mwaka 2020/21 hadi 2023/24 ambapo katika miaka miwili, 2021/22 na 2023/24 bajeti ilitekelezwa kwa wastani wa asilimia 97.

"Mwenendo huu unaashiria kwamba Serikali ina uwezo wa kukusanya fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza mipango iliyojiwekea. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii," alisema.

Hata hivyo aliongeza kuwa Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa mipango na bajeti yake zinagharamiwa zaidi na mapato ya ndani na sio kutegemea mikopo.

"Hivyo kuna haja ya Serikali kuongeza mapato yake ya ndani kuweza kufikia walau asilimia 85 ya bajeti. Hivi sasa mapato ya ndani yanagharamia bajeti kwa wastani wa asilimia 70 na asilimia 30 ni mikopo," alisema.

Kuhusu ukomo wa bajeti, Mheshimiwa Njeza alisema Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha ukomo wa Bajeti kwa Mafungu unaenda sambamba na uidhinishwaji wa mwongozo wa bajeti ili kuwapa Maafisa masuuli nafasi ya kuandaa bajeti inayoendana na ukomo wa bajeti na maombi kwa mahitaji maalum yanayohitaji nyongeza ya bajeti, maombi hayo yafanyike mapema.

# Wabunge Vijana wapewa Mafunzo ya Uongozi na Maadili

**Na. Omary Machunda**

**Wabunge Vijana wamepata mafunzo juu ya masuala ya Uongozi na Maadili kwa Viongozi wa Umma yaliyofanyika katika Ukumbi wa Spika uliopo Viwanja vya Bunge Jijini Dodoma.**

Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa ushirikiano wa Ofisi ya Bunge na Taasisi ya Uongozi ya Jijini Dar Es Salaam chini ya ufadhili wa Ofisi ya Bunge, yalilenga kuwakumbusha Wabunge vijana juu ya masuala ya kuzingatia ili kuwa viongozi bora wa sasa na baadae.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kundi hili linaloundwa na wabunge wenye umri chini ya miaka 40 ambao kwa sasa wapo Sabini na mbili (72) katika Bunge hili la Kumi na Mbili, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson alielekeza wabunge hao wapate mafunzo hayo wakati wa vikao vya Kamati za Bunge.

Akifungua mafunzo hayo, Mwenyeiti wa Umoja wa Wabunge Vijana Tanzania (TYPC) Mheshimiwa Zainab Katimba alimshukuru Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuwawezesha wabunge vijana kupata ujuzi na maarifa katika nyanja mbalimbali ikiwemo uongozi, maadili, uchumi na siasa kupitia utekelezaji wa Program ya Mafunzo kwa wabunge na watumishi wa Ofisi ya Bunge.

"Waheshimiwa wabunge sote ni mashahidi kwamba Spika wetu amekuwa msaada mkubwa sana kwa Umoja wetu toka tunauanzisha, amekuwa akitupa msaada wa mawazo, ushauri na hata rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango yetu tuliyojiwekea, hivyo tunamshukuru sana," alisema.

Aidha, Mheshimiwa Katimba alisisitiza umuhimu wa wajumbe wa Umoja huo kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Spika kupitia kwa Katibu wa Bunge ili kufanikisha utekelezaji wa programu mbalimbali zilizopangwa kutekelezwa na TYPC kupitia Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa 2024 – 2029.

Yapo mambo mengi tuliyopanga kuyatekeleza katika Mpango Mkakati wetu wa Miaka Mitano, hivyo ni jukumu letu kuhakikisha tunatoa ushirikiano katika Ofisi ya Spika wa Bunge Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ili mambo yote hayo tunayoyakusudia yaweze kupata kufahamika na kupata ridhaa yake kwa ajili ya utekelezaji," alisema.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa TYPC Mheshimiwa Salome Makamba aliwaasa Wabunge hao kufuatilia kwa



**makini uwasilishaji wa mada husika kwenye mafunzo hayo ili kupata maudhui yaliyokusudiwa kutoka kwa wawezeshaji wa mafunzo hayo.**

**Waheshimiwa wWabunge vijana wenzangu tumepata bahati sana kupata mafunzo haya maalum kutoka Taasisi inayoheshimika kwenye tasnia ya Uongozi ndani na nje ya nchi yetu, hakuna asiyewafahamu Uongozi Institute, ni wabobezi wakubwa katika masuala haya, hivyo nawasihi tuwasikilize kwa akini ili tuchote maarifa haya muhimu kwetu kama viongozi vijana," alisema.**

Akiwasilisha Mada ya kwanza juu ya Sanaa na Utamaduni wa Uongozi, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi Ndg. Kadari Singo aliwaasa Wabunge vijana kupenda kujifunza mara kwa mara kupitia kwa Viongozi waliowatangulia ili kuboresha utendaji kazi wao katika majukumu mbalimbali waliyoaminiwa kuyatekeleza.

"Hakuna kiongozi aliyemtimilifu kwa asilimia mia moja na hakuna kiongozi asiyetegemea maarifa ya watu wengine, mnapaswa kujifunza kutoka kwa viongozi wengine lakini pia mjifunze hata kutoka miongoni mwa wasaidizi wenu pamoja na watu mnaowaongoza, wala msiwadharau yapo mengi yatakayowasaidia katika safari yenu ya uongozi," alisema.

Naye Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel aliwakumbusha Wabunge vijana kuchunga kauli na maneno yao wanayotoa kwa jamii wakati wote wa maisha ya uongozi kwa kuwa kauli hizo zinaishi na kutoa tathmini ya uongozi wao kwa siku za mbeleni.

Akiwasilisha mada kuhusu Uongozi wa Mabadiliko kwa Maendeleo ya Taifa, Prof. Gabriel aliwasihi Wabunge hao vijana wajitahidi kutokutoa kauli ambazo hazina ukakasi mara zote wanapozugumza na jamii.

"Kauli zina tafsiriwa kulingana na uzito wake, kauli zinatoa picha juu ya uongozi wako, kauli zinakujenga ama zinakubomoa, muwe makini sana kuchambua maneno ya kuongea na watu, tambua unaongea wakati gani, mahali gani na katika muktadha gani," alisema.

Akichangia jambo katika mafunzo hayo, Mbunge wa Korogwe Mjini Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea alishauri Ofisi ya Bunge iwawezeshe wabunge vijana kupata mafunzo kama hayo mara kwa kwa mara ili kuwajengea kumbukumbu juu ya masuala muhimu ya kuzingatia katika uongozi na utumishi wa Umma.

"Kuna mambo mengi nimejifunza kupitia mafunzo hayo, mengine nilikuwa nayajua na mengine ni mapya kwangu, hivyo tunaomba muangalie uwezekano wa kutuletea mafunzo ya namna hii mara kwa mara ili tuepuke kufanya mambo yasiyotakiwa kufanywa na viongozi," alisema.

Mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku tano pamoja na mambo mengine yalilenga kuwakumbusha Wabunge vijana juu ya mchango na nafasi zao kwenye jamii na Taifa kwa ujumla pamoja na kuwakumbusha mambo ya kuepuka kama Viongozi wakati wote wa Utumishi wao na hata baada ya kutoka kwenye nafasi hizo za uongozi.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Uongozi wa Spika wake Dkt. Tulia Ackson limekuwa likitambua uwepo wa makundi pamoja na vyama mbalimbali vya kibunge kama sehemu ya kurahisisha utatuzi wa changamoto zinazowakabili wananchi wa Tanzania kutoka katika makundi hayo.

Miongoni mwa vyama vya kibunge vinavyofanya shughuli zake bungeni ni pamoja na Umoja wa Wabunge Vijana Tanzania ambalo ni Jukwaa la Kibunge maalum kwaajili ya kushughulikia changamoto zinazowakabili vijana hapa nchini ikiwemo suala la ajira, ukosefu wa mitaji na changamoto nyingine za kiuchumi na kijamii kwa kundi hilo kubwa hapa nchini kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

Katika Mafunzo hayo, Mada zipatazo saba ziliwasilishwa na wakufunzi kutoka Taasisi ya Uongozi huku miongoni mwa Mada hizo zikiwa ni pamoja na *The Art and Practice of Leadership na Mada ya Personal Leadership and Emotional Inteligence* zilizowasilishwa na Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi Ndg. Kadari Singo.

Mada nyingine zilikuwa ni *Transformational Leadership for Sustainable National Development na Mada ya Leading Change – Towards Attainment of National Social Economic Development* zilizowasilishwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama Prof. Elisante Ole Gabriel.

Aidha, Mada ya Fostering Wellbeing for Outstanding Leadership Perfomance iliwasilishwa na Ndg. Moses Raymond wakati Dkt. Kassim Hussein alihitimisha kwa wasilisho la Mada mbili ambazo ni Good Governance, Ethics and Anti-Corruption na Mada ya Leadership Ethical Dilemmas.

Mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Umoja wa Wabunge Tanzania uliopangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2024 – 2029) huku dhamira kuu katika Mpango Mkakati huo ni kuwawezesha wajumbe wa Umoja huo kupata Taarifa, Ujuzi na Maarifa kutoka kwa wataalam wa sekta mbalimbali za kiuchumi, kijamii, kisiasa na sekta ya mawasiliano na teknolojia.

# Spika Akabidhi Uenyekiti Jukwaa la Maspika EAC, Ahimiza umoja


**Na. Debora Sanja**

**Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Novemba 13, 2024 alikabidhi nafasi ya Mwenyekiti wa Jukwaa la Maspika wa Bunge wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Spika wa Bunge la Kenya, Mheshimiwa Moses Wetang'ula.**

Mheshimiwa Spika alikabidhi nafasi hiyo aliyoitumikia kwa kipindi cha mwaka mmoja, katika mkutano wa Maspika uliofanyika jijini Nairobi nchini Kenya.

Akizungumza kabla ya kukabidhi nafasi hiyo, Mheshimiwa Spika aliwashukuru maspika kwa umoja na kujitoa kwao katika kuendeleza malengo ya jukwaa hilo.

Alimnukuu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kusisitiza umuhimu wa kudumisha umoja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo kwa sasa ina wanachama 8 huku ikiwaleta pamoja zaidi ya wananchi milioni kumi na mbili.



Spika wa Bunge, Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson** katika picha ya pamoja na Spika wa Bunge la Kenya Mheshimiwa **Moses Wetang'ula** wakati wa makabidhiano ya nafasi ya Mwenyekiti wa Jukwaa la Maspika wa Bunge wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

> **Maendeleo ya Jumuiya yanaonekana siyo kwa kuongezeka kwa wanachama peke yake bali pia katika ukuaji wa uchumi ambao licha ya changamoto za kiuchumi lakini ulikuwa kwa wastani wa asilimia 4.5.**
>
> *- Dkt Tulia Ackson*



Spika wa Bunge, Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson** na Katibu wa Bunge, Ndugu **Baraka Leonard** waliposhiriki katika kikao cha makabidhiano ya nafasi ya Mwenyekiti wa Jukwaa la Maspika wa Bunge wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Alisema katika kipindi chake akiwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Maspika, kumekuwepo mafanikio mengi ikiwemo uimarishaji wa mifumo ya sheria katika nchi wanachama pamoja na kuridhiwa kwa itifaki muhumu za kukuza ushirikiano wa kikanda.

"Vilevile tumepiga hatua kubwa katika kukuza usawa wa kijinsia ndani ya vyombo vyetu vya kutunga sheria pamoja na kuanzisha mipango ya kuongeza uwakilishi wa wanawake Bungeni," alisema.

Alisema Maendeleo ya Jumuiya yanaonekana siyo kwa kuongezeka kwa wanachama peke yake bali pia katika ukuaji wa uchumi ambao licha ya changamoto za kiuchumi lakini ulikuwa kwa wastani wa asilimia 4.5.

"Hata hivyo, katika malengo yetu ya kifedha ni muhimu kuhakikisha kwamba kila raia wa Afrika Mashariki wananufaika moja moja na maendeleo haya," alisema.

Mheshimiwa Dkt. Tulia alisema bado Jumuiya ya Afrika Mashariki inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo vita na mizozo inayoendelea, tofauti ya kiuchumi, madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa na uharibufu wa mazingira pamoja na mikazo inayosababishwa na uchumi wa ulimwengu.

Alisema migogoro hiyo imekuwa siyo tishio tu kwa uchumi wa wananchi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, bali pia kwa wananchi wake huku akitaja Mgogoro wa Sudan



Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Katikati ya waliokaa) katika picha ya pamoja na Maspika wa Mabunge ya Afrika Mashariki (waliokaa) pamoja na makatibu wa Mabunge hayo (waliosimama)wakati wa makabidhiano ya nafasi ya Mwenyekiti wa Jukwaa la Maspika wa Bunge wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

ya Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambayo pia huathiri nchi za Jirani na hivyo kuharibu mipango ya kikanda.

Kwa upande mwingine, Mheshimiwa Spika alieleza matarajio yake kutoka katika Jukwaa hilo la Maspika kwamba litaendelea kutetea sera zinazotoa kipaumbele kwa maendeleo endelevu na kuhakikisha hakuna mtu anayeachwa nyuma.

"Natarajia pia Jukwaa litaendelea kuimarisha ushirikiano na mashirika ya kiraia kwa kuwa ni muhimu katika utekelezaji wa mipango ya kushughulikia masuala ya kijamii kama vile kupunguza umasikini na upatikanaji wa elimu," alisema.

Alisisitiza kukumbatia teknolojia kama chombo cha kuongeza uwazi na uwajibikaji katika michakato ya sheria na kwamba kwa kutumia majukwa ya kidijitali wanaweza kushirikiana kwa ufanisi zaidi na wapiga kura na kukuza ushiriki wa umma katika utawala.

Alisema kwa siku zijazo umuhimu wa teknolojia, hasa Akili Mnemba (AI) katika kukuza uchumi ni muhimu na kwamba, AI inatarajiwa kuboresha huduma za umma kwa kuongeza ufanisi na kupunguza gharama.

"Ni lazima Wabunge kuunda mifumo ambayo itahakikisha IA inatumika kwa uwazi na uwajibikaji, kutafakari maaadili yetu na kuheshimu haki za wananchi.

"Jukwaa la Maspika lina jukumu muhimu la kutetea sera zinazoongoza utekelezaji wa maadili ya AI katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhakikisha teknolojia hii inaendeleza maendeleo bila kuathiri misingi yetu ya demokrasia, uwajibikaji na utu wetu, alisema.

Alisema ni muhimu kwa wanachama wa EAC kutekeleza Azimio kuhusu 'Mchango wa Akili Mnemba katika Demokrasia, Haki za Binadamu na Utawala wa Sheria' ambalo lilipitishwa na IPU katika mkutano wake wa 149.

Alisema Azimio hilo linaeleza namna ya kuunganisha AI katika jamii kwa njia ambayo inaheshimu haki za binadamu na kuzingatia maadili.

Akizungumzia nafasi yake ya Rais wa IPU, Mheshimiwa Spika alisema anajivunia jukumu hilo kwa Afrika Mashariki na Bara lote la Afrika na kwamba katika kipindi cha miaka miwili ijayo,EAC ina fursa ya kipekee ya kupaza sauti yake katika majukwaa ya kimataifa.

"Nafasi yangu IPU inatoa fursa ya kuchagiza mahitaji maalumu na vipaumbele vya Afrika Mashariki, kushawishi mijadala ya kimataifa ya kibunge juu ya masuala muhimu kama hali ya hewa, ujenzi wa amani na uthabiti wa uchumi, tunapaswa kutumia fursa hii kuimarisha ushirikiano wa kikanda," alisema.

Aidha, Mheshimiwa Spika alitumia nafasi hiyo kuwatia moyo maspika wanawake katika Jumuiya hiyo na kuwataka waendelee kuongoza kwa kujiamini kwa kuwa uongozi wao unafungua njia na ni mfano kwa wanawake wengine.

Aliahidi pia kufanya kazi kwa ukaribu na Maspika wote kuhakikisha maslahi ya Afrika Mashariki yanawakilishwa ipasavyo wakati wa uongozi wake kama Rais wa IPU.

"Afrika Mashariki ijayo inategemea nguvu ya mahusiano yetu na uwezo wa kuunganisha agenda za mabunge. Jukwaa la Maspika lina jukumu la kipekee la kuhakikisha mabunge yanaunga mkono kazi za Bunge la Afrika Mashariki na kutetea Kanuni za Mkataba wa EAC.

Bunge la Afrika Mashariki hutumika kama sauti ya watu katika Kanda nzima, lakini linaweza kuwa na ufanisi ikiwa sisi mabunge ya kitaifa tutaunga mkono na kutekeleza maazimio yake," alisema.

Alisema maono ya Jumuiya ya 2050 yanasisitiza Afrika Mashariki yenye mafanikio, ushindani, usalama na umoja wa kisiasa na kwamba jukumu la Jukwaa la Maspika ni kutafsiri maono hayo kuwa halisi kwa wananchi.


"Kwa sasa zaidi ya asilimia 65 ya idadi ya watu wa EAC ni vijana wa miaka 30, idadi hii ya vijana ina uwezo mkubwa na inatupa jukumu la kutengeneza mazingira ambayo vijana wanaweza kustawi na kutoa mchango kwa jamii.

"Kupitia uratibu wa kisheria na kujitoa kwa pamoja katika ajenda yetu ya mtangamano, tunaweza kujenga Afrika Mashariki ambayo inatoa fursa kwa raia wake wote bila kujali utaifa," alisema.

**"Afrika Mashariki ijayo inategemea nguvu ya mahusiano yetu na uwezo wa kuunganisha agenda za mabunge. Jukwaa la Maspika lina jukumu la kipekee la kuhakikisha mabunge yanaunga mkono kazi za Bunge la Afrika Mashariki na kutetea Kanuni za Mkataba wa EAC."**



Spika wa Bunge la Tanzania, Mheshimiwa **Dkt.Tulia Ackson**



Katibu wa Bunge la Tanzania, Ndg. **Baraka Leonard** katika picha ya pamoja na Naibu Katibu wa Bunge la Kenya, Bw. **Jeremiah Ndombi**

Akihitimisha hotuba yake, Mheshimiwa Dtk. Tulia alitoa shukrani kwa maspika wote kwa kuwa kujitoa na maono yao kumekuwa na thamani katika uongozi wake.

"Asanteni kwa kuwa sehemu muhimu katika safari yangu iliyojaa kujifunza na ukuaji binafsi. Wakati huu siyo wa kuaga tu bali ni wito wa kuungana kwa nguvu mpya tunapoanza sura inayofuata ya safari yetu ya pamoja.

"Nawatia moyo kubaki imara kuwahudumia watu wenu, majukumu ya Spika ni muhimu siyo tu kwa ajili ya kutunga sheria lakini pia kama viongozi ambao wanamchango katika kesho ijayo ya mataifa yenu. Tuendelee kuweka matumaini miongoni mwa wananchi wetu kwa kuonyesha uadilifu na huruma," alisema.

Mheshimiwa Dkt. Tulia alisema anao uhakika kwamba mrithi wake katika nafasi hiyo ya Mwenyekiti ataendelea kuendeleza ajenda za ushirikiano wa EAC na kuifanya Jumuiya hiyo kutekeleza maono ya umoja, amani na ustawi wa pamoja.

Alitoa wito kwa wanachama wote wa Jumuiya hiyo kuendeleza moyo wa ushirikiano ikiwemo kutumia nguvu ya pamoja na uzoefu mbalimbali kushinda changamoto na kutoa fursa kwa ajili ya ukuaji.

Mheshimiwa Spika alimalizia kwa kumnukuu Rais wa Uganda, Mheshimiwa Yoweri Museveni kuhimiza umoja, kuweka kipaumbele amani na usalama, kufanya kazi kwa bidii kutengeneza Afrika Mashariki yenye ustawi kwa watu wote.

Mkutano huo wa Maspika ulitanguliwa na Mkutano wa Makatibu wa Bunge wa Mabunge ya EAC ambapo pia Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard alikabidhi nafasi ya Mwenyekiti wa Mkutano huo kwa Katibu wa Bunge la Kenya.

Kwa upande wake akitoa hotuba ya kukabidhi nafasi hiyo, aliwashukuru Makatibu wa Bunge kwa kumpa ushirikiano ndani ya kipindi kifupi tangu alipoteuliwa kushika nafasi ya Katibu wa Bunge la Tanzania.

Pamoja na kushukuru kwa mapokezi mazuri kutoka kwa Mwenyeji wa Mkutano huo ambaye ni Bunge la Kenya, Katibu wa Bunge aliishukuru Sekretarieti ya Mkutano huo ambao ni Bunge la Afrika Mashariki (EALA) kwa maandalizi mazuri ya Mkutano.

Alimpongeza Katibu wa Bunge la Kenya ambaye kwa niaba yake alikuwepo Naibu Katibu wa Bunge, Jeremiah Ndombi kwa kuchukua nafasi ya Mwenyekiti na kumtakia kila la heri.

Katibu wa Bunge pia alisisitiza umuhimu wa lugha ya kiswahili kutumika katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mkutano wa Maspika wa Mabunge ya Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unatarajiwa kufanyika Tanzania Mei, 2025.

# Bunge Kinara Tuzo Za Uandaaji Bora Wa Hesabu

**Na Deonisius Simba.**

**Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeibuka mshindi wa kwanza katika Uandaaji Bora wa Hesabu za Mwaka 2023 katika Kundi la Wizara na Taasisi za Serikali.**

Tuzo hiyo ilitolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) tarehe 29 Novemba, 2024 katika Hoteli ya APC iliyopo Bunju Jijini Dar es Salaam wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wahasibu na Wakaguzi.

Zaidi ya hayo, taasisi hizo zinatathminiwa kwa kufuata viwango vya utayarishaji wa hesabu, sheria za utawala bora, na miongozo ya ukaguzi na uandaaji wa hesabu kama ilivyotolewa na NBAA.

Kufuata na kukidhi vigezo vyote hivyo ni hatua muhimu inayothibitisha uwazi, uaminifu na ubora wa taarifa za fedha na kihasibu za taasisi husika.



Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt Tulia Ackson akionyesha Bungeni tuzo ambayo Ofisi ya Bunge imepewa baada ya kuibuka mshindi wa kwanza katika uandaaji bora wa Hesabu za Mwaka 2023 katika Kundi la Wizara na Taasisi za Serikali.

Kwa Mwaka 2023, Taasisi 86 zilikaguliwa na kushiriki katika tuzo za uandaaji wa hesabu bora. Tuzo hizi hutolewa kwa taasisi zinazokidhi vigezo vya kitaifa na kimataifa katika uandaaji wa taarifa za fedha na kihasibu.

Masharti muhimu ya kushinda tuzo hizi ni pamoja na taasisi kuwa imesajiliwa na NBAA, hesabu zake kuwa zimekaguliwa na kupewa hati safi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndg. Baraka Leonard alisema tuzo hizo ni uthibitisho wa dhamira ya Bunge ya kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na weledi katika matumizi sahihi ya viwango vya juu vya kitaalamu katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa zake za kifedha.

Ndg. Leonard alisema kuwa Ofisi ya Bunge inayo watumishi wenye weledi wa kutosha katika usimamizi bora wa kifedha



**Tumejipanga vizuri na tutaendelea kufanya kazi kama timu. Ushirikiano huu ndiyo nguzo kuu ya mafanikio yetu,**

*- Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Leonard.*

Katibu wa Bunge, Ndg. **Baraka Leonard** akimkabidhi Spika wa Bunge, Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson** Tuzo ya uandaaji Bora wa Hesabu za Mwaka 2023 katika Kundi la Wizara na Taasisi za Serikali, Kushoto ni Ndg **Layson Mwanjisi,** Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Bunge

na uandaaji wa taarifa zinazozingatia viwango vya kimataifa. "Tuzo hizi ni uthibitisho kuwa Bunge tunao watumishi wenye weledi katika kusimamia, kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha kwa kuzingatia viwango vya kimataifa".

Ameongeza kwa kusema kuwa, Bunge limejipanga zaidi kwa kuimarisha utayarishaji wa taarifa za kifedha kwa Mwaka 2024 kwa kuendelea kuwapatia mafunzo wahasibu wake.

Vilevile, amewapongeza watumishi wa Bunge kwa kazi kubwa waliyoifanya kuhakikisha taarifa zao zinakaguliwa na kupitishwa na wakaguzi wa nje kwa viwango bora.

"Tumejipanga vizuri na tutaendelea kufanya kazi kama timu. Ushirikiano huu ndiyo nguzo kuu ya mafanikio yetu," alisema Ndg. Leonard.

Katika hafla hiyo, mgeni rasmi alikuwa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Natu Mwamba aliyewakilishwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (IAG), CPA. Benjamin Magai.

Kwa upande wake Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizungumza kabla ya kuonesha tuzo hiyo tarehe 28 Januari, 2025 wakati akiongoza Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge Jijini Dodoma, alisema mhimili wa Bunge umeonesha mfano bora wa kusimamia weledi wa wahasibu na wakaguzi katika kusimamia mali za umma kwa kuzingatia pia Bunge lina jukumu la kusimamia taasisi nyingine za umma.

Vilevile, aliwapongeza Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Leonard, Mhasibu Mkuu wa Bunge, CPA Layson Mwanjisi pamoja na watumishi wote wa Bunge kwa kazi nzuri iliyofanyika ya uandaaji bora wa hesabu iliyosaidia kupata tuzo hiyo.

Aidha, alitoa rai kwa wahasibu na wakaguzi wote nchini kuendelea kufanya kazi zao kwa ufanisi kila mwaka wa fedha ili kuondoa changamoto za matumizi mabaya ya fedha za umma.

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) imekuwa ikiandaa tuzo kila mwaka kwa waandaaji wa taarifa za kifedha zinazozingatia viwango vya kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na Sekta za Kibiashara (IFRS).

# Waziri Mkuu: Andaeni taarifa za utekezaji Maazimio ya Bunge



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Kassim Majaliwa** akizungumza Bungeni.

**Na. Halima Laizer**

**Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa ameziagiza Wizara zote kuandaa taarifa za utekelezaji na ufafanuzi wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge za Usimamizi wa Fedha za Umma wakati zikiwasilisha taarifa zake katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge.**

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo wakati akisoma hotuba ya kuarishwa kwa Mkutano huo Novemba 8, 2024.

Wakati wa Mkutano huo, Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) ziliwasilisha taarifa za mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Majaliwa alisema hoja za Waheshimiwa Wabunge zitaisaidia Serikali kuimarisha utendaji wake katika kuwahudumia wananchi.

“Hivyo basi nawahakikishia kwamba Serikali imepokea michango yenu na inaahidi kuifanyia kazi ipasavyo.

“Ofisi ya Waziri Mkuu itaandaa taarifa jumuishi ya Serikali na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Spika ikiwa ni mrejesho wa utekelezaji maoni na mapendekezo ya Kamati,” alisema

Waziri Mkuu aliwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao yote yenye tija na kujenga na kwamba anaamini michango hiyo itaisaidia Serikali kutekeleza mapendekezo na maazimio yaliyotolewa kupitia taarifa hizo za Kamati.

Aidha, kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2024/2025, Waziri Mkuu aliwaelekeza Maafisa Masuuli wote nchini kuhakikisha wanafanyia kazi hoja, ushauri na maoni pamoja na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge ikiwa ni pamoja na kuainisha vipaumbele muhimu.

Alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kuchochea uchumi shindani, kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa bidhaa viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji wa biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

Alisema Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambao umejikita kuendeleza

**Alisema lengo ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2033, asilimia 80 ya Watanzania wote wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ambayo ni Gesi, Umeme, Makaa ya mawe na KUNIPOA.**

kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo ya maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Waziri Mkuu alisema katika kipindi cha robo ya kwanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025, ridhaa ya shilingi trilioni 11.67 ilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

"Matumizi ya maendeleo yamejumuisha kugharamia miradi na programu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), ujenzi na ukarabati wa barabara, madaraja na viwanja vya ndege na mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere.

"Mafanikio hayo yanatokana na mikakati mbalimbali iliyowekwa na Serikali, hiyo ni pamoja na kuendelea kuimarisha na kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato na kuhamasisha matumizi ya mashine za kutolea risiti za kieletroniki," alisema.

Aliwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao katika Mpango huo pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa mwaka 2025/2026.

Alisema Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaweka mkazo katika maeneo ya miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa na kujielekeza katika vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026.

Akizungumzia kuhusu maswali yalioulizwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, Waziri Mkuu alisema jumla ya maswali 133 ya msingi na mengine 149 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali.

Alisema maswali sita ya papo kwa papo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Kwa upande wa miswada ya sheria, alisema Bunge lilipokea na kusoma kwa mara ya kwanza miswada minne.

Aliitaja miswada hiyo kuwa ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2024, Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kazi wa Mwaka 2024 na Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi wa mwaka 2024.

Katika hotuba yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu alimpongeza Ndugu Baraka Leonard kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge na kumhakikishia kuwa Serikali itampa ushirikiano wote unaohitajika wakati wote anapotekeleza majukumu yake.

Aidha, alimpongeza Mheshimiwa Spika na Rais wa Umoja wa Mabunge ya Duniani (IPU), kwa kuongoza Mkutano wa 149 wa Umoja wa Mabunge Dunia uliofanyika kuanzia tarehe 13 Oktoba, 2024 huko Geneva, Uswisi.

"Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia ushupavu uliouonesha wakati wa mkutano huo na jinsi ulivyoonesha msimamo usioyumba wakati wote.

"Sina shaka, uongozi wako utaweka alama katika historia ya uongozi wa Umoja wa Mabunge Duniani, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla, tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Spika ili aendelee na majukumu yake kwa ufanisi," alisema.

Kuhusu suala la matumizi ya nishati safi, aliitaka Wizara ya Nishati kuendelea kufanya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa mkakati wa matumizi ya nishati Safi ya Kupikia.

Aliwaagiza wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya wote ifikapo Desemba mwaka huu watoe taarifa ya utekelezaji kuonesha taasisi ngapi ambazo tayari zimetekeleza agizo hilo.

Alisema lengo ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2033, asilimia 80 ya Watanzania wote wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ambayo ni gesi, umeme, makaa ya mawe na KUNIPOA.

## Michezo

Waziri Mkuu alisema Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuweka mikakati mbalimbali katika Sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo ili kuleta tija na mafanikio na kwamba inaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa lengo la kufanikisha mipango ya maendeleo ya sekta hiyo.

Kuhusu maandalizi ya Michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika ya Mwaka 2027 (AFCON 2027), alisema Serikali imeshaanza mchakato wa maandalizi ya mashindano hayo yanayotarajiwa kufanyika mwaka 2027.

Alisema miongoni mwa maandalizi hayo ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu, uendeshaji wa masoko ya utalii, uandaaji wa Timu ya Taifa, ulinzi na usalama.

Serikali inatekeleza miradi ya ujenzi wa viwanja vya michezo ikiwemo kiwanja cha Arusha, pamoja na kukarabati Uwanja vya Benjamin Mkapa, Uhuru na Amani - Zanzibar ili kukidhi vigezo vya mashindano ya Michuano ya Mataifa ya Afrika (CHAN).

Akihitimisha hoja yake, Waziri Mkuu aliziagiza Kamati za Maafa ngazi ya vijiji, wilaya, mkoa na Taifa kujipanga kikamilifu kukabiliana na changamoto za mvua endapo zitajitokeza.

Aidha, aliwataka wakulima wote nchini kutumia mvua hizo kulima mazao yanayoendana na upatikanaji wa mvua katika maeneo yao na kuzingatia ushauri wa wataalamu wa kilimo.

"Watanzania wote tuendelee kujenga tabia ya kufuatilia taarifa za utabiri wa hali ya hewa pamoja na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Serikali ikiwemo kuhama kwenye maeneo hatarishi na kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo yaliyo salama," alisema.

Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa Hoja ya Kuahirisha Bunge hadi tarehe 28 Januari, 2025.

# Bunge Lampongeza Rais Samia Kuandaa Mkutano Wa Nishati Afrika



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan** akihutubia Mkutano wa Nishati Afrika (Mission 300) Mwaka 2025 uliofanyika Jijini Dar es Salaam

**Na. Zuhura Mtatifikolo**

**Bunge limepitisha azimio la kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika (Mission 300) Mwaka 2025 kwa kufanikisha mkutano huo ambao umeleta sifa ya kipekee kwa nchi na watanzania wamenufaika na fursa mbalimbali.**

Mkutano huo ulifanyika Januari 27na 28, 2025 Jijini Dar es Saalam na kuwakutanisha Wakuu wa Serikali na nchi za Afrika, viongozi wa wafantabiashara, washirika wa maendeleo, wakuu wa Taasisi za Kimataifa ikiwamo Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani (IMF), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) na Rockerfeller Foundation pamoja na wadau wakuu kwenye nyanja mbalimbali katika juhudi kubwa za kuwafikishia umeme watu milioni 300 Barani Afrika ifikapo mwaka 2030.

Tanzania chini ya Rais Samia ilikuwa mwenyeji wa Mkutano huo na kuhudhuriwa na Wakuu wa nchi na Serikali wapatao 21 ambapo pamoja na mambo mengine, Mkutano huo ulilenga kutafuta majawabu ya tatizo la nishati Barani Afrika na kuharakisha ufikiwaji wa maendeleo endelevu katika Bara la Afrika kwa ujumla.

Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt.Tulia Ackson, anasema Bunge limeazimia kumpongeza Rais Samia na azimio hilo litapelekwa kwa maandishi kwa Mheshimiwa Rais.

"Nipongeze Umoja wa Wabunge Wanawake kwa kuja na wazo hili, nimpongeze Mwenyekiti wetu wa TWPG Mheshimiwa Shally Raymond, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Katibu wetu Mheshimiwa Agness Hokororo na tunawapongeza sana viongozi wetu,"alisema.

Alisema ni vizuri kumpongeza Rais kwa mambo anayoyafanya ili kumtia moyo kwa kuwa Wabunge ni mashahidi wa mafanikio yanayoonekana kwenye maeneo yao.



Mbunge wa Viti maalum (CCM), Mheshimiwa **Asia Halamga** akisoma Bungeni Azimio la kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kufanikisha Mkutano wa Nishati Afrika (Mission 300) Mwaka 2025 uliofanyika Jijini Dar es Salaam.

Awali, akisoma azimio hilo, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mheshimiwa Asia Halamga alisema mkutano huo ulikuwa na manufaa makubwa sana kwa uchumi wa Tanzania na Bara zima la Afrika.

Alisema wawekezaji katika sekta ya hoteli na malazi, usafiri na usafirishaji, wauzaji wa vyakula na vinywaji, wauzaji wa bidhaa mbalimbali pamoja na sekta ya utalii wamenufaika na Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo.

"Kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano, wafanyabiashara wameweza kutengeneza mtandao katika biashara zao kwa kufanya mazungumzo ya kibiashara yaani Business to Business na Business to Customer (B2B na B2C) pembezoni mwa Mkutano huo na tumeingiza fedha za kigeni suala ambalo limeleta manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi yetu,"alisema.

Alisema mkutano huo umeazimia ikiwamo mataifa mbalimbali yametoa ahadi za mipango ya mageuzi makubwa ya nishati yanayolenga kuimarisha nishati mbadala na jadidifu, kuboreshwa kwa gridi za umeme na kuimarisha upatikanaji wa suluhu ya nishati safi za kupikia.

Alisema mkutano huo pia, uliazimia mipango ya Kitaifa ya nishati kwa lengo la kuvutia wawekezaji na mageuzi ya sera na kutolewa kwa ahadi za ufadhili kutoka taasisi za kifedha za kimataifa kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia.

Alisema manufaa mengine ni kuvutia sekta binafsi kuwekeza mitaji katika sekta ya nishati Barani Afrika na kufikiwa kwa Azimio la Dar es Salaam ambalo limelenga kuhakikisha upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 Barani Afrika ifikapo mwaka 2030.

"Azimio la Dar es Salaam lina manufaa makubwa kwa Bara la Afrika kwani kupitia azimio hilo imekubalika kwamba upo umuhimu wa kuzingatia usawa wa kijinsia katika kuongeza upatikanaji wa nishati hasa kwa wanawake na wafanyakazi ili kuimarisha mustakabali endelevu,"alisema Mheshimiwa Halamga.

> Rais Samia ameonesha nia ya dhati kuhakikisha kuwa **ifikapo 2030 asilimia 75** ya Watanzania watakuwa wamepata nishati safi ya kupikia na hatimaye kufikia 2034 Watanzania wote wawe wamepata nishati safi ya kupikia

Vilevile, Azimio hilo linasisitiza umuhimu wa kuunganisha nishati miongoni mwa nchi za Afrika, kutumia vyanzo vya nishati jadidifu kama jua, upepo, umeme wa maji, nishati za joto ardhi ili kuwa na mifumo imara ya nishati.

Alisema wanampongeza kwa mafanikio hayo na kuhudhuriwa na wageni takribani 2,600 wakiwamo Wakuu wa Serikali na nchi takribani 21 kutoka Barani Afrika, Mawaziri na Viongozi mbalimbali wa Taasisi za Kimataifa za Fedha na Nishati na wadau wengine.

Alisema mkutano ulikuwa wa weledi na viwango vya hali ya juu Kimataifa kutokana na uratibu mzuri uliofanywa na serikali anayoiongoza.

"Rais Samia ameonesha nia ya dhati kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 asilimia 75 ya watanzania watakuwa wamepata nishati safi ya kupikia na hatimaye kufikia mwaka 2034 Watanzania wote wawe wamepata nishati safi ya kupikia,"alisema.

## Wabunge waunga Mkono

Akichangia azimio hilo, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Mheshimiwa Jesca Kishoa alisema anaungana na wajumbe wa mkutano mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa uamuzi wa kumpitisha Rais Samia kuwa mgombea urais katika uchaguzi mkuu mwaka huu kwa maono aliyonayo kwenye nishati, uchumi na diplomasia.

Alieleza kuwa Rais Samia amefanya kazi ya kuimarisha diplomasia, uchumi na kuwa kinara wa matumizi ya nishati safi.

"Kwa haya yaliyofanyika mkutano mkuu na mengine haya mambo yamehalalisha maamuzi ya mkutano mkuu wa CCM yaliyofanyika mwaka huu na mimi naungana kwa asilimia 100 kwa uamuzi wa wajumbe wa CCM walioufanya," alisema.

Naye, Mbunge wa Singida Magharibi (CCM), Mheshimiwa Elibariki Kingu, alisema Mheshimiwa Rais Samia ameionesha dunia na Afrika kuwa ni mwanamke shupavu na uwezo wa kuleta mabadiliko duniani.

### Kauli ya Dkt.Biteko

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko akichangia azimio hilo, alisema mpango wa nishati uliofikiwa huo wangepambana na wasingezidi milioni 5.2," alisema.

Alieeleza kuwa kwenye nishati safi ya kupikia wanataka watoke asilimia 9.9 kwenda asilimia 75 ndani ya miaka mitano.

"Mchango wa Nishati jadidifu itoke asilimia 56 iliyopo twende asilimia 65 na tutalifikia suala hili bila wasiwasi wowote," alisema.

Alisema mkutano huo ulikuwa na mwitikio mkubwa wa watu kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia.

"Sababu mbili zilizofanya mkutano huu kuja Tanzania ni




**Kuhusu mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, alisema utakamilika rasmi mwishoni mwa mwezi Februari mwaka huu baada ya kukabidhiwa mtambo wa tisa wa kuzalisha umeme.**

Hadi leo asubuhi mitambo yote nane imekabidhiwa na mtambo mmoja wa tisa utakabidhiwa mwishoni mwa Februari mwaka huu na mradi wa bwawa hili tutakuwa tumemaliza,

- Waziri Dkt Doto Biteko

kwenye mkutano huo umetoa viashiria vitano ikiwamo cha upatikanaji wa umeme kwa Tanzania ni asilimia 78.4.

Alisema katika mpango huo waliosaini miaka mitano ijayo Tanzania itafikia upatikanaji wa umeme kwa asilimia 100.

"Uunganishaji umeme na wateja leo tunapozungumza hatua tuliyonayo tumeunganisha wateja milioni 5.5 na mpango ni kupeleka kwa wateja milioni 13.5 na usingekuwa mpango kuimarika kwa diplomasia yetu na mataifa mengine na haijaimarishwa na mwingine ni yeye Mheshimiwa Rais Samia, kasi kubwa ya upelekaji umeme kwa wananchi hasa vijijini. Benki ya Dunia walivyofanya tathmini mwaka jana Tanzania iliongoza na wakaona mahali pekee pa kupeleka mpango huu ni Tanzania," alisema.

Alibainisha kuwa Rais Samia ametoa msukumo mkubwa kwenye sekta ya nishati na kuahidi makubaliano yaliyofikiwa kwenye mkutano huo atayasimamia na hayatabaki kwenye makaratasi.

Kuhusu mradi wa Bwawa la kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, alisema utakamilika rasmi mwishoni mwa mwezi Februari mwaka huu baada ya kukabidhiwa mtambo wa tisa wa kuzalisha umeme.

"Hadi leo asubuhi mitambo yote nane imekabidhiwa na mtambo mmoja wa tisa utakabidhiwa mwishoni mwa Februari mwaka huu na mradi wa bwawa hili tutakuwa tumemaliza," alisema.

# Usimamizi wa Kibunge wa Fedha za Umma



Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) katika mojawapo ya kikao kazi Jijini Dodoma

**Na. Athuman Hussein**, *ndc*
a.brambati@Bunge.go.tz

**Mwishilizo wa ufafanuzi kuhusu 'Usimamizi wa Kibunge wa Fedha za Umma" unaungana na mwendelezo unaoanza katika toleo hili. Kwa kukumbushia, toleo lililopita, lilitoa ufafanuzi kuhusu mamlaka, madaraka na majukumu ya Kamati za Bunge katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Ombwe la kiuelewa na mkanganyiko kuhusu dhana hizo tatu ni eneo kuu katika toleo lililopita.**

Muhimu katika hayo ni kiini cha makala ambacho kipo kwenye lengo la usimamizi wa kibunge, hususani uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Mwanasiasa, Afisa wa Jeshi na Mwandishi wa Uingereza aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo, alipata kunukuliwa akizungumzia uwajibikaji wa viongozi. Kiongozi huyo wa nchi ambayo ndiyo chimbuko la taratibu za kibunge kwa nchi za Jumuiya ya Madola, akiwa mliberali kiuchumi alisisitisa uwajibikaji.

Katika msisitizo wake aliwalenga viongozi kwa kuwakumbusha kuwa 'uwajibikaji ni gharama ya ukuu''. Alimaanisha kwamba, kwa viongozi na watendaji wakuu' uwajibikaji ni bei wanayolipa kwa dhamana ya kuwaongoza wengine.'' Maana yake ni kuwa jambo lolote kuhusu uwajibikaji linagusa uongozi. Usimamizi wa fedha za umma unagusa uwajibikaji, hivyo ni jambo miongoni mwa mambo katika uongozi kwa wabunge, watendaji na watumishi wengine wa umma.

Nchini Tanzania, Rais wa kwanza katika historia ya nchi hii alisisitiza kuwa fedha za umma ni mali ya wananchi na kila mtumishi wa umma anawajibika kutumia mali hiyo kwa manufaa ya wananchi. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linalo wajibu wa kusimamia na kufuatilia matumizi ya Fedha za Umma.

Katika muktadaha huo, toleo lililopita liliahidi ufafanuzi wa mchakato wa usimamizi wa kibunge wa fedha za umma. Kwa kutambua kuwa "Ahadi ni deni, na deni linapaswa kulipwa'', toleo hili linaeleza mchakato wa usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma. Ufafanuzi huu ni utekelezaji wa ahadi liyotolewa kwenye safu ya usimamizi wa kibunge wa fedha za umma kwa toleo lililopita.

Mchakato wa kibunge wa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma unahusu mfululizo wa hatua au shughuli za kibunge ili kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Lengo hasa ni kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake kwa ufanisi katika eneo la usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Ibara ya 63 (2) ya Katiba kama ilivyoelezwa katika matoleo yaliyopita, imelipa Bunge madaraka ya kuisimamia Serikali. Kwa madaraka hayo Bunge lina jukumu la kufuatilia matumizi ya fedha za umma. Utekelezaji wa majukumu hayo unawezesha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Bunge kwa desturi yake huendesha mambo yake kwa mfuatano maalumu wa mambo au shughuli ambao unazingatia mpangilio uliowekewa utaratibu kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za Bunge. Desturi hii inasisitizwa na



Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Mheshimiwa **Japhet Hasunga** akizungumza wakati wa kikao cha kamati hiyo. Kulia ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa **Nagenjwa Kaboyoka**

usemi wa busara kwamba: **Shika Adabu, Adabu Itakuletea Heshima**. Ujumbe wake ni pamoja na mkazo unaowekwa kwenye misingi ya mchakato wa kibunge kuzingatiwa ifaavyo, ili kutapata matokeo mazuri.

Maelezo hayo yanasuhubiana na umuhimu wa mchakato wa kibunge wa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa msingi huo, safu hii haina budi kujumuisha ufafanuzi wa mchakato wa huo. Kwa wasomaji wa safu hii, ni muhimu kuyachukua hayo kwa mtazamo ndani ya msemo: "Usipokosa kuelewa, hutakuwa na shaka". Wito kwa msomaji, fuatilia maelezo haya kwa umakini ili uwe miongoni mwa wasio na shaka kuhusu usimamizi wa ikibunge wa matumizi ya fedha za umma.

Mchakato wa kibunge wa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma una namna mbalimbali za kuueleza. Namna hizo zinaweza kuwekwa katika kategoria kuu mbili: Ya kwanza ni kategoria ya mchakato mrefu kwa kujumuisha Bunge na wadau wengine nje ya Bunge kama wahusika na kategoria ya pili ni mchakato halisi ndani ya Bunge lenyewe.

Mchakato mrefu unajumuisha hatua za uidhinishaji wa bajeti na utekelezaji wa bajeti. Vilevile, unahusu ufuatiliaji wa matumizi ya fedha. Mengine ni uwasilishaji wa taarifa za hesabu za fedha, ukaguzi wa hesabu za fedha, uwekaji mezani *(laying on the table)* ripoti za ukaguzi na mwisho Bunge kuamua kupitia maazimio ya Bunge kuhusu matokeo ya uchambuzi wa ripoti za ukaguzi.

Mchakato mfupi unaelezwa kuanzia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilishwa Bungeni hadi Taarifa za Kamati zinapojadiliwa na Bunge ili kupitisha Maazimio kuhusu matumizi ya fedha za umma. Kategoria zote mbili za ufafanuzi zinaweza kueleweka vizuri kwa kuweka mchakato huo katika hatua kubwa mbili. Hatua hizo ni usimamizi kabla ya matumizi *(Ex ante financial oversight)* na usimamizi baada ya matumizi *(post ante financial oversight)*. Hatua hizo zote zimepewa msingi kwenye Katiba, Sheria, Kanuni za Bunge na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge.

Hatua ya usimamizi wa kibunge wa fedha za umma kabla ya matumizi *(Ex-ante oversight)* ni utaratibu *(mechanism)* wa kupitia, kuchambua na kuchunguza mapendekezo ya uamuzi wa kibajeti, sera za kibajeti na makadirio ya matumizi kabla ya kuidhinishwa na kuanza kwa utekelezaji. Hatua hii inalenga kuhakikisha kwamba fedha za umma zinatumika kwa ufanisi, uwazi na kwa namna ambayo inaendana na vipaumbele vilivyozingatiwa na Bunge. Hatua hii inajumuisha Bunge kupitisha bajeti, kupitisha Muswada wa Sheria ya Fedha na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali.

> **Kanuni za Bunge zimeweka utaratibu na mchakato unaohusu kusimamia matumizi ya fedha za umma kabla ya kuanza kutumika. Usimamizi huo unaanza kwa Bunge kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mwongozo wa mapendekezo ya mpango na mwongozo wa kuandaa bajeti ya Serikali. Utaratibu huo umeelezwa katika kanuni ya 113 (3) (b) ya Kanuni za Bunge**

Bunge kuidhinisha bajeti ni sehemu ya usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kabla ya kufanyika kwa matumizi. Msingi wake unatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila Mwaka wa Bajeti. Madhumuni ya Jukumu hilo kwa mujibu wa Katiba ni kuwezesha utekelezaji wa madaraka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa muktadha huo usimamizi wa matumizi ya fedha za umma ni jukumu ndani ya madaraka ya Bunge.

Kanuni za Bunge zimeweka utaratibu na mchakato unaohusu kusimamia matumizi ya fedha za umma kabla ya kuanza kutumika. Usimamizi huo unaanza kwa Bunge kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mwongozo wa mapendekezo ya mpango na mwongozo wa kuandaa bajeti ya Serikali. Utaratibu huo umeelezwa katika kanuni ya 113 (3) (b) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa kanuni hiyo, kazi hiyo hufanyika wakati wa Mkutano wa Bunge wa Mwezi Oktoba – Novemba kila Mwaka.

> **kanuni ya 117 ya Kanuni za Bunge inafafanua namna Bunge linavyoshughulikia bajeti kwenye ngazi ya Kamati za Bunge. Ufafanuzi huo unaweka bayana namna Kamati za Bunge zinavyohusika katika kuona vipaumbele vya kibunge kiutungaji wa sheria** *(Legislative Priorities)*

Mantiki ya hatua hiyo ni kuwezesha upatikanaji wa vipaumbele vya kiutungaji sheria za fedha *(legislative priorities)*. Vipaumbele hivyo vinajenga msingi wa uamuzi wa kibunge kuhusu masuala ya kibajeti. Aidha, kwa namna hiyo Bunge linasimamia matumizi ya fedha za umma katika hatua za awali za uainishaji wa mahitaji ya matumizi ya fedha kwenye shughuli za umma.

Hatua ya pili ni uwasilishaji wa makadirio ya matumizi ya Serikali. Kanuni ya 116 ya Kanuni za Bunge inaweka utaratibu ambao unaliwezesha Bunge kutekeelza jukumu la usimamizi wa fedha za umma kabla ya matumizi yake *(ex-ante Financial Oversight).* Kanuni hiyo inaweka masharti kuhusu uwasilishaji wa mapendekezo ya Serikali ya kiwango cha ukomo wa bajeti ya Serikali.

Aidha, kanuni ya 117 ya Kanuni za Bunge inafafanua namna Bunge linavyoshughulikia bajeti kwenye ngazi ya Kamati za Bunge. Ufafanuzi huo unaweka bayana namna Kamati za Bunge zinavyohusika katika kuona vipaumbele vya kibunge kiutungaji wa sheria *(Legislative Priorities)*. Uhusika huo wa Kamati za Bunge ni sehemu ya usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma, hususani katika kusimamia vipaumbele vya matumizi.

Kwa utaratibu huo, kamati za kisekta hufanya usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kwa kulinganisha na matarajio ya kisera. Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, inazitaka kamati za kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Lengo lake ni udhibiti wa matumizi katika bajeti ya mwaka unaofuata.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Mheshimiwa **Halima Mdee** akizungumza wakati wa kikao cha kamati hiyo. Kulia ni Katibu wa Kamati hiyo Ndg **Amina Salum.**



Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge inazitaka kamati za kisekta kutumia siku zisizozidi tisa ili kuchambua taarifa za utekelezaji na makadirio ya matumizi ya Serikali kwa Mwaka unaofuata. Uchambuzi wa makadirio ni sehemu ya usimamizi wa fedha za umma kabla ya matumizi. Uchambuzi huo ni mchakato wa kusimamia upangaji wa matumizi ya fedha za umma kwa vipaumbele anuai kwa kila sekta na kwa sekta zote.

Hatua nyingine ni mjadiliano ya Bunge kuhusu makadirio ya matumizi ya Serikali. Kanuni ya 118 (1) ya Kanuni za Bunge imelitaka Bunge kutumia siku zisizozidi hamsini na nne ili kujadili makadirio ya matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kufanya hivyo, Bunge linasimamia matumizi ya fedha za umma katika hatua ya kuainisha vipaumbele vya matumizi ya fedha umma.

Kutilia nguvu madaraka hayo ya Bunge, kanuni ya 121 (1) ya Kanuni za Bunge inamruhusu Mbunge kutoa hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika makadirio ya matumizi ya Seikali. Sharti kubwa kwa ruhusa hiyo ni kuwa, mabadiliko yanayopendekezwa yasibadili madhumuni ya fungu *(vote)*.

Lengo la ruhusa hiyo ni kuzingatia dhima ya Bunge kusimamia vipaumbele vya Bunge kisheria *(legislative policies)* katika kupanga matumizi ya fedha za umma. Usimamizi huo chini ya kanuni ya 121 ya Kanuni za Bunge unajulikana kuwa usimamizi wa Kibunge wa matumizi ya fedha za umma kabla ya matumizi.

Katika mwendelezo wa kusimamia vipaumbele vya matumizi ya fedha za umma, Bunge likishajadili na kupitisha bajeti, linaendelea kusimamia nguvu za kisheria za matumizi yaliyoidhinishwa. Kufanikisha hilo, Bunge hupitisha miswada miwili ya Sheria inayoendana na Bajeti iliyoidhinishwa. Miswada hiyo ni Muswada wa Sheria ya Fedha (*Finance Bill*) na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya fedha za Serikali (*Appropriation Bill*)

Muswada wa Sheria ya Fedha ni nyenzo muhimu inayobainisha hatua za kisera za Serikali kuhusu mapato ya Serikali ambayo yanawezesha matumizi ya Fedha za Umma. Sheria hiyo katika usimamizi wa fedha za umma kabla ya matumizi inafanya kazi tatu.

Kwanza ni kuweka mipaka ya makusanyo ya fedha kwa ajili ya matumizi katika utekelezaji wa shughuli za umma. Bila kuweka masharti yanayopatikana katika Sheria ya Fedha za Serikali, matumizi ya fedha za umma yatakuwa makubwa na yatakabiliwa na hatari. Miongoni mwa hatari hizo ni kukosekana kwa uhakika kuhusu uhalali wa kuelekeza fedha iliyokusanywa kwenye baadhi ya vipaumbele.

Kwa mfano, Sheria ya Fedha inaweka masharti kuhusu ukusanyaji wa fedha kwa ajili ya mifuko maalumu kama vile mfuko wa barabara. Iwapo hakuna Sheria ya Fedha, makusanyo ya Fedha za mfuko wa barabara yatakosa mipaka na kwa ujumla wake matumizi ya fedha za umma hayatakuwa yamedhibitiwa kibunge hivyo, usimamizi utakuwa na changamoto.

Pili, ni hatari ya shughuli za umma kutopata kiasi cha fedha kitakiwacho wakati wa utekelezaji. Iwapo shughuli za umma zitapata fedha kidogo, matumizi yake hayatakidhi mahitaji na inaweza kusababisha kupotea kwa fedha. Kwa madhumuni ya kudhibiti hilo, Bunge linapitisha Sheria ya Fedha.

Tatu, bajeti inayopitishwa na Bunge inaweza kukosa utekelezaji wenye tija na ufanisi. Masharti ya Sheria ya Fedha yanaweka uhakika wa utekelezaji wa bajeti. Kwa kukosekana kwa masharti hayo, fedha iliyoidhinishwa na Bunge inaweza kuchelewa kupatikana. Kuchelewa huko kutasababisha matumizi ya fedha za umma yasiyoendana na makusudio ya Bunge. Kwa msingi huo, masharti ya Sheria ya Fedha yanaweka usimamizi kabla ya matumizi (*ex-ante financial oversight)*.

Muswada wa pili unahusu Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali (*Appropriation Act*). Sheria hii inaweka uhalali wa matumizi ya fedha za umma zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa kufanya hivyo, Sheria hii inaweka msingi wa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma yaliyoidhinishwa na Bunge. Msingi huu unatumika kudhibiti mipango ya matumizi ili isikinzane na idhini ya Bunge.

Kwa ujumla, usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma unaweza kuainishwa kwa hatua zake. Hatua hizo zinaweza kuwekwa katika kategoria mbili ambazo ni usimamizi wa kibunge kabla ya matumizi (Ex-ante financial oversight) na usimamizi baada ya matumizi (post-ante financial oversight). Katika toleo hili, safu hii imefafanua usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kabla ya matumizi.

Maelezo yamehusu hatua ya Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango. Lengo ni kushiriki katika uainishaji wa vipaumbele vinavyoweka msingi wa mgawanyo wa matumizi. Vilevile, uwasilishaji wa kiwango cha ukomo wa bajeti ya matumizi ya fedha za umma umefafanuliwa. Ufafanuzi huo umeonesha kuwa kiwango hicho kinazingatiwa kama kianzio cha kiasi cha fedha kinachoweza kupangwa kwa matumizi ya fedha za umma kwa mwaka unaofuata.

Kingine muhimu ni majadiliano ya makadirio ya matumizi baada ya kamati za kisekta kutoka ziara za ukaguzi wa miradi. Sanjari na hayo, maelezo kuhusu miswada miwili ya sheria yametolewa. Maelezo hayo yameonesha umuhimu wa sheria hizo katika usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma.

Katika toleo lijalo ufafanuzi utatolewa kuhusu usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma baada ya matumizi (ex-ante financial oversight). Umuhimu wa kufuatilia safu hii unatokana na busara za waswahili kwamba, 'FEDHA BILA NIDHAMU NI KAMA MAJI KWENYE TENGA, HUISHA BILA FAIDA. Kwa busara hiyo, kufuatilia safu hiyo kunawezesha kupata indhari inayozingatiwa na Bunge. KARIBU MSOMAJI KATIKA TOLEO LIJALO.

# Baraza la Wafanyakazi lakutana Zanzibar



Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge, Ndg. **Joshua Chamwela** akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi, kwa niaba ya Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Leonard

**Na Deonisius Simba**

**Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Bunge lilikutana na kufanya kikao kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali yatakayosaidia kuboresha utendaji kazi wa watumishi wa Ofisi ya Bunge.**

Kikao hicho cha siku mbili kilichofanyika Novemba 21 na 22, 2024 katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Tunguu Zanzibar kiliwashirikisha wajumbe mbalimbali wa Baraza hilo, Viongozi wa TUGHE, Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Ofisi ya Bunge.

Pamoja na mambo mengine, Baraza hilo lilijadili na kupitisha muhtasari wa maazimio ya kikao cha Baraza cha tarehe 17.

> **lengo la kikao hik ni kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Ofisi ya Bunge pamoja na kujadili na kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.**
>
> - *Ndg. Joshua Chamwela*

Akifungua kikao cha Baraza hilo, kwa niaba ya Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Leonard, Mkurugenzi wa Idara ya Shughuli za Bunge, Ndg. Joshua Chamwela, alisema lengo la kikao hicho ni kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Ofisi ya Bunge pamoja na kujadili na kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

"Tumekutana kwenye kikao hiki cha Baraza ili kupitia kwa pamoja changamoto zetu hasa suala la mafunzo kwa watumishi wetu, wapate mafunzo katika kiwango kinachohitajika katika kuboresha utoaji wa huduma zetu." alisema Ndg. Chamwela.

Alieleza kuwa uwepo wa Baraza la Wafanyakazi katika sehemu za kazi unasaidia kuongeza ushirikishwaji wa watumishi katika kupanga na kutekeleza majukumu yao, kuleta usawa katika kujadili mambo muhimu, kutoa ushauri juu ya tija na ufanisi wa kazi ikiwemo kukumbushana, kuelimishana na kuweka mazingira bora ya utendaji kazi na kuweka umoja kati ya wafanyakazi na viongozi.

"Ni matumaini yangu Baraza hili litakuwa na mijadala yenye uwazi na mambo yote yatakayojadiliwa yatasaidia kuimarisha utendaji wa majukumu ya Ofisi kwa lengo la kuhakikisha mazingira ya utendaji kazi yanaboreshwa kwa manufaa ya kutoa huduma bora, inajulikana kuwa Ofisi ya Bunge ina mambo mengi yanayogusa jamii moja kwa moja ikiwemo masuala ya utoaji wa elimu kwa umma kuhusu Bunge," alisema Chamwela.



Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Bunge, Viongozi wa TUGHE na Wakuu wa Idara na Vitengo vya Ofisi ya Bunge katika picha ya pamoja.

Aliongeza kuwa ni muhimu kwa kila mjumbe wa Baraza hilo kutumia nafasi aliyopewa ili uwakilishi wake uweze kuleta tija na kuwa chachu katika kuleta maendeleo ya watumishi wote kwa ujumla.

Pia alizungumzia ahadi ya Katibu wa Bunge ya kuweka mazingira bora kwa kila mtumishi ili kurahisisha ufanisi katika utendaji wa kazi pamoja na kutoa vitendea kazi vya kutosha.

"Matarajio ya Katibu wa Bunge ni kuona wafanyakazi wake wakiendelea kuchapa kazi kwa ushirikiano, nidhamu, upendo na weledi wa hali ya juu ili kutimiza lengo halisi la kiutumishi ndani ya muhimili huo." Alisema Ndg. Chamwela.

Kwa upande wake, Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Afya na Serikali Kuu Taifa (TUGHE), Ndg. Hery Mkunda, aliipongeza Ofisi ya Bunge kwa namna ambavyo wamekuwa wakitekeleza majukumu yao, sambamba na kuitisha kikao cha Baraza la Wafanyakazi kujadili masuala mbalimbali yanayohusu ofisi hiyo.

Alisema kuwa majadiliano ambayo yamekuwa yakifanyika katika Mkutano wa Baraza hilo yamekuwa yakisaidia kutatua changamoto zinazojitokeza sehemu ya kazi na pia kuboresha mazingira ya utendaji kazi.

Aliwahimiza wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi kuendelea kujituma, kufanya kazi kwa bidii ili kuifanya taasisi yao iendelee kukua.



Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Afya na Serikali Kuu tawi la Ofisi ya Bunge (TUGHE), Ndg. Chacha Nyakega alitoa rai kwa Watumishi wa Ofisi ya Bunge kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili waweze kuendana na dhana ya weledi na ubora.

"Natoa rai kwa Watumishi wenzangu wa Ofisi ya Bunge kuendelea kuchapa kazi kwa bidii ili tuendane na dhana ya weledi na ubora." alisema Ndg. Nyakega.

# Bunge Lawaaga Watumishi Tisa Waliostaafu




Spika wa Bunge Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson** na Katibu wa Bunge Ndg. **Baraka Leonard** wakiwapa mkono wa kwaheri Watumishi wa Ofisi ya Bunge waliostaafu Utumishi wa Umma katika halfa iliyofanyika Jijini Dodoma





**Na Debora Sanja**

**Bunge limewapatia zawadi maalumu watumishi wastaafu wa Ofisi ya Bunge kwa kutambua mchango wao katika utumishi wa Bunge.**

Watumishi hao walitangazwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na Benki ya Azania baada kumalizika kwa Bonanza la Bunge iliyofanyika katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma

Kabla ya kuwakabidhi zawadi hizo, Katibu wa Bunge alisema Bunge limeona ni vyema likatambua mchango wa watumishi hao waliolitumikia Bunge kwa kipindi kirefu.

"Niwapongeze washiriki wote wa Bunge Bonanza, tukio hili limenifanya nitambue mchango wa Watumishi tisa waliotumikia Bunge kwa uaminifu mkubwa hadi kuhitimisha utumishi wao.

"Ofisi ya Bunge imeona itumie fursa hii kuwakabidhi wenzetu kidogo tulichonacho ikiwa ni ishara ya upendo na kazi kuu waliyoifanya katika kutumikia Ofisi ya Bunge," alisema.

Waliopewa tuzo hizo ni Ndugu Mohamed Haji Mwanga aliyekuwa Mpambe wa Bunge, Ndugu Lawrence Makigi aliyekuwa Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Uendeshaji Idara ya Shughuli za za Bunge na Ndugu Nizar Ngwada aliyekuwa Afisa Hesabu Mwandamizi.

Wengine ni Ndugu Flora Yesaya aliyekuwa Afisa Hesabu Mkuu, Ndugu Rujina Mponzi aliyekuwa Mwandishi Mwendesha Ofisi, Ndugu Mbegea Malendemla aliyekuwa Msaidizi wa Afya Mkuu, Ndugu Novatus Kaboneka na Ndugu Almas Kitojo waliokuwa walinzi wakuu na Ndugu Mariam Ally Ichirima aliyekuwa Msaidizi wa Ofisi Mwandamizi

Akitoa salamu za shukrani kwa niaba ya watumishi wenzake, Ndugu Mohamed Mwanga aliishukuru Ofisi ya Bunge kwa heshima iliyowapatia ambayo haitasahaulika katika maisha yao.

"Shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Bunge na watumishi wote kwa ushirikiano wenu wakati wote wa utumishi wetu, tunaahidi kuwa tupo tayari kushirikiana na ninyi wakati wowote tutakapohitajika, tupo tayari," alisema.

# Hayati Dkt. Ndugulile alivyohudumu Bungeni

**Na: Abdallah Said Hancha**

**Utumishi wa umma ni miongoni mwa miito ya juu zaidi, inayohitaji kujitolea, uadilifu, na uwajibikaji kwa ajili ya maendeleo ya watu na Taifa kwa ujumla. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge mashuhuri wa Jimbo la Kigamboni, alidhihirisha maadili haya katika kipindi chote cha utumishi wake, akitumikia kwa ari na kujitolea kwa wapiga kura wake, jimbo lake na taifa la Tanzania.**

Tunaposimulia historia ya maisha yake, tunamuenzi kiongozi huyu ambaye maono yake, uthabiti na juhudi zake zilichangia kuboresha sera, maendeleo ya jimbo na hivyo kuacha athari ya kudumu kwa nchi yetu. Utumishi wake kama Mbunge utabaki kama somo na kumbukumbu za Bunge na katika mioyo ya wale aliowatumikia kwa bidii na huruma.

Makala haya ni uthibitisho wa mchango wake ambao ni ukumbusho kwa kiongozi wa kweli anavyopaswa kuwa hasa kwa kuzingatia mabadiliko chanya anayoleta katika jamii. Ingawa hayuko nasi tena, utendaji wake unahamasisha vizazi vijavyo kudumisha maadili ya kuhudumia watu, kuimarisha umoja na maendeleo ya jimbo na Taifa.



### Taarifa ya Kifo Chake

Tarehe 27 Novemba, 2024 Taifa la Tanzania liligubikwa na simanzi na majonzi mazito kufuatia taarifa ya kifo cha Mbunge wa Jimbo la Kigamboni ambaye pia aliwahi kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mhe. Dkt. Ndugulie pia amewahi kuwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Taarifa hiyo, ilitolewa na Mhe Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Tulia Ackson.

Akitoa taarifa hiyo kwa niaba ya Bunge, Mheshimiwa Tulia alisema "nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mbunge wa Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Kanda ya Afrika, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ngugulile. Kwa niaba ya Wabunge natoa pole kwa familia , wakazi wa Kigamboni na Watanzania wote. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi"

### Bunge lasimama kumuombea

Wakati taarifa ya kifo cha Mhe.Dkt Ndugulile ikitolewa, Bunge halikuwa katika vikao vyake kwani Wabunge walikuwa majimboni. Hivyo, Bunge lilipoitishwa ili kuanza vikao vyake siku ya Jumanne tarehe 28 Januari, 2025 Waheshimiwa Wabunge wakiongozwa na Spika wa Bunge walipata nafasi ya kutoa heshima kwa aliyekuwa mbunge mwenzao kwa kusimama kumuombea kabla ya shughuli mbalimbali za Bunge kuanza.

### Kuingia Bungeni

Mheshimiwa Ndugulile, alichaguliwa kuwa Mbunge kupitia jimbo la Kigamboni mwaka 2010. Bunge hili (2010 – 2015) lilikuwa ni Bunge la kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililoitishwa tarehe 12 Novemba, 2010 kufuatia tangazo la Serikali Na. 805A la tarehe 08 Novemba, 2010 lililotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kipindi hicho, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Bunge la Kumi lilikuwa na jumla ya Wabunge 357 kikatiba likiongozwa na Spika wa kipindi hicho Mheshimiwa Anne Semamba Makinda akiwa ndiye Spika wa kwanza mwanamke katika historia ya Bunge la Tanzania.

Akihudumu katika Bunge hili, Ndugulile alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuanzia mwaka 2010 hadi 2013 na Kuanzia mwaka 2013 hadi 2015 akawa Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya.

### Makamu Mwenyekiti Kamati ya Ushauri (IPU)

Akiendelea kuhudumu katika Bunge la Kumi, Mheshimiwa Dkt. Ndulile alipata nafasi ya kuwa mmoja wa Wabunge waliokuwa wakiliwakilisha Bunge letu katika mikutano ya Umoja wa Mabunge ya Dunia (IPU). Kushiriki kwake IPU kunatokana na kuwa katika nafasi ya Ubunge wa Tanzania kulikomwezesha kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Masuala ya Afya ya kina mama, watoto katika Umoja huo Kuanzia mwaka 2010 hadi 2013. Aidha, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo mwaka 2015 hadi 2017.

Bunge hili lilivunjwa tarehe 07 Agosti, 2015 kwa Tangazo la Serikali Na. 323A la tarehe 07 Agosti, 2015 kupisha uchaguzi mkuu.

### Awa Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Mhe. Ndugulile aligombea tena Ubunge kupitia jimbo la Kigamboni na kushinda kwa mara nyingine kiti cha ubunge na hivyo kurejea Bungeni mwaka 2015 kuhudumu katika Bunge la Kumi na Moja (2015 – 2020) lililoitishwa tarehe 17 Novemba, 2015 kufuatia tangazo la Serikali Na. 513 la tarehe 06 Novemba, 2015 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Bunge la Kumi na Moja lilikuwa na jumla ya Wabunge 393 kikatiba. Bunge hili liliongozwa na Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni alikuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Katibu wa Bunge alikuwa Dkt. Thomas Didimu Kashililah hadi mwaka 2017 alipoteuliwa Ndg. Stephen Nzohabonayo Kagaigai.

Akihudumu katika Bunge hili la Kumi na Moja, Mheshimiwa Ndugulile alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya; kuanzia mwaka 2015 hadi 2017. Aidha, alichaguliwa na Bunge mwaka 2015 kuwa mmoja wa Wabunge wawakilishi wa Bunge la Tanzania katika Bunge la Afrika (Pan African Parliament). Vilevile alikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri wa Masuala ya Afya ya Akina Mama, Watoto na UKIMWI katika Umoja wa Mabunge Duniani (IPU)

### Kuwa Naibu Waziri

Akiwa katika nafasi hii ya Uenyekiti, Mhe. Ndugulile aliteuliwa na Rais Magufuli kuwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Nafasi hii ya Naibu Waziri aliitumikia Kuanzia mwezi Oktoba, 2017 hadi Mei 2020 na kurejea tena Bungeni kuhudumu kama Mbunge wa kawaida hadi Bunge la Kumi na Moja lilipovunjwa tarehe 31 Julai, 2020 kwa Tangazo la Serikali Na. 532 la tarehe 13 Julai, 2020 Kupisha uchaguzi mkuu.

Uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 Mhe Ndugulile akagombea tena ubunge kupitia jimbo la Kigamboni na kushinda kwa mara ya tatu mfululizo. Kushinda kwake kukamuwezesha kurudi tena Bungeni kuhudumu katika Bunge la Kumi na Mbili (2020 – 2025) ambalo liliitishwa tarehe 10 Novemba, 2020 kufuatia tangazo la Serikali Na. 942A la tarehe 05 Novemba. 2020 na Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli. Bunge hili liliongozwa na Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai hadi tarehe 06 Januari, 2022 alipojiuzulu na kuchaguliwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson tarehe 04 Februari, 2022. Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni aliendelea kuwa Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa. Katibu wa Bunge alikuwa Ndg. Stephen Nzohabonayo Kagaigai hadi tarehe 15 Mei, 2021 alipoteuliwa Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, ndc akiwa ndiye Katibu wa kwanza mwanamke katika historia ya Bunge la Tanzania.

Akihudumu katika Bunge hili la Kumi na Mbili, Mhe. Ndugulile aliteuliwa na Rais wa awamu ya tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Naibu Waziri wa Afya. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani tarehe 19 Machi, 2021 kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021, Mheshimiwa Ndugulile aliteuliwa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Alihudumu katika nafasi hiyo ya Waziri hadi Septemba 2021 na kurejea tena Bungeni kuhudumu akiwa katika nafasi yake ya Ubunge.

### Makamu Mwenyekiti na Mjumbe wa *IPU*

Baada ya kurejea Bungeni na kuhudumu kwa nafasi ya mbunge wa kawaida akishiriki vikao mbalimbali vya Kamati yake aliyopangiwa na Spika wa Bunge kuwa mjumbe hadi alipochaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ambayo kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2003 inajukumu la kusimamia Wizara ya Afya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini. Aidha, katika kipindi hiki alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Masuala ya Afya ya Akina Mama, Watoto na masuala ya UKIMWI katika Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Nafasi hizi alizihudumu hadi mauti yalipomfika

### Mwanachama wa Vyama vya Hiari vya Kibunge

Kama ilivyo kwa mabunge mengine duniani, Bunge la Tanzania limeruhusu vyama vya hiari vya kibunge kufanya shughuli zao ambapo wabunge wa vyama mbalimbali huungana kujadili na kulisemea jambo ambalo hudhani lina manufaa kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Hivyo wanachama huwa na katiba zao zinazowaongoza katika kutekeleza majukumu au ajenda zao. Kwa sasa Bunge la Tanzania lina jumla ya vikundi hivi kumi na viwili. Mheshimiwa Ndugulile hakujitenga bali alikuwa ni mwanachama wa baadhi wa vikundi hivi hususan Umoja wa Wabunge wa Tanzania Kupambana na Janga la UKIMWI (TAPAC) ambapo aliwahi kuwa Makamu Mwenyekiti chini ya uongozi wa Mbunge mwanaharakati wa wakati huo Mheshimiwa. Lediana Mng'ong'o. Aidha, alikuwa ni mwanachama wa Kikundi cha Wabunge kinachohusu masuala ya Lishe maarufu kama "Vinara wa Lishe".

### Kazi nyinginezo alizowahi kufanya

Ndugulile aliyekuwa na taaluma mbalimbali za utabibu na afya ya jamii kabla ya pia kuamua kuwa mwanasiasa alifanya kazi mbalimbali kabla ya kuwa Mbunge. Alianza kama daktari wa afya ya jamii na akapanda hadi nafasi za uongozi, ikiwa ni pamoja na kuwa Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Uchunguzi nchini Tanzania. Pia aliwahi kuwa Meneja wa Mpango wa Damu Salama, ambapo aliongoza mipango ya kitaifa ya kuboresha ubora na upatikanaji wa huduma hizo.

Katika duru za kimataifa, alifanya kazi kama Mshauri Mkazi nchini Afrika Kusini, katika Kituo cha Kupambana na Kuzuia Magonjwa nchini Afrika ya Kusini.  Aidha, Oktoba 27, 2024 Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aligombea na kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, baada ya kupigiwa kura na nchi Wanachama wa Afrika wakati wa kikao cha Sabini na Nne cha Kamati ya Kanda ya Afrika ya Shrika la Afya Duniani (WHO), kilichofanyika Brazzaville, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Wagombea wengine walikuwa Dkt. Boureima Hama Sambo (aliyependekezwa na Niger,) Dkt. Ibrahima Socé Fall (aliyependekezwa na Senegal) na Dkt. Richard Mihigo (aliyependekezwa na Rwanda).

Katika salamu zake za shukrani na kukubali majukumu yake mapya, Dkt. Ndugulile alieleza dhamira ya kusimamia afya za wananchi wa Kanda ya Afrika kwa kusema "Nimeheshimiwa sana na kuaminiwa kuchaguliwa katika nafasi ya Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani, Kanda ya Afrika. Nashukuru Nchi Wanachama kwa imani iliyoonyeshwa kwangu. Naahidi kushirikiana nanyi na ninaamini kwa pamoja tunaweza kujenga Afrika yenye afya njema," alisema Dkt. Ndugulile.

Kabla ya kukutwa na mauti, Dkt. Ndugulile alikuwa anatarajiwa kuanza rasmi jukumu lake katika Shirika la Afya la Dunia Februari, 2025.

### Historia Fupi ya Mheshimiwa Ndugulile

Marehemu Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile alizaliwa tarehe 31 Machi, 1969 katika Wilaya ya Mbulu Mkoa wa Manyara. Yeye ni mtoto wa kwanza kati ya watoto wa Marehemu Gabriel Sengo Ndugulile na mkewe Bi Martha Wingia Kimaro. Ndugu zake wengine ni Dennis, Lillian, Godwin, Frank, na Wilbert.

### Elimu

Marehemu alihitimu elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Ufukoni Jijini Dar es Salaam mwaka 1982 kabla ya kjiunga na elimu ya sekondari katika Shule ya Sekondari ya Prince Edward nchini Zimbabwe na kuhitimu mwaka 1987.  Alijiunga na elimu ya sekondari ya juu katika Shule ya Sekondari Tambaza Jijini Dar es Salaam na kuhitimu mwaka 1989.

Mwaka 1997, Marehemu alihitimu na kutunukiwa Shahada ya Kwanza ya Udaktari (Degree of Doctor of Medicine) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mwaka 2001  Marehemu alihitimu na kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Udaktari (Degree of Master of Medicine) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mwaka 2010 - Marehemu alihitimu na kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Afya ya Jamii Masters of Medicine Chuo Kikuu cha Western Cape nchini Afrika Kusini na mwaka 2022  Marehemu alijiendeleza kitaaluma na kufanikiwa kuhitimu Shahada ya Kwanza ya Sheria katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Marehemu alijiendeleza kitaaluma katika fani mbalimbali na kutunukiwa tuzo anuai ikiwa ni pamoja na Cheti cha Uongozi katika Ubunifu wa Masuala Afya Barani Afrika (Enhancing Leadership Innovation for Africa's Health Sector Program) nchini Afrika Kusini.

### Familia

Mheshimiwa Ndugulile alifunga ndoa na Bi Magdalena Lyimo tarehe 11 Septemba, 1999 Jijini Dar es Salaam katika Kanisa la Immaculate lililopo Upanda. Yeye na mkewe walijaaliwa kupata watoto wawili ambao ni Martha na Melvin.

### Maziko

Baada ya kufafariki Novemba 27, 2024 nchini India alipokuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Apolo, mwili wa Marehemu Ndugulile ulisafirishwa kuja Tanzania tarehe 29 Novemba, 2024. Misa ya kwanza ya kumombea marehemu ilifanyika tarehe 02 Desemba, 2025 katika Kanisa la Immaculate na baadaye katika viwanja vya Karimjee ambako pia Waheshimiwa Wabunge na Wageni mbalimbali wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa heshima zao za mwisho kwa marehemu. Tarehe 03 Desemba, 2024  mwili wa marehemu ulielekea Kanisa la Bikira Maria Consolata, lililopo Kigamboni kwa ajili ya misa ya kumuombea marehemu kabla ya kwenda Viwanja vya Machava kwa ajili ya wananchi kutoa heshima zao za mwisho. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile alizikwa katika makaburi ya Mwongozo yaliyopo Kigamboni  tarehe 03 Desemba, 2024.

**Dkt Faustine Ndugulile**

1. Hakika ametupanga, Mola duniani humu,
Roho zetu kazilenga, kuelekea kuzimu,
Hakuna ataepinga, aendelee kudumu,
Sisi wote tutazimu, tutazimu sisi wote.

2. Ndugulile maishani, msafawe umetimu,
Ameitwa na Manani, sasa kawa marehemu,
Amekiri bila kani, msafara ni muhimu,
Sisi wote tutazimu, tutazimu sisi wote.

3. Beti tatu kaditama, naweka chini kalamu,
Tuache kushika tama, tumuombee Rahimu,
Kilio tulie vyema, na huku tukijihimu
Sisi wote tutazimu, tutazimu sisi wote.



# **Pius Msekwa:** Hazina ya Bunge, Hazina ya Taifa!

- **Kutoka Karani hadi Spika wa Bunge**

**Na Patson A.Sobha**

**Bunge la Tanzania linajivunia mambo mengi ya mafanikio tangu enzi za kupata uhuru, lakini jambo moja la kipekee sana ni kuwahi kuwa na uongozi wa Mheshimiwa Mzee Pius Chipanda Msekwa ambaye ni hazina ya aina yake kwa Bunge na Taifa kwa ujumla.**

Mzee Msekwa akiwa mmoja wa wanasiasa waliolelewa kwa karibu na Mwalimu Julius Nyerere, amewahi kushika nyadhifa mbalimbali zikiwemo za kibunge, kiserikali na katika ngazi ya chama cha siasa akianzia enzi za TANU na hatimaye Chama cha Mapinduzi.

Ukienda kwa wanasiasa na hasa ndani ya CCM, Mheshimiwa. Msekwa ni hazina ya maarifa ya siasa na uongozi, kwa Serikali ni tunu ya utawala na utumishi wa umma akiwa ametumikia nafasi lukuki katika vyombo vya masuala ya sheria, Mkuu wa Mkoa, Mwenyekiti na Mjumbe wa Tume na Bodi Mbalimbali.

Kwa upande wa Bunge, Mzee Msekwa alikuwa Katibu wa Bunge wa kwanza, Mbunge, Naibu Spika, Spika wa Bunge na kiongozi mahiri aliyeleta mabadiliko chanya katika historia ya Bunge ikiwemo kubuni Joho la Spika na kujenga jengo la Bunge.

Ukimtaja Mzee Msekwa kwa wanataaluma wanamfahamu kama Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam mwaka 1970 – 1977, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, na mwandishi mahiri wa vitabu.

Mzee Msekwa, ukimuuliza wakati wowote swali lolote kuhusu Bunge, liwe la kihistoria ama la utalaamu wa mambo ya Bunge, hukosi kupata majibu ya kina kutoka kwa nguli huyu wa masuala ya kibunge Tanzania.

Mara zote anapojibu au kueleza, utatamani kumsikiliza kwa namna anavyotiririsha majibu murua yanayodhihirisha siyo tu ubobevu, umahiri na uzoefu wake wa zaidi ya miaka 45 katika shughuli za Bunge, bali pia shauku yake ya kutaka kuelimisha wengine.

Umahiri wa Mzee Pius Chipanda Msekwa, haukuanzia kwenye masuala ya Bunge, bali historia inaweka dhahiri kwamba akiwa mwanafunzi shuleni na chuoni, alikuwa na juhudi na weledi mkubwa katika masomo yake.

Mzee Msekwa, hakuishia kuwa mahiri kwenye masomo yake tu, bali aliendelea kushamiri hata katika kazi na hatimaye uongozi wa ngazi mbalimbali alizowahi kutumikia na hata anazotumikia hadi sasa.

> **Tunaweza kusema kuwa bila shaka umahiri wake pia ndio ulimwezesha kuteuliwa akiwa na kijana wa umri wa miaka 25 kuwa Katibu wa Bunge wa kwanza Mtanganyika aliyechukua nafasi hiyo kutoka kwa Mwingereza Bw. Geofrey William Young Hucks.**

### Kuzaliwa na safari yake ya elimu

Katika kitabu chake, "Uongozi na Utawala wa Mwalimu Julius Nyerere: Miaka 25 ya Utumishi wa Umma Chini ya Uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere", inaelezwa kuwa Mzee Pius Msekwa alizaliwa katika kijiji cha Bugombe wilayani Ukerewe tarehe 9 Juni, 1935.

Safari ya maisha ya kielimu ya Mzee Msekwa ilianzia wakati wa hali ngumu ya maisha katika kila sekta hasa huduma za kijamii kama elimu, afya na usafiri. Hata hivyo alibahatika kusoma chekechea na elimu ya msingi katika shule ya Kanisa Katoliki Kagunguli, Ukerewe.

"Wakati huo hali ya maisha ikiwa imegubika sekta za kijamii kama elimu, afya, na usafiri, "Mimi nilibahatika kusoma elimu ya chekechea na msingi katika shule ya Kanisa Katoliki hadi darasa la nne." Alisema Msekwa katika mahojiano na Maafisa Habari wa Bunge.

Mheshimiwa Msekwa, aliongeza kwamba baada ya darasa la nne, akaenda kusoma darasa la tano hadi la kumi Nyegezi Mwanza, ambapo alifaulu mtihani na kisha kujiunga na Chuo cha Mtakatifu Francis ambacho kwa sasa ni Shule ya Sekondari ya Pugu, iliyopo jijini Dar es salaam.

Mzee Msekwa anakumbuka hali ngumu ya usafiri wa kutumia mitumbwi kutoka na kurudi Kisiwa cha Ukerewe wakati anasoma Nyegezi, Mwanza. "Ilikuwa hali ngumu sana, tukifika lazima tuandike barua ya kuwajulisha nyumbani kwamba tumefika salama, maana safari ya majini haikuwa ya uhakika," alisema.

Baba yake alifariki wakati Pius Msekwa akiwa anasoma darasa la tano, hata hivyo, alipata udhamini wa mfanyabiashara mwenye asili ya Bara la Asia hadi hapo alipomaliza masomo ya miaka miwili katika chuo hicho.

Jitihada za Msekwa kuanzia ngazi za chini za elimu hadi chuo kikuu, zilidhihirisha uwezo wake na kumpa mafanikio ya kimasomo hata kufikia kuwa mahiri sana katika lugha ya Kiingereza.

Miongoni mwa mafaniko yake akiwa sekondari ni pamoja na kupata tuzo ya tabia njema na bidii katika masomo. Aidha, ufaulu wake wa darasa la 12 ulikuwa wa kiwango cha daraja la kwanza katika mtihani wa Cambridge School Certificate na hivyo kupata fursa ya kuchaguliwa kujiunga na Chuo Kikuu cha Makerere.

Akiwa chuoni Makerere, aliendelea kudhihirisha uwezo wake kimasomo siyo tu kumudu somo la lugha ya kiingereza, bali aliweza kushinda pia zawadi ya fedha baada ya kufanikiwa kuwa mshindi wa shindano la uandishi wa insha katika somo la uchumi.

Mzee Msekwa alisoma Shahada yake ya Kwanza Katika Somo la Historia Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda na kuhitimu mwaka 1960 kisha alirudi nchini Tanzania ambapo akaajiriwa kama Katibu wa Bunge Msaidizi aliye katika mafunzo kabla ya kuteuliwa rasmi kushika nafasi hiyo mwaka 1962 nafasi aliyoitumikia hadi mwaka 1970.

Weledi wa Mzee Msekwa, ulijikita zaidi katika historia, sayansi ya siasa, uongozi wa umma na sheria ya katiba na utawala. Alipata Shahada yake ya Umahiri katika Sayansi ya Siasa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es salaam wakati akiwa kiongozi wa chuo hicho.

### Safari ya Uongozi

Wahenga walisema nyota njema huonekana asubuhi, pengine ndiyo maana uzoefu w a MzeeMsekwa katika uongozi ulianza mapema alipokuwa anasoma Chuo Kikuu cha Makerere ambako alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wanafunzi wa chuo hicho.

Tunaweza kusema kuwa bila shaka umahiri wake pia ndio ulimwezesha kuteuliwa akiwa nI kijana wa umri wa miaka 25 kuwa Katibu wa Bunge wa kwanza Mtanganyika aliyechukua nafasi hiyo kutoka kwa Mwingereza Bw. Geofrey William Young Hucks.

Katika utumishi wa umma, Mzee Msekwa ametumikia nyadhifa mbalimbali ikiwemo kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam kuanzia mwaka 1970 hadi 1977 ambapo pia alikuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mitihani Tanzania.



Mzee Msekwa alitumikia katika nafasi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora na Kilimanjaro kati ya mwaka 1981 – 1984. Aidha, aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka 1984 – 1989 na baadaye kuwa Mjumbe wa Tume ya Rais ya Mipango mwaka 1989 – 1990.

Katika sekta ya sheria Mzee Msekwa amewahi kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mapitio ya Mfumo wa Mahakama (Tume ya Msekwa) mwaka 1975 – 1977, Mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Sheria za Tanzania (1983 - 2007), na Mjumbe wa Kikosi Kazi cha Mabadiliko ya Sekta ya Sheria (1993 - 1994).

Halikadhalika, Mzee Msekwa amewahi kuwa Mwenyekiti wa bodi mbalimbali zikiwemo: Bodi ya Chuo cha Ushirika Moshi (1984 – 2005), Bodi ya Uongozi wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka (1984 – 2000), na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (1985 – 2000).

Kwa upande wa nyanja za kisiasa, Mzee Msekwa alitumikia nyadhifa za juu katika ngazi ya Katibu Mkuu Mtendaji wa TANU mwaka 1967 – 1970, na baada ya kuzaliwa Chama cha Mapinduzi, akawa Katibu Mkuu Mtendaji wake mwaka 1977 – 1980, na hatimaye akaja kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa mwaka 2007 – 2012.

Mwaka 1990 Mzee Msekwa aligombea ubunge kupitia jimbo la Ukerewe, nafasi ambayo ilimwezesha kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge, akiwa chini ya uongozi wa Spika Chifu Adam Sapi Mkwawa.

Mwezi Aprili, 1994, Mhe. Chifu Adam Sapi Mkwawa, akiwa Spika wa Bunge kwa miaka 30 aliamua kujiuzuru kwa hiari, na kupisha uchaguzi, ambapo Wabunge walimchagua Mzee Pius Msekwa kuwa Spika wa Bunge, nafasi aliyotumikia hadi mwaka 2005.

> **Katika kitabu chake cha "Uongozi na Utawala wa Mwalimu Julius Nyerere", Mzee Msekwa anaweka bayana moja kati ya hazina kubwa alizotoa kwa taifa lake kuwa ni kuwasaidia wengine katika masomo.**

### Mwandishi wa Vitabu

Tusemapo Mzee Msekwa ni hazina, hatuangalii tu utumishi wake uliotukuka, bali tunazingatia kwamba amekuwa mstari wa mbele katika kuhamishia weledi, ujuzi, uzoefu, hekima na busara zake katika maandishi kwa kuandika vitabu mbalimbali kwa ajili ya kizazi hiki na kijacho.

Miongoni mwa vitabu alivyoandika ni pamoja na: Towards Party Supremacy (1977), Education Policy Formation Before and After the Arusha Declaration (1979), Parliament Privilege in Tanzania (2003), Insha za ufafanuzi wa baadhi ya masuala ya chama (1982), Essays on The Transition to Multi-partism in Tanzania (1995), na 50 Years of Independence: Reflections on Tanzania's Multi-Party Parliament (2000).

Vitabu vingine ni pamoja na: A Concise Political History of Tanzania alichoandika mwaka 2011, Uongozi na Utawala wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere cha mwaka 2012, The Story of Tanzania Parliament, cha mwaka 2013, na Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, alichoandika mwaka 2019.

Katika kitabu chake cha "Uongozi na Utawala wa Mwalimu Julius Nyerere", Mzee Msekwa anaweka bayana moja kati ya hazina kubwa alizotoa kwa taifa lake kuwa ni kuwasaidia wengine katika masomo.

Msekwa, anaongeza kusema kuwa alitoa fadhila zaidi kwa jamii alipokuwa Spika wa Bunge pale alipoamua kujenga shule ya sekondari katika kijiji alichozaliwa cha Bugombe, Kisiwani Ukerewe na baadaye kuikabidhi kwa Serikali.

Shule hiyo inayojulikana kama Shule ya Sekondari ya Pius Msekwa, aliijenga kama njia ya kuwasaidia wengine akikumbuka wema aliotendewa na mfanyabiashara mwenye asili ya Asia aliyemfadhili masomo yake.

"Niliguswa sana na wema huo, niliendelea kukumbuka na kuenzi kitendo chake hicho wakati wote.... Kwa ajili hiyo baadaye sana katika maisha yangu nilipokuwa nimepata uwezo wa kufanya hivyo, nilihamasika kuwatendea watu wengine wema kama huo," anasema Mzee Msekwa katika kitabu chake.

Tafadhali usikose kuungana nami katika toleo lijalo kwa ajili ya mwendelezo wa makala hii.

# KONA YA MALENGA

## Waheshimiwa Wajumbe Wa Tume Ya Bunge

1. Jadidi ninajihimu, jambo kuja waambia,
   Tume ya Bunge muhimu, wajumbe nawatajia,
   Muweze kuwafahamu, pia kuwazingatia,
   Wajumbe nawatajia, wa Tume muwafahamu.

2. Naanza na Mwenyekiti, Spika wetu Tulia,
   Mussa Zungu madhubuti, naye yu-mumo sawia,
   Huipanga mikakati, mambo kuyapangilia,
   Wajumbe nawatajia, wa Tume muwafahamu.

3. Na Lukuvi muadhama, ni mjumbe maridhia,
   Kwenye tume hujituma, tena bila kusinzia,
   Hakuna kinachokwama, malengo huyafikia,
   Wajumbe nawatajia, wa Tume muwafahamu.

4. Yupo Rashid Shangazi, naye Janejelly pia,
   Zahoro mwenye maozi, kadhalika Fakharia,
   Hao ni wachapa kazi, kwenye tume huingia,
   Wajumbe nawatajia, wa Tume muwafahamu.

5. Aeshi wa Khalfani, tume aitumikia,
   Halima Mdee ndani, wapo kwenye mizania,
   Hujadili kwa makini, wakiwa na njema nia,
   Wajumbe nawatajia, wa Tume muwafahamu.

6. Na yupo Khalifa Issa, mweledi alotimia,
   Aliyejaa hamasa, kazi huifurahia,
   Tume ina watu hasa, kwa kweli twajivunia,
   Wajumbe nawatajia, wa Tume muwafahamu.

7. Ndugu Baraka Katibu, makofi twampigia,
   Kazi zote huratibu, kwa mujibu wa sheria,
   Hutekeleza wajibu, kwa asilimia mia.
   Wajumbe nawatajia, wa Tume muwafahamu.

8. Tume ya Bunge ni hiyo, niliyo watangazia,
   Majina yao ni hayo, niliyowaandikia,
   Twawasifu wana moyo, wanatuonesha njia,
   Wajumbe nawatajia, wa Tume muwafahamu.

**Jadidi**
**Abdallah S. Hancha - 0713 291139**

# Ushiriki wa Bunge la Tanzania Michezo ya EAC



**Na. Debora Sanja**

**Timu za Bunge la Tanzania zilishiriki Mashindano ya Michezo ya Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuibuka washindi wa medali na makombe katika michezo mbalimbali.**

Mashindano hayo yaliyofanyika Desemba 6-17.2024 Jijini Mombasa nchini Kenya ambapo nchi nyingine zilizoshiriki ni wenyeji Bunge la Kenya, Burundi, Rwanda na Uganda.

Tuzo hizo zilitolewa katika hafla maalumu iliyoandaliwa na mwenyeji wa mashindano hayo ambaye ni Bunge la Kenya.

Katika matokeo ya jumla, Timu ya Bunge la Tanzania ya mpira wa wavu wanawake iliibuka mshindi wa kwanza na kujinyakulia Kombe na medali za dhahabu.

Timu ya mpira wa miguu, timu ya kamba wanaume na wanawake, timu ya mpira wa pete na timu ya mpira wa wavu wanawake zimeibuka mshindi wa pili na kupata medali za fedha.

Kwa upande wa mchezo wa riadha Mheshimiwa Anatropia Theonest aliitoa kimasomaso Timu ya Bunge la Tanzania kwa kupata medali tatu za dhahabu kwa kushinda nafasi ya kwanza katika mbio za meta 1500,800 na 400

Katika mchezo wa vishale, Timu ya Bunge imeibuka mshindi wa pili kwa kupata medali ya fedha

> Mashindano yalizinduliwa na **Rais wa Kenya, Mheshimiwa William Ruto** **ambapo pamoja na mambo mengine alihimiza umuhimu wa Utengamano wa Afrika Mashariki katika kuchochea maendeleo ya nchi wanachama na kutoa wito michezo hiyo kuendelea kudumisha umoja na mshikamano.**

Wakati huo huo katika mchezo huo, Mheshimiwa Yahya Mhata alishinda nafasi ya kwanza kwa upande wa wanaume na Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis akishika nafasi ya kwanza kwa wanawake ambapo wote walipata medali za dhahabu na makombe.

Katika mchezo wa gofu, Timu ya Bunge ya wanawake ilishika nafasi ya pili na kujinyakulia medali ya fedha huku Timu ya Wanaume ikishika nafasi ya tatu.

Awali mashindano hayo yalizinduliwa na Rais wa Kenya, Mheshimiwa William Ruto ambapo pamoja na mambo




Rais wa Kenya, Mheshimiwa **Dkt. William Ruto** akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mashindano ya Michezo ya Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Hafla iliyofanyika Jijini Mombasa, Kenya

mengine alihimiza umuhimu wa utengamano wa Afrika Mashariki katika kuchochea maendeleo ya nchi wanachama na kutoa wito michezo hiyo kuendelea kudumisha umoja na mshikamano.

Alisema michezo hiyo inatoa fursa ya kuimarisha moyo wa mshikamano na kuimarisha uhusiano wa kirafiki kama majirani na nchi washirika.

Aidha, alisema Jumuiya ya Afrika Mashariki inafanya kuoanisha sera, kupanua mitandao ya miundombinu na kuimarisha biashara ya mipakani ili kudumisha ushirikiano wa kikanda.

Alisema juhudi hizo zinasaidia kujenga Afrika Mashariki yenye ushindani na shirikishi zaidi na kufanya Jumuiya kuwa na maendeleo makubwa zaidi barani Afrika.

"Muungano wa Afrika utaongozwa na mtangamano wa Afrika Mashariki, ikiwa Mikataba ya Makubaliano wa Eneo Huru la Biashara Bara la Afrika utafanikiwa basi Injini yake itakuwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema.

Mheshimiwa Ruto alitumia nafasi hiyo kutoa pole kwa Bunge la Tanzania kwa ajali ya basi iliyowahusisha Waheshimiwa Wabunge wakati wakielekea Mombasa nchini Kenya kwa ajili ya kushiriki mashindano hayo.

"Napenda nichukue fursa hii kutoa pole kwa marafiki zetu wa Tanzania kwa ajali iliyotokea, tunawatakia heri wote walioapata maumivu na majeraha na tunamuomba Mungu awape afueni," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bunge Sport Club, Mheshimiwa Abbas Tarimba alisema licha ya baadhi wa wachezaji wa Timu ya Bunge kujeruhiwa katika ajali ya gari wapo tayari kushindana kikamilifu.

"Pamoja na ajali ambayo wenzetu 17 wamepata majeraha Tanzania tumeamua kuja kushindana, tumejiandaa na tutaonesha ushindani," alisema.

Katika mechi ya ufunguzi wa mashindano hayo, Timu ya Bunge la Kenya ya mpira wa miguu ilikutana na Timu ya Bunge la Afrika Mashariki kwenye uwanja wa Mbaraki mjini Mombasa.



Timu ya Bunge la Tanzania ya Wanawake yakuvuta Kamba ikishiriki katika Mashindano ya Michezo ya Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yayofanyika Jijini Mombasa, Kenya



# Mashabiki wa Simba Waibuka Kidedea Bunge Bonanza

**Na Debora Sanja**

**Mashabiki wa Timu ya Simba (Wekundu wa Msimbazi), wameibuka mshindi wa jumla katika Bonanza la Bunge lililofanyika tarehe 1 Februari, 2025 katika Viwanja vya Shule ya Sekondari John Merlin Jijini Dodoma.**

Bonanza hilo ambalo lilidhaminiwa na Benki ya Azania lilihusisha mashabiki wa Timu ya Simba na Yanga kutoka Ofisi ya Bunge (Waheshimiwa Wabunge na watumishi), watumishi kutoka Hospitali ya Benjamini Mkapa, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (DUWASA) na Wizara ya Maji.

Taasisi nyingine ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma (PSSSF), Chuo cha Mipango Dodoma, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na mashabiki wa Timu za Simba na Yanga wa Mkoa wa Dodoma na viongozi wao.

Akitangaza mshindi katika hafla ya chakula cha jioni, Spika wa Bunge Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson alisema katika Bonanza hilo Simba imeibuka mshindi wa jumla kwa kujinyakulia pointi 90 huku Yanga ikiambulia pointi 81.

Baadhi ya michezo ambayo timu za mashabiki wa Simba (mchanganyiko) iliongoza ni pamoja mchezo wa mpira wa miguu, mchezo wa mpira kikapu wanawake, mchezo wa mpira wa wavu wanaume, mchezo wa mpira wa pete wanawake na kuvuta kamba wanawake na wanaume.

Michezo mingine iliyoongoza ni mchezo wa mpira wa meza wanawake na wanaume, mchezo wa *'draft'* wanawake, mchezo wa kurusha vishale wanaume, mchezo wa *'pool table'*wanawake na wanaume na mchezo wa karata wanawake.

Mheshimiwa Spika aliishukuru Benki ya Azania kwa ushirikiano wao na kwa kudhamini Bunge Bonanza kwa ukubwa wa hali ya juu.

“Azania Benki mmetufanya tufurahi, tumefahamiana na watu mbalimbali shukrani kwa kututengenezea fursa hii.

“Nawapongeza pia kwa kazi kubwa kuchangia maendeleo ya nchi, Bunge tunatambua mchango wenu na tunawatakia kila la kheri katika mwaka unaoanza,” alisema.

Aidha, aliwashukukru Waheshimiwa Wabunge, watumishi na washiriki wengine wote kwa ushirikiano walituonesha katika Bonanza hilo.

Awali akizungumza katika Viwanja vya John Merlin kabla ya kukabidhi tuzo kwa washindi wa michezo mbalimbali, Mgeni Maalum, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia alimpongeza Mheshmiwa Spika kwa kubuni wazo la Bunge Bonanza.

Alisema wazo hilo la kuanzisha Bunge Bonanza linaunga mkono jitihada za Mheshimiwa Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan za kukuza michezo na kupambana na magonjwa yasiyoambukiza.

“Sisi kama Shirikisho tumekuja hapa kwa ajili ya jambo hili muhimu, uwepo wangu nimewawakilisha viongozi wengine wa michezo yote iliyofanyika hapa, nimekuja hapa ili kuonyesha ushindani katika tamasha hili ambalo linashindanisha timu kongwe za jadi, hongereni sana,” alisema.

Alisema TFF inajivunia mafanikio iliyoyapata ambayo yametokana na wadau mbalimbali ikiwemo Wabunge kwa kuweza kupitisha miswada mbalimbali iliyofanikisha maendeleo ya michezo nchini.

“Bado tunawategemea Mhimili wa Bunge, tunaomba ushirikiano wenu katika mchezo wa mpira wa miguu na michezo mingine,” alisema.

Aidha, aliahidi kushirikiana na Bunge katika ujenzi Shule ya Sekondari ya Wavulana pindi muda utakapofika wa kufanya hivyo katika jambo hilo muhimu kwa jamii.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bunge Bonanza, Mheshimiwa Festo Sanga mbali na kuwashukuru washiriki wote wa Bonanza hilo, alisema dhima yake ni



Mashabiki wa Timu ya Simba wakikabidhiwa kombe na Spika wa Bunge Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson** kombe la washindi wa Jumla wa Azania Bunge Bonanza



kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kuhamasisha michezo na kampeni ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza.

"Tunatamani kuendelea kulifanya Bonanza hili kuwa moja ya bonanza kubwa zaidi hapa nchini, tarehe 12 Aprili, 2025 tunakusudia kufanya Bunge Marathon kwa mara ya pili kwa lengo la kuchangia ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Bunge.

Alizishukuru taasisi mbalimbali na viongozi kutoka timu mbalimbali nchini kwa kuwaunga mkono kwa kushiriki Bonanza hilo lililokuwa na Kauli Mbiu 'Utani Wetu, Umoja Wetu'.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Azania,Bi Esther Mang'enya alisema Benki hiyo inathamini umuhimu wa Bunge Bonanza katika kuimarisha afya.

"Sisi tumeona ni muhimu kurudisha faida kwa jamii kwa sababu tunajua umuhimu wa afya Azania inafanya



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimwa **Kassim Majaliwa** na Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. **Tulia Ackson** wakiwaongoza Wabunge, Watumishi na Washiriki wengine mbalimbali kushiriki katika Azania Bunge Bonanza

biashara na wateja wote, wateja wadogo, wateja wa kati na wateja wakubwa, vilevile tunayo akaunti maalumu ikiwemo akaunti ya wanawake," alisema.

Baadhi ya michezo iliyoshindanishwa katika Bonanza ni pamoja na mchezo wa mpira wa miguu, mchezo wa mpira kikapu wanawake na wanaume, mchezo wa mpira wa wavu wanawake, mchezo wa mpira wa pete wanawake na wanaume na kuvuta kamba wanawake na wanaume.

Michezo mingine ni mchezo wa mpira wa meza wanawake na wanaume, mchezo wa *'draft'* wanawake na wanaume, mchezo wa kurusha vishale wanawake na wanaume, mchezo wa '*pool table'* wanawake na wanaume na wanaume na mchezo wa karata wanawake na wanaume.

Mingine ni mchezo wa kurusha vishale wanawake na wanaume, mbio za mita 100, 1,500, 800 wanawake na wanaume, mchezo wa bao, mchezo wa kurusha tufe wanawake na wanaume, mchezo wa karata wanawake na wanaume, mchezo wa kukimbia na gunia wanawake na wanaume na mchezo wa kukimbiza kuku wanawake na wanaume.

Michezo mingine ni mchezo wa kunywa soda kwa haraka wanawake na wanaume, mchezo wa kula chakula kwa haraka wanawake na wanaume, mchezo wa kupita kwenye pipa wanawake na wanaume, mchezo wa kukimbia na kikombe chenye maji wanawake na



wanaume na mchezo wa kuruka kamba wanawake na wanaume.

Mingine ni mchezo wa kupiga danadana wanawake na wanaume, mchezo wa kuvaa soksi wanawake na wanaume, mchezo wa ingia toka wanawake na wanaume na mchezo wa kujaza maji kwenye chupa wanawake na wanaume.













Mashabiki wa Timu ya Simba na Yanga walivyochuana katika Azania Bunge Bonanza lililofanyika katika Viwanja vya shule ya Sekondari ya John Merlini, Jijini Dodoma













Mchuano wa mashabiki wa Simba na Yanga katika michezo ya Azania Bunge Bonanza iliyofanyika katika Viwanja vya shule ya Sekondari ya John Merlini, Jijini Dodoma






**Jarida hili limeandaliwa na:** Ofisi ya Bunge, 10 Barabara ya Morogoro S.L.P. 941, 40490 Tambukareli, DODOMA.
**Nukushi:** +255 26234218 **Simu:** +255 26 232276-5 **Barua Pepe:** cna@bunge.go.tz


Bunge.tanzania Bunge la Tanzania Bunge_tv Bunge TV Tanzania www.parliament.go.tz